ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi – Tarehe 28 Febuari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali *PAC*): Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani ya Muhtasari wa Ripoti Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2016/2017.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 3

Utuoaji wa Bonus kwa Wafanyakazi wa SMZ

Mhe.Suleiman Sarahan Said -- Aliuliza

Kwa muda mrefu tumekuwa tukiiga mambo ya maendeleo kutoka nchi nyengine. Hata hivyo, hivi karibuni Rais wa Zanzibar, Dkt Ali Mohammed Shein ameamua kuwapa hidaya wazee wenye umri wa kuanzia miaka sabini kiasi cha Tsh 20,000/= kila mmoja kwa kila mwisho wa mwezi, jambo ambalo ni mfano wa kuigwa na nchi nyingi duniani.

(a) Je, katika kubuni mipango mipya ya maendeleo ya nchi yetu, Serikali ina mpango gani wa kuwapa bonus wafanyakazi kila anaefikisha miaka 5 bila kujali kiwango cha elimu, cheo nk.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha suala hili ili kuwapa moyo wafanyakazi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako, na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kumjibu

Mhe. Suleiman Sarhan Said Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake swali lake nambari 3 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Awamu ya Saba chini ya uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, iliamua kutoa malipo ya shilingi 20,000/= kila mwezi kwa wazee wote wenye umri kuanzia miaka 70 na kuendelea. Ni kweli pia kwamba hatua hizi sio za kawaida miongoni mwa chini zetu nyingi duniani.

Mhe. Spika**,** kuhusu utoaji wa "*Bonus*" kwa watumishi, ni kweli kwa kawaida utaratibu unaotumika hautegemei elimu au cheo cha mtumishi, bali hutegemea uzalishaji wa Taasisi unaotokana na utendaji mzuri wa wafanyakazi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kufuatana na mipango yake ya maendeleo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina mpango wa kuwapa *bonus* wafanyakazi kila wanapofikisha miaka mitano kazini.

b) Mhe. Spika**,** kwa kuwa hivi sasa hakuna Mpango kama huo Serikalini, kwa hivyo, Serikali haioni sababu ya kuliharakisha suala hili. Badala yake Serikali imekuwa ikiandaa mipango mengine mbali mbali ambayo pia yenye lengo la kuwapa moyo watumishi wake, ikiwa ni pamoja na kupandisha kima cha chini cha mshahara kwa mara ya tatu ifikapo mwezi wa Aprili 2017 kutokana na kima cha sasa Shs. 150,000/= na kufikia mshahara wa Shs. 300,000/=. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba ilikwishafanya marekebisho ya mishahara kutoka Shs 100,000/= hadi Shs. 150,000/= na kuongeza maposho mbali mbali katika kipindi cha 2011 na 2014. Aidha Serikali inatekeleza jukumu la kuwasomesha watumishi wake na kuwachukulia dhamana ya mikopo wanayokopeshwa na Taasisi mbali mbali za fedha. Hatua hizo ni miongoni mwa jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha maslahi ya watumishi na kuwapa moyo watumishi hao. Ahsante.

Mhe.Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika na mimi namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mheshimiwa ni kweli lakini

swali langu linakuja kwamba binadamu yeyote akifanya kazi na akiwa anapata *bonus* inakuwa kitu kama ambacho kinamtia moyo zaidi. Mimi ningeomba kwamba angalau kila baada ya miaka mitano basi kutokana na utendaji wake wa kazi watu wale muwasaidie *bonus*, lakini kama miaka mitano unaona ni kidogo. Jee, hata kwa miaka kumi suala hilo haliwezi kutekelezeka.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora namuomba kumjibu Mhe. Sarhan swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe Spika, wazo la Mhe. Sarahan siyo baya ni zuri na linatizamika. Sasa jibu langu mama nimesema kwamba Serikali haina mpango huo kwa hivi sasa lakini basi waje tuangalie huko mbele tunakokwenda hali ikiruhusu Mhe. Rais hana tatizo kama tunavyomjua na kwa maslahi ya watumishi ya umma anakuwa pamoja na mambo mengine anajali sana. Kwa hivyo waje kuangalia huko mbele inshaallah Mhe. Rais atakavyolichukulia, lakini naamini kwamba kwa kuwa Mhe. Rais hata juzi alipoonana na sisi Wajumbe wza Baraza la Wawakilishi nilimsikia zaidi katika pamoja na mambo mengine kuhusiana na masuala ya maslahi ya watumishi wa umma, ni mheshimiwa ambaye anajali sana na matarajio yetu na hili napo pia ikifika wakati bila shaka kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu litakuwa halina pingamizi. Kwa hivyo tuacheni tupeni muda tuweze kuliangalia hilo nashukuru.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Nchi**,** Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa majibu yake mazuri sana ambayo ameyajibu na ndivyo hali halisi ilivyo.

Lakini mimi nilitaka nishauri mambo mawili pengine tukumbushane tu. Moja ni kwamba Mhe. Spika, hivi karibuni Serikali ilifanya utaratibu maalum wa kutiza *experience* ya wafanyakazi waliofanya kazi zaidi ya miaka 15 na tukawapandisha katika kiwango kizuri sana kiasi ambacho wale waliokuwa na *certificate* wengine wamewapita hata wenye *diploma* baada ya kupandisha vile. Sasa hivi kazi tunavyofanya wale wenye *diploma* ambao kiwango chao nao kimeonekana kama kimedumaa, nao tunawahesabu miaka hivi nao tuwapandishe kufikia kiwango angalau kizuri. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, Taasisi zenyewe zina utaratibu na hakuna matatizo hata kitakachowazuia chochote kuwapa motisha wafanyakazi wao, baadhi ya Taasisi hasa mashirika haya wanafanya hivyo baada muda fulani wakimaliza mwaka wanafanya sherehe zao wanawakabidhi zawadi mbali mbali hata katika Wizara ya Elimu, maskulini yanafanyika hayo. Sasa mimi nadhani sisi serikali wache tutizame uwezekano wa kufanya hivyo lakini pia la pili kila Taasisi, Wizara ina wajibu wa kuwapa pongezi wafanyakazi, hata kama hutompa *promotion* lakini angalau umuandike barua ya kumpongeza tu kumwambia unafanya kazi vizuri, nadhani hiyo itasaidia kupata motisha ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*).

Nam. 33

Utaratibu wa Matumizi ya Mifereji ya Nje ya Nyumba

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza

Katika Baraza la Nane la Wawakilishi Serikali kupitia Wizara hii ilitoa ahadi kuwa wananchi hawatolipa bili za maji kwa mifereji ya nje lakini hivi sasa wananchi wanatakiwa walipie bili hizo.

a) Je, Maagizo yepi ya Serikalini ni sahihi.
b) Kama ahadi hiyo imefutwa kwanini wananchi hawapewi taarifa mapema.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake nambari 33 lakini kwanza kabla ya kumjibu ninapenda kutoa ufafanuzi mbele ya Baraza lako Tukufu kwamba mifereji inayohudumia jamii *(Public stand pipes)* hailipiwi, Aidha naomba ieleweke ya kwamba Serikali inapozungumzia mifereji ya nje isiolipiwa ni ile tu iliyoidhinishwa na Mamlaka baada ya kupokea maombi kutoka kwa wananchi wa eneo husika na sio mifereji ya nje iliyowekwa na mtu kwa matumizi yake binafsi bila ya idhini ya Mamlaka. Hivyo ieleweke kwamba hakuna kauli zinazotofautiana kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, baada ya hapo sasa naomba kumjibu Mhe. Hidaya swali lake kama ifuatavyo:

a. Bado maagizo ya Serikali yapo pale pale ya mifereji ya nje iliyothibitishwa na Mamlaka kuhudumia jamii hailipiwi.

b. Ahadi hiyo haijafutwa na ndio inayoendelea kutekelezwa hadi sasa. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kw majibu yake mazuri, lakini ningependa nimuulize swali la nyongeza.

Mhe. Waziri tunafahamu kwamba wananchi wapata taabu sana juu ya suala la maji na sasa hivi Wizara imeweka hii bili ya kulipia maji kwa wananchi ambao wanaunga mifereji ya ndani. Je, Wizara haioni kwamba hili suala la kulipia maji kwa kila mwezi kwa mwananchi ni suala ambalo tunaweza kuwakwamisha kimaisha kutokana na hali kwa sababu tunajua kwamba wananchi hawa ni maskini na hali ni ngumu ya kimaisha, lakini tukilipa maji kila mwezi itakuwa kuna hasara kubwa kwa hawa wananchi. Kwa nini Wizara haiweki kiwango maalum kwamba mwananchi akishalipa hiki kwa ada yote ya kuunga mfereji iwe ndiyo basi na isiwe kila mwezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe.Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Naomba kwanza ifahamike ya kwamba kiuhakika hatulipii bali tunachangia na tunachangia gharama za uendeshaji na mambo mengine kusudi hayo maji yawe endelevu yapatikane kama dhamira ya Serikali ilivyo kwa wananchi wote, ukichukua mfano wa chupa nduchu ya milimita 500 unanunua Shs. 500/- ukipata 8 Shs. 4,000/- ni sawa ambazo unatakiwa kuchangia mwezi mzima kwenye Serikali.

Sasa ieleweke kwamba tunachangia na si kununua halisi, na tukisema kwamba isichangiwe itapelekea mpaka yale maji yasiwafikie wananchi kama ambavyo tunategemea. Sasa mimi niombe Waheshimiwa Wawakilishi tuwe na moyo huo na tushajihishane kwa wananchi wetu waweze kuchangia ipasavyo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri swali moja lenye (a) na (b).

Wakati anajibu suala mama la Mhe. Hidaya ametamka kwamba Serikali haijaondosha utaratibu wa kutokulipia mifereji ya nje ile ambayo imesajiliwa na Serikali au Mamlaka ya ZAWA, kwa bahati katika jimbo langu mimi nina mifereji miwili inatambulikana kisheria ya tangu asili na ambayo imesajiliwa. Moja uko kituo cha Polisi cha Ng'ambu na mmoja uko Kwalimsha kwa Mwalimu Mwita.

a) Mheshimiwa nataka niseme kidogo tu nitakapompa ushahidi Mhe. Naibu Waziri kwamba mamlaka inakwenda kinyume na maagizo na taratibu za Serikali za kutokulipia mifereji iliyosajiliwa yuko tayari kuomba radhi. *(Makofi)*

b) Ili kumthibitishia hilo nina *reference* ya Mamlaka ya ZAWA ambayo imelipiwa na mrefeji wake kwa sababu unatambulikana umeandikwa *zero* na risiti halali, namuomba Mhe. Naibu Waziri ajibu masuala haya. La kwanza yuko tayari kuomba radhi na la pili uthibitisho wa Taasisi ya Serikali ya kulipia huo mfereji wa Serikali unaotambulika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mheshimiwa Waziri mwenyewe naomba ujibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani Mhe. Ali Salum Haji (Kirova) swali lake kama ifuatavyo.

(a) Naendelea kusema mifereji ya nje iliyothibitishwa na Mamlaka ya ZAWA hailipiwi na mimi bahati nzuri ni mdau wa mifereji yote miwili ambayo Mhe. Ali ameizungumza. Mfereji wa Kwalimsha toka sisi wadogo mfereji ule upo na tunaweze kuhudumia, kama Mamlaka yangu inafanya hivyo maana yake inakwenda kinyume na utaratibu ambao Serikali imeridhia. Naomba niliseme hili wazi kwamba wanakwenda kinyume na utaratibu kama hivyo, mifereji yote iliyothibitishwa na ipo kwa muda mrefu, mifereji hiyo haiwezi kulipiwa na hata hiyo ya watu binafsi ambayo sasa hivi inahudumia watu kutokana na visima vyao kama umekuja ZAWA umefuata taratibu bado hailipiwi kama hawakufata taratibu ndio inayolipiwa. Naomba niseme hivyo.(*Makofi*)

(b) Alizungumzia swali la kwamba kwa sababu yeye anasema kama ana uthibitisho ya kwamba Mamlaka inalipisha mifereji hiyo, kama nilivyosema awali kama mamlaka inafanya hivyo inakwenda kinyume

na utaratibu wa Serikali kwa maana Wizara agizo hilo imelitoa. Kwa hivyo kukiri makosa si tatizo kwa sababu Mamlaka yangu imefanya kosa na mimi nitalifuatilia na kama hivyo ndivyo hatua nitazichukua, kwa sababu mimi ndiye msimamizi wa mamlaka hiyo kwa hivyo hatua nitazichukua kwa sababu hilo ndilo agizo la Serikali *(Makofi).*

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake Mhe. Waziri kwamba amesema mifereji ambayo inahudumia jamii ambayo iliyopo nje hakuna ruhusa ya kulipia. Lakini mimi nina ushahidi tosha katika Shehia ya Kilombero kuna mifereji mingi ya nje ambayo imeanzishwa kupitia mradi wa TASAF kabla ya sheria hii ambayo ukusanyaji wa kulipia maji, lakini wametakiwa tena Mamlaka ya Maji (ZAWA) imekuja kuwalipisha wananchi wa Shehia ya Kilombero waisajili upya mifereji ile. Jee, huu ni utaratibu na kama si utaratibu nyinyi kama Wizara mtawachukulia hatua gani. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe.Waziri majibu, Waziri mwenyewe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naendelea kujibu tena swali hili la nyongeza la Mhe. Asha Abdalla wa Jimbo la Kiwengwa...

Mhe. Spika: Waheshimiwa samahani kuna *echo* mungemuacha Mhe. Waziri akajibu ili akasikika vizuri majibu yake. Endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa kama ifuatavyo:

Bado naendelea kusema kwamba utaratibu wa Serikali na kauli ya Serikali mifereji ya nje iliyosajiliwa ndani ya Mamlaka ya ZAWA hairuhusiwi kulipiwa. Mifereji ya nje inayolipiwa ni ile ambayo haijasajiliwa ambayo ni ya mtu mmoja mmoja na wao kwa sababu wanatoa huduma kwa wananchi pia wakiripoti Mamlaka ikaisajili basi mifereji hiyo pia bado itakuwa hailipiwi.

Kama kuna suala hili naendelea kusema kwamba tushirikiane kwa pamoja kutambua hayo maeneo na mtwambie ili na sisi tuweze kufanya kazi zetu ipasavyo, kwa sababu kama ninavyosema sisi kama binadamu hatuwezi kujua maeneo yote wala changamoto zote ambazo zimeikabili Wizara kwa wakati mmoja tukazijua.

Lakini kama zipo basi mimi naamua kuzibeba na naamua kuzifanyia kazi na hili sisemi tu kwamba maeneo tu mawili ambayo yametajwa hapo, naomba nitamke rasmi na wananchi wanisikie kama, kwamba kuna maeneo yenye matatizo kama hayo basi naomba aturipotie ili tuweze kufanya kazi ipasavyo. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe.Waziri kwa majibu Katibu kwa Wizara inayofuata.

Nam. 79

Matumizi ya Bonde la Mpunga la Tibirinzi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kuwajali sana wananchi wake na hasa pale wanapofikwa na maafa au maharibiko ya msimu wa mavuno na mambo mengine. Katika bonde la Tibirinzi kuna mashamba yaliyokua yakilimwa mpunga na sasa mashamba hayo kutokana na mabadiliko ya tabia za nchi yamekua kila kipindi yanaingia maji ya bahari na yanaonekana yatachukua muda mrefu kulimika tena.

a. Jee, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa fidia wakulima hao na mashamba hayo yakabakia Serikalini ili Serikali ikatafuta matumizi mengine.

b. Na kama Serikali itakubali kuwafidia, lini wananchi hao watafidiwa ili wapate kujielekeza kwenye shughuli nyengine.

c. Je, Serikali imefanya utafiti wa kina kwenye eneo hilo, kujua kama linaweza kutumika kwa matumizi gani ili kuondokana na hasara hizo za kila mwaka.

Mhe. Spika: Waheshimiwa tusikilizane kidogo maana yake kidogo kuna sauti zinakuja huku hatusikii majibu vizuri na Waziri atakuwa haisikii maswali yenu ya nyongeza. Tuendelee Mhe. Waziri

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarhan Said wa Jimbo la

Chake Chake swali lake nambari 79 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara inakiri kuingia maji ya bahari katika bonde la Tibirinzi hali hii imetokana na kuziba kwa mtaro pamoja na kuharibika banio la kuzuia maji ya bahari. Aidha, miundombinu hii ilijengwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwenye miaka ya 1990 kwa lengo la kuzuia maji ya bahari yasiingie katika eleo hilo, hivyo kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na uchakavu wa miundombinu hiyo hivi karibuni athari imejitokeza zaidi kwa asilimia 50% ya eneo hilo limeathirika kwa kuingiwa na maji ya bahari.

a) Mhe. Spika, ardhi ni mali ya serikai kupitia Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992 (hakimiliki ya ardhi kifungu Nam. 3) hivyo serikali haipaswi kutoa fidia kwa archi kinachotolewa fidia ni vilivyomo juu ya ardhi kama vile (mimea, majengo na kadhalika).

b) Mhe. Spika, wizara bado haijafanya utafiti wa matumizi mengine ya eneo hilo, aidha kutokana na wingi wa maji ya bahari yanayoingia katika eneo hilo ufugaji wa samaki unaweza kufaa.

Mhe. Spika, wizara ina mpango wa kuanzisha mabwawa ya kufugia samaki na kadhalika kutokana na kuwa na uwezo wa kuzalisha vifaranga vya aina nyingi ya mazao ya baharini. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika na nashukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Spika, nakubaliana na majibu yake lakini nataka kusema kwamba eneo lile sasa hivi ndio limekuwa kwa kweli limemaliza hadhi yake kwa upande wa kilimo. Sasa wananchi wameliona eneo lile sasa ni la kujenga nyumba ambalo watu sasa hivi wanaingia, nikisema maana hiyo ni kwamba serikali ikae tayari kuwavua watu kwa sababu sasa hivi eneo lile linaingia maji ya bahari na linaingia maji ya mvua. Sasa namwambia Mhe. Naibu Waziri kwamba pamoja na majibu yake lakini jee, huoni umuhimu wa bonde lile kuliweka mipaka ili wananchi wasilijenge na litumike katika kusudio ulilokusudia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, napenda kumshauri Mhe. Mwakilishi kwamba hili ni jukumu letu sote kwanza kuhakikisha wananchi hawajengi katika maeneo ambayo hatarishi, kwa sababu hii ni hatari kwa wao na sisi kwa ujumla. Mhe. Mwakilishi hili eneo tutalitembelea na kutoa taaluma kwa

wananchi athari za maji ya mvua kwa sababu hata wakijenga basi kazi itakuwa ni bure. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri maeneo yote ambayo kwamba yanatumika kwa kilimo ambayo yanaingia chumvi tukiacha kuyadhibiti na tukilenga zaidi kwenye ufugaji wa samaki hatuoni kwamba kilimo cha mpunga tunakiondosha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, mpunga unaendana na samaki, mtu hali wali bila ya kitoweo. Mabonde ya mpunga tunayo na hiyo sehemu unayosema imeingia maji basi si kama labda ni eneo lote ambalo tutachukua kwa kufugia samaki, lile ambalo eneo linaingia maji ya chumvi tunaweza kufanya ufugaji wa samaki, na lile eneo ambalo maji ya chumvi hayaingii basi tutaendeleza kilimo chetu cha mpunga kama kawaida. Nashukuru.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu lake mama alisema kwamba sababu ya kuingia maji chumvi ni kutokana na ubovu wa banio lilotengenezwa na Wizara ya Ujenzi. Jee, banio hilo hadi sasa haliwezi kutengenezwa jengine ili kunusuru maji hayo yasiweze kuingia katika sehemu hiyo ya Tibirinzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, ninapenda kumjibu Mhe. Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema hapo hata kama tutatengeneza hilo banio basi vile vile bado italeta athari, kwa hiyo ni bora au ni ushauri mzuri aidha kulima chumvi ama kufuga samaki. Ahsante.

Nam. 85

Kupotea kwa Kitalu cha Asili cha Mimea – Mwanafojo Chake-Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ilifungua vitalu vingi vya miche ya miti mbali mbali kwa nia njema na kwa kuendeleza maendeleo ya wananchi wake. Katika eneo la Chake-Chake Mwanafojo, kipo kitalu cha asili cha miaka mingi, kilichokuwa chachu ya wakulima kupanda miti kwa misimu yote. Hata hivyo, kitalu hicho kwa sasa hakina tena hadhi hiyo na maeneo hayo yameanza kuvamiwa kwa kujengwa nyumba za makaazi ya kudumu.

a) Je, kitalu hicho kimefikwa na matatizo gani mpaka kupoteza haiba yake ya zamani.

b) Je, eneo hilo la kitalu limepimwa na lina hati yake kuzuia uvamizi wa wananchi kufanya makazi.

c) Miche iliyokuwa ikizalishwa katika kitalu hicho ilikuwa aina nyingi sana kama mikarafu, minazi, michungwa, milimau, midimu na mengine. Je sasa hivi inazalishwa miche ya aina gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 85 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda nikubaliane na hoja ya mheshimiwa kuhusiana na serikali kufungua vitalu vingi kwa nia ya kuwaendeleza wananchi wake ikiwemo katika eneo la Mwanatojo, Wilaya ya Chake-Chake. Aidha, kitalu hicho cha asili cha miaka mingi bado kipo na kinaendelea kutoa huduma kwa wananchi na eneo lake bado lipo katika ukubwa ule ule lakini hapo zamani eneo hilo lilikuwa limegawiwa matumizi yake katika maeneo matatu.

Eneo la kwanza kwa uoteshaji wa miche ya matunda, eneo la pili kwa uoteshaji wa miche ya mikarafuu na eneo la tatu kwa uoteshaji wa miche ya misitu. Chanzo cha maji katika maeneo yote hayo kilikuwa ni mto uliopita karibu na maeneo hayo, hivyo kutokana na mabadiliko ya Tabianchi, mto huo umekauka

na wizara yangu ikalazimika kuchimba kisima katika eneo moja ambalo ndilo linalotumika kwa uoteshaji wa miche yote.

Baada ya maelezo ya jumla sasa napenda kujibu hoja hizo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, tatizo kubwa linalokabili kituo hicho ni uhaba mkubwa wa wafanyakazi ambao hawawezi kuotesha na kuilea miche mingi kama ilivyokuwa hapo zamani. Wakati huo kituo hicho kilipokuwa kikizalisha miche mingi ya aina mbali mbali, kilikuwa na wafanyakazi wapatao 27 na kwa sasa kituo kumebakiwa na wafanyakazi 10 tu ambao ni kidogo sana kulingana na kazi za kituo. Pamoja na tatizo la wafanyakazi, tatizo la maji kama tulivyolitaja hapo juu limepelekea kazi za uoteshaji wa miche kituoni hapo kuwekwa katika sehemu moja karibu na kisima ili kurahisisha upatikanaji wa maji hayo yanayotumika katika uoteshaji wa miche hiyo.

a) Mhe. Spika, eneo hilo tayari limepimwa kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira (*SMOLE*) na kuwekwa vigingi (*beacons*) kwa nia ya kulidhibiti na kuzuia uvamizi na kwa sasa tunasubiri kupatiwa hatimiliki,

   Aidha, eneo hilo halijavamiwa na maeneo yaliyojengwa au kutumika kwa shughuli nyengine yako nje ya kituo ambayo yanamilikiwa na watu binafsi.

b) Ni kweli kituo hicho kilikuwa kinazalisha miche ya miti ya aina mbali mbali lakini kwa sasa kimejikita zaidi katika uzalishaji wa miche ya mikarafuu kutokana na umuhimu wake kitaifa. Kama nilivyokwishaeleza hapo juu kwamba kituo kina uhaba wa wafanyakazi, hali hii ndio inayosababisha kupungua kwa uoteshaji wa miche katika kituo hicho. Hata hivyo, kituo ingawa kwa kiwango kidogo bado kinaendelea kuotesha miche ya minazi na michenza. Kwa upande wa miti ya misitu na matunda wananchi wanaendelea kupata miche hiyo kutoka katika vitalu vya Konde na Ole.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri naomba kumuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kitalu kile kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni kitalu kimoja wapo ambacho Wapemba tulikuwa tunakitegemea, suala zito lilikuwa suala la maji mpaka akachimba kisima, lakini eneo lile kwa ukarabati linaweza

likajengeka tena mto kutokana na mpango wake ulivyo kwamba maji yanaweza yakakauka mpaka yakafika kwamba hapana.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri haoni umuhimu wa kutengeneza ule mto ili ule mto ukaweza kubakisha maji ili yakaweza kuendelea na hiyo.

b) Ni kwamba anakiri kuwa wafanyakazi walioko pale ni kidogo na wameshindwa kutekeleza wajibu wao. Je, haoni umuhimu wa kuongeza wafanyakazi pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika,kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake yenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.)

a) Umuhimu wa kutengeneza mto upo lakini kwa bahati nzuri ama mbaya wenzetu tayari ZAWA wameshachimba kisima na wanatumia. Kwa hivyo yale maji ni vigumu sana kuja zake huku kwenye mto na kutokana na hali ya tabianchi.

b) Umuhimu wa kuajiri wafanyakazi pia huo upo na tayari tumeshafanya *application* lakini kutokana na Sheria ya Utumishi tunasubiri ruhusa itoke ndio tuweze kuajiri. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pia niipongeze Serikali yangu ya Zanzibar kwa kuona suala la kuweka vitalu katika kila sehemu yetu hii ya Zanzibar kwamba ni jambo la muhimu.

Mhe. Spika, katika Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja kuna kitalu ambacho kipo Kivunge. Mhe. Naibu Waziri hiki kitalu ambacho kipo Kivunge tunajua ni kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kaskani “A”. Lakini kitalu hiki mpaka sasa hivi hatukifahamu kipo kwa niaba gani kwa sababu kitalu kipo na kina baadhi tu ya miche, ila miche mingi kwa sasa pale haipo na hatujui ufanyaji kazi wake ukoje. Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Naibu Waziri utupe hebu kuhusu hiki kitalu kilichopo hapo Kivunge kipo kwa niaba gani, na wafanyakazi wake wanafanya kazi gani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema mwanzo vitalu ni vya miche tofauti, matunda, mikarafuu pamoja na miche mengine ya misitu. Kwa hivyo, hicho kitalu unachosema labda ungeniambia wafanyakazi hawapo, hawaji ama vipi. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Jee, serikali ina mpango gani kwa vikundi vya ushirika au watu binafsi ambao kuwa wanafanya shughuli hizi za vitalu kuweza kuwapa nguvu kifedha na kiutaalamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Serikali inawasaidia sana vikundi binafsi ambavyo vimeweka vitalu hivyo, kutokana na kwamba serikali miche ya mikarafuu kwanza inatoa bure wao wanauza mmoja 1000/- na kuna wengine mpaka 2000/-. Kwa hivyo, hiyo ni usaidizi tosha ambao unawasaidia kwa kifedha na utaalamu tunaendelea kuwapa kila siku. Ahsante.

Nam. 51

Pengo katika Usafiri wa Baharini

Mhe. Mussa Foum Mussa - Alijibu:-

Siku za karibuni meli ya MV. Mapinduzi II ilienda kufanyiwa matengenezo madogo katika bandari ya Mombasa – Kenya ambapo katika muda huo lilijitokeza tatizo kubwa sana la abiria kutopata usafiri kwa sababu chombo kilichokuwepo ni kimoja tu, MV. Azam Sealink.

(a) Je, Mhe. Waziri hili unalifahamu
(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza usafiri baina ya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu inalielewa hilo na serikali kwa upande wake ilichukua hali hiyo kama changamoto ya kuona ipo haja ya kuongeza huduma za usafiri wa baharini hususan kwa safari za Unguja na Pemba.

(b) Katika kuifanyia kazi changamoto hiyo, kama nilivyoeleza katika majibu yaliyotangulia, hivi sasa serikali inakamilisha taratibu za ujenzi wa meli mbili mpya, moja ikiwa ya mafuta na nyengine ni ya abiria na mizigo ambazo meli hizo zitachukua nafasi ya Meli ya MV Maendeleo ambayo kwa hivi sasa imechakaa na imo katika hatua za kuuzwa. Mradi huu wa ujenzi wa meli mpya unatarajiwa kutekelezwa mapema kabla mwaka wa fedha wa 2017-2018 baada ya taratibu husika kukamilika ndani ya mwaka huu wa 2016-2017.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kabla ya kustaafu kwake aliwahi kusema kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano iko tayari kutoa pesa ili kuweka meli nyengine ijapo kwa njia ya ubia. Jee, Mhe. Naibu Waziri suala hilo unalifahamu, na ikiwa unalifahamu jee limefikia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, napenda kumuarifu kwamba wizara inalifahamu suala hilo.

(b) Kama tunavyojua ahadi za viongozi wetu huwa zinaratibiwa. Kwa hiyo, hii ahadi tushairatibu na tumeshapeleka sehemu husika. Kwa hivyo tunasubiri pale hali itaporohusu basi nina imani kubwa sana Mhe. Rais Mstaafu kupitia sasa hivi Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambapo viongozi waliostaafu, lakini bado ipo pale pale basi nina imani kubwa sana ahadi hii itatekelezwa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba, kwanza tunashukuru Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kutununulia meli mpya na ya kisasa na nzuri sana.

Mhe. Spika, meli yetu ile ni nzuri sana tatizo lake kubwa ni milango, lakini katika matembezi yetu ya Kamati ya Mawasiliano tuliwahi kufikia Kampuni moja Mombasa kumuelezea kadhia ile ya milango, kwamba je, ina uwezekano wa kuweza kurekebishwa. Jibu wakasema kwamba wana uwezo kwa sababu wameshajenga meli nyingi katika uzoefu wao.

Sasa mimi nilikuwa namuuliza Mhe. Naibu Waziri je, upo utaratibu au nia ya kuipeleka meli ile kufanyiwa matengenezo katika sehemu za milango, na kama hakuna, uko tayari kwenda kufanya mazungumzo angalau kujua nini kinaweza kufanyika ili kukidhi haja ya wananchi katika meli ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Kiutaratibu meli yetu ya MV. Mapinduzi II imejengwa kwa *standard* za kimataifa, iwapo utabadilisha jambo dogo tu basi kuna hatari ya kuja kutokea kama yale yalivyotokea kwa MV. Skagit. Kwa hivyo, mimi namuomba sana Mhe. Mwakilishi akubaliane kwamba meli ile maumbile yake ndio yale na kama kuna changamoto kama tunavyosema kuna milango ambayo inatakiwa ifunguke, kwa bandari ya Mkoani mlango mmoja baadhi ya muda unakuwa unafunguka kutegemea na hali ilivyo ya *high tide* na *low tide*. Kwa hiyo, bado tutaendelea kutaka kutengeneza miundombinu lakini meli ile tutaiacha vile vile tusiharibu uzuri wake na umadhubuti wake. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi pia. Mimi ningependa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa meli hii ya MV. Mapinduzi imenunuliwa kwa bei ya fedha nyingi na kama kwa kutegemea usafiri baina ya Pemba/Dar es Salaam/Unguja bado itakuwa hailipi juu ya matumizi na pesa ambazo serikali yetu au fedha ambayo Serikali imetumia kununua kwa ajili ya wananchi. Ni lini serikali itaanzisha safari baina ya kwenda Dar es Salaam na Mtwara, Dar es Salaam na Tanga, Tanga kuja Pemba kwa ajili ya safari za ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Pia kuna mahitaji makubwa sana juu ya wananchi watakaotoka Tanzania hasa kutoka visiwa vyetu vya Zanzibar pamoja na wananchi wa Comoro. Je, serikali haioni umuhimu wa kuanzisha safari angalau kwa mwezi mara moja kutoka Comoro kuja Zanzibar pamoja na Dar es Salaam ili tuweze kunyanyua kipato chetu kwenye biashara hii ya usafiri huu hatima yake angalau wananchi wapate huduma na serikali iweze kupata pato bila ya usumbufu wowote. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri pamoja na kwamba ni swali jipya kama unaweza kulijibu nakuruhusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake kama ifuatavyo:

Ni kweli kabisa tunataka sana kuona MV. Mapinduzi II inakwenda maeneo aliyoyataja lakini kama nilivyosema hapo kabla tunataka kwanza kutengeneza miundombinu ili ile meli yetu ikienda pale kufunga gati, mfano Bandari ya Dar es Salaam au Tanga iweze vile vile kuchukua na mizigo, kwani biashara kubwa sasa hivi ya meli kama ile ni mizigo. Kwa hivyo tuko katika hatua hiyo.

Na kuhusu ushauri wake huu wa kutaka kwamba meli ya MV. Mapinduzi II kwenda mpaka Comoro na Mombasa ni ushauri mzuri na Mhe. Rais sisi ameshatuagiza tufanye kazi hiyo, na hivi karibuni kabisa tutapeleka serikalini hatua tuliyofikia kwa ajili ya kutekeleza agizo la Mhe. Rais. Kwa hivyo, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi na hilo ni agizo la Mhe. Rais. Ahsante sana mheshimiwa.

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kanuni ya 37 nathubutu kusema kwamba majibu ya Mhe. Naibu Waziri aliulizwa swali na akajibu kwamba hawako tayari kubadilisha chochote au kutengeneza milango katika meli ile ili kuondoa ubora wake.

Majibu ya pili anasema kwamba wako tayari kubadilisha milango ili iende kwenye soko iwe na uhakika, tukamate ipi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa mimi ningeshauri sana mkawa kimya sana wakati yanapotolewa majibu. Kwa sababu humu ndani mna tatizo la *echo* na mara nyingi sana Waziri anapojibu watu wengi huwa wanazungumza. Matokeo yake

ndio hayo unasikia jawabu mbili mbili. Tujitahidi sana kutunza nidhamu humu ndani kwa kuwa kimya ili tupate majibu mazuri.

Tunaendelea swali linalofuata lako wewe mwenyewe Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Nam. 54

Serikali kuuza Meli zake Chakavu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:

Pamoja na Shirika la Meli na Uwakala kuboreshwa upya na kuongeza tija kwa serikali, bado kuna changamoto za kuendesha meli chakavu, ambazo ni mzigo mkubwa kwa shirika hilo na kupelekea hasara ya mara kwa mara kwa kukarabati meli hizi zilizokwisha kupitwa na muda wa kutumika.

(a) Je, serikali ina mpango gani kuuza meli hizo za MV Maendeleo na MT. Ukombozi

(b) Je, serikali imejipanga vipi kuimarisha huduma bora za usafiri wa meli katika kukuza huduma za jamii, kiuchumi na kibiashara

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 54 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Meli ya MV. Maendeleo na MT. Ukombozi kwa pamoja zilinunuliwa mnamo mwaka 1980 na serikali zikiwa mpya kabisa kutoka nchini Japan. Kwa kuzingatia umri wa meli hizo ni ukweli usio shaka kabisa kwamba meli hizo sasa zimechakaa sambamba na hilo, kulingana na matakwa ya shirika linalosimamia masuala ya Meli Duniani (*I.M.O*), Meli ya MT. Ukombozi hivi sasa imepoteza sifa ya kufanya biashara kutokana na maumbile yake *(Single hull Ship).*

Kwa kuzingatia hayo na kama nilivyoeleza katika majibu yaliyotangulia, serikali imeamua kwa dhati kabisa kuziuza meli hizo ikiwa ni njia moja wapo ya kulipunguzia mzigo Shirika la Meli kutoka

uendeshaji wa shirika na pia kufuata maelekezo ya "*I.M.O"* katika uendeshaji wa meli za mafuta.

(b) Katika kuimarisha huduma za usafiri wa meli kutokana na kukua kwa huduma za kijamii, kiuchumi na kibiashara, serikali katika awamu ya kwanza imenunua meli mpya na ya kisasa ya MV. Mapinduzi II. Katika kuendeleza azma hiyo, hivi sasa serikali inakamilisha utaratibu wa ujenzi wa meli mpya ya abiria Meli ya MV. Maendeleo II pamoja na Meli ya Mafuta ili kukuza zaidi huduma za meli zetu hapa Zanzibar.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, pamoja na majibu yenye ukakasi, ni lini serikali itatangaza rasmi kuziuza meli hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba tutatangaza kuuza meli hizo mara tu utaratibu husika utapokamilika. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nitakuwa sijamtendea haki Mhe. Waziri wa Ardhi, Nishati na Mazingira kwa kujibu swali la msingi kwa umakini wa hali ya juu, nimpongeze kwa dhati kabisa ...

Mhe. Spika: Mheshimiwa uliza swali la nyongeza tafadhali usiende huko.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante unajua mnyonge mnyongeni haki yake mpeni kafanya kazi nzuri kujibu swali.

Mhe. Spika, nina maswali mawili ya nyongeza ni madogo sana..

Meli hiyo ya MT. Ukombozi imekodishwa kwa kampuni gani na imeshakusanya kiasi gani mpaka muda huu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali naona kama la kitakwimu sana lakini nakuruhusu ujaribu kulijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi makini wa Jimbo la Paje swali lake kama ifuatavyo.

Meli ya MT. Ukombozi imekodishwa kwa Kampuni ya *GAPCO* na kwa siku inalipa US$ 3300, kwa hiyo ni wastani wa US$ 100,000 kwa mwezi.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kununua meli mpya ya Mapinduzi II, lakini kuna changamoto ambazo zinajitokeza wakati wa kipindi cha Disemba na Januari kwa Shirika la Meli kuuza tiketi hizo mikononi zaidi. Je, wizara yake wanalijua hili, kama wanalijua ni hatua gani za kisheria ambazo zimechukuliwa ili kuondosha usumbufu kwa wananchi zaidi na tukiangalia meli hii ni ya serikali na ipo zaidi kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Viwe Khamis Abdalla kama ifuatavyo.

Ni kweli kuna kipindi cha nyuma kulitokea tukio kama hili na sisi tukachukua hatua ya kusimamisha baadhi ya mawakala wanaouza tiketi zile kupitia mapaparazi. Kwa hivyo, hivi sasa tumejipanga ili kuhakikisha kwamba tatizo hili halitokei, lakini pale itapotokea na tukagundua basi hatua kali za kisheria tutachukua kwa wale wote wanaovunja sheria zetu za usafiri baharini.

Nam. 26

Tatizo la Upatikanaji wa Dawa na Vifaa vya Uhakika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kumekuwa na ukosefu mkubwa wa vifaa muhimu vya matibabu kama vile *gloves*, *kenduler* ya *drip* na gozi za kuzuia damu ambapo hali hii inawapa wakati mgumu wagonjwa wasiokuwa na uwezo kununua vifaa hivyo katika maduka binafsi.

(a) Ili kutimiza azma ya Mhe. Rais ya kuwaondolea wananchi gharama kubwa za matibabu. Je, wizara imechukua hatua gani ya haraka ya kuondoa tatizo hilo kwa wananchi

(b) Je, kwa nini Hospitali ya Mnazi Mmoja upatikanaji wa dawa na vifaa umekuwa sio wa uhakika na kwa baadhi ya vituo dawa kupatikana kwa msimu kama embe inayozaliwa kwa msimu tofauti

(c) Kwa kuwa Hospitali hii inataka kuingia katika mpango wa kuwa Hospitali ya Rufaa, lini matatizo ya vifaa na dawa kupatikana nusu nusu yataondoka na kubaki historia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kutoa jibu hili naomba nifanye marekebisho kidogo kutokana na maelezo aliyoyatoa Mhe. Jaku Hashim, naomba nirekebisha kidogo. Mhe. Jaku alisema ukosefu mkubwa wa vifaa muhimu vya matibabu kama vile *gloves, kenduler* ya *drip*.

Mhe. Spika, kifa hiki cha *kenduler* katika hospitali zetu hatuna, lakini tunafikiri Mhe. Jaku Hashim alikusudia kusema *Cannula*. *Cannula* ni kifaa kidogo kama pini ambacho anawekwa mgonjwa kwenye mshipa baadae inawekwa *drip* ili kumrahisishia na kumuondoa maumivu ya kuingiza *drip* au sindano mara kwa mara katika mishipa yake.

Mhe. Spika, kwa sasa Hospitali ya Mnazi Mmoja haina ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi kama vile *gloves*, *cannula* pamoja na alivyoviainisha Mhe. Mwakilishi katika swali lake la msingi lenye kifungu (a). Hali hii ilikuwepo katika kipindi kifupi kilichopita, lakini serikali chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein ilihakikisha na kufanya kila lililowezekana na kuweza kuingiza bajeti kwa asilimia kubwa katika hospitali hii, kwa dhamira ya kupunguza na kuondosha kabisa baadhi ya changamoto na kuona wagonjwa wanaofika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja wanapata huduma zinazohitajika tena kwa wakati muafaka.

Mhe. Spika, upatikanaji wa dawa na vifaa katika hospitali zetu zote sa serikali na vituo vya afya ni wa uhakika na wizara yangu itakapoona kwa vyovyote vile utaratibu uliopo umekuwa ni kikwazo itatafuta utaratibu mzuri zaidi, ili kuhakikisha lengo la serikali la kufikisha huduma bora za afya kwa wananchi linafanikiwa na bila ya kikwazo chochote.

Mhe. Spika, ni kweli dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kufanya kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa na inafanya juhudi za makusudi ili kufikia lengo hilo kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Kwa kuongeza bajeti kila inapohitajika ili kuondoa tatizo la vifaa, dawa na kubaki kuwa ni historia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, na mimi nikubaliane naye Mhe. Naibu Waziri kwa umakini wa Dkt. Ali Mohammed Shein kuhusu Sekta ya Afya, hilo nalizungumza hata saa tisa usiku wakati usingizi umechanganya kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein katika sekta ya afya amejitahidi kupita kiasi. Lakini hii *mistake* ya *kendular* sio makosa yangu ni makosa ya Ofisi ya Spika, siyo makosa yangu katika *type*. Lakini tukubaliane hapa, pana ripoti ya Wizara ya Afya tumejadili juzi, haya si maneno yangu, naomba Mhe. Spika, kwa ruhusa yako niyanukuu:-

"Katika Hospitali ya Wazazi imebaini kuwa uhaba wa baadhi ya vifaa vya kuzalishia, uhaba wa baadhi ya watendaji muhimu, vifaa hivi vya kujifungulia kama mipira, *gloves* na vyenginevyo vinakuwa na upungufu".

Ndio yaliyomkuta Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto jana haya, tunajibu hoja akasema sisi ndio tunachokijua zaidi. Mhe. Hassan Khamis hapa akawa mkali sasa tukubali kipi?

Mhe Spika: Swali lako nini Mheshimiwa, mbona sijakuelewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe Spika, ripoti ya kamati inasema kuna upungufu yeye anakuja anasema hakuna upungufu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa tuko katika kipindi cha maswali ripoti ya kamati imekuja wapi tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, unajua hili ni Baraza sasa kuja kutaka kudanganya wananchi...

Mhe. Spika: Jibu analo basi naomba ukae atakujibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri ...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, lile lilikuwa la mwanzo tu, bado la pili.

Mhe. Spika: Subiri Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: La pili katika vituo ambavyo vimenituma mimi ambavyo vilivyonipa kazi ya kuja kuwatetea ikiwemo Jambiani, Kitogani, Bwejuu kuna upungufu wa dawa za *pressure* yaani inaitwa *aprinox, metformin*

na *amlodipin.* Vile vile kuna upungufu wa dawa za kisukari, lini tutafuatana mimi na yeye ili wananchi wetu wakaona kuwa tunafanya kazi pamoja mimi na yeye mguu kwa mguu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kaka yangu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kuhusu ripoti ilivyoeleza ripoti imesema kwamba bila shaka imeeleza kwamba ni matatizo ambayo yanatokea mara kwa mara na mimi nakiri kwamba tatizo hilo linatokea, lakini kwa hivi sasa tatizo hili katika wizara hatuna. Hilo ni swali la kwanza. (*Makofi*).

Kuhusu swali la pili la ukosefu wa baadhi ya dawa kama alivyoainisha kama dawa za *pressure* katika vituo hivyo ambavyo amevitaja na kunitaka lini niko tayari kufuatana naye. Kwanza nataka nimwambie Mhe. Jaku Hashim kwamba utaratibu wa uchukuaji wa dawa katika vituo vyetu uko na upo mzuri. Kwa hivyo, inawezekana tatizo la ukosefu wa dawa katika vituo ambavyo ameviainisha unatokana na uchelewaji wa watendaji wa kituo hicho kwenda katika Bohari yetu na kupeleka makisio kupatiwa dawa ambazo wanahitaji. Lakini nikwambie tu kwamba niko tayari wakati wowote kufuatana na yeye kwenda katika vituo ambavyo umesema.(*Makofi*).

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongea lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Na kwa sababu nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Afya kwa kupata *accreditation* ya maabara kuu ya Mnazi Mmoja. Swali langu liko hapa.

(a) Mpaka sasa maabara ile haifanyi *test* zozote zilizokuwa kubwa ni tatizo gani lililotukumba pamoja na kukosa *reagent* kwa muda huu.

(b) Kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja imeanza kuzidiwa ki-*population* na wananchi wengi na tumeelekeza kuzifungua hospitali kama za majimbo ikiwemo Mpendae, Kwamtipura na kwengineko. Jee, ni lini serikali itafanya vituo vile viweze kufanya kazi mpaka saa nne za usiku kama kituo kikuu cha Mpendae.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed swali lake la nyongeza lenye (a) na (b), lakini nitamuomba baadae arudie swali la (a), naomba nianze na swali la (b)

Ni kweli Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja imeonesha kuzidiwa. Hili linatokana na tabia kwa sababu serikali imejenga vituo mbali mbali ambavyo ni vya kuzalisha na vinatoa huduma pamoja na huduma ya uzazi na watoto, lakini watu wengi au wananchi hawapendi kuvitumia vituo hivyo niseme au wana wasi wasi au sijui wanaamini sana Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na mapungufu yote ambayo yanabainishwa, lakini bado Hospitali ya Mnazi Mmoja iko vizuri na wananchi wanapenda zaidi huduma za hospitali ile.

Jambo hili limepelekea Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa na mzigo mkubwa wa wagonjwa na haiwezekani mgonjwa katoka katika sehemu mbali Kwamtipura au wapi akafika pale, kama ni mzazi au ni mgonjwa wa kawaida baadae kwa sababu kule kipo kituo daktari akamwambia rudi katika kituo chako cha kijiji chako. Hilo haliwezekani inabidi tubebe mzigo atibiwe, kama ni kulazwa alazwe, kama ni kuzalishwa azalishwe, hili linasababisha sana Hospitali ya Mnazi Mmoja kubeba wagonjwa wengi na ndio maana hata bajeti pale haitoshi kadri bajeti itakavyoongezwa Hospitali ya Mnazi Mmoja bado itakuwa ni ndogo.

Mhe. Spika, naomba anisaidie katika swali la (a) sikulipata vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Mohamed Said Mohamed au Mhe. Waziri mwenyewe.

Mhe Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante sana nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri ambaye sasa ameshakuwa mtaalamu wa kubobea katika Wizara ya Afya kwa majibu yake mazuri. Na naomba nimpongeze Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa swali lake zuri sana alilouliza la kiufundi, lakini wakati huo huo naomba tupokee pongezi kwa kupata cheti hiki kinachotambulikana katika *SADC* juu ya maabara yetu pale Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, tatizo kubwa linalotukabili ni suala la *procurement.* Kampuni nyingi zinazo-*supply* vitendanishi (*reagent*) kwa ajili ya maabara hawataki ku-*supply quantity* ndogo ndogo na sisi kwa sababu ya udogo wetu huwa tunanunua *quantity* ndogo, wao wanataka ku-*supply quantity* kubwa.

Nitaomba nitoe mfano kwa lugha ya kawaida, wao wanataka tununue *drum* wakati sisi tunahitaji *gallon*. Sasa hapo huwa tunapata matatizo baadhi ya

wakati kwamba vile vifaa vinachelewa mpaka wale watu tunaonunua kwao wakubali kwa zile *quantity* ndogo na kuna *reagent* ambazo huwezi kununua kwa wingi ukaziweka kwa muda mrefu kwa sababu zitakuja kuharibika na ni hasara kubwa. Tulichokifanya hivi sasa katika kuboresha *procurement* yetu, tumemchukua mtu mmoja mwenye utaalamu wa maabara kukaa katika *central medical store* yaani ile Bohari Kuu ya dawa ili ashirikiane na wale wana Bohari kwa ajili ya kuagizia zile dawa, hilo tumefanikiwa.

La pili wiki iliyopita tu namshukuru Mwenyezi Mungu tumepata baadhi ya vitendanishi na sasa hivi *test* nyingi zinafanyika pale kasoro *test* mbili tu za *biochemistry* ambazo hazifanyiki, lakini *test* nyengine zote sasa hivi zinafanyika maabara ya Mnazi Mmoja. Na mimi mwenyewe nilikuweko leo asubuhi kulithibitisha hilo, kwa sababu nilikuweko maabara leo asubuhi saa mbili. Kwa hivyo, nashukuru sana naomba nilijuilishe Baraza lako tukufu, Mhe. Mohamed Said Mohamed pamoja na wananchi.

Ahsante sana Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, swali langu la kwanza alipokuwa akilijibu niliuliza jengine hakulijibu. Ni lini itakuwa tayari kufungua hospitali zile za majimboni mpaka saa nne ya usiku.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe malizia hilo jibu la swali.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante, nilifikiri ameridhika na jibu la Mhe. Naibu Waziri lakini nitaomba niongeze pamoja na majibu hayo mazuri.

Mhe. Spika, sasa hivi Hospitali ya Mnazi Mmoja tunataka kuelekea kwenye rufaa, lazima tukubaliane sote na *process* ya kuelekea kwenye rufaa ni ku-*strengthen* hizi *Primary Health Care Unit* pamoja na Hospitali ya Mpendae ya Mhe. Mohamed Said Mohamed. Sasa tutafika wakati huduma zote tunazozitoa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja itabidi unaingia pale getini Mnazi Mmoja itafika wakati huo, unaingia kwa *refer*, yaani daktari mwengine umeshindikana wewe kupata matibabu huko amekupa cheti anaku-*refer* kuja Hospitali Mnazi Mmoja kama wenzetu Muhimbili. Hospiali ya Muhimbili wao wameshaana huwezi kwenda bila ya kuwa na *refer file* ama cheti cha *refer,* yaani lazima uwe umeelekezwa na daktari mwengine ameandika kwamba wewe huku matibabu yako yameshindikana sasa hivi unatakiwa uende hospitali hii ya rufaa, tunaelekea huko.

Mhe. Spika, lakini tuna hofu kuelekea huko sasa hivi mpaka tuviongezee nguvu vituo hivi ambavyo Mheshimiwa amevitaja vituo vyote. Kwa hivyo, tunataka kuongezea nguvu upande wa wafanyakazi, hivi karibuni tunatarajia ku-*recruit* wafanyakazi wengi sana ambao tutawasambaza katika vituo hivi. Lakini pia tunataka kuongeza *shift* ili baadhi ya vituo sio vyote vituo kama 23 hivi kwa Unguja na vituo kama 18 kwa Pemba, viweze kufunguliwa kwa *shifting* pamoja na *shift* ya usiku yaani saa 24.

Kwa hivyo, hiyo ni *process* ambayo tutakwenda na katika kipindi hiki cha bajeti tutaomba bajeti ya kutosha ili tuweze kufanya hilo, kuelekea kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Rufaa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, afya ni muhimu sana katika maisha ya binaadamu, lakini kuna tatizo la uhaba wa madawa katika vituo vyangu vituo vilivyomo katika jimbo langu la Ziwani kama vile Wesha, Mbuzini na Ziwani na tulikwenda mimi na wewe kuvitemebelea vituo vile tukaona tatizo lile lililopo.

Je, limefikia hatua gani tatizo lile ili kulitatua kuhakikisha kwamba dawa pale zinapatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli tulikwenda mimi na yeye na tuliona upungufu mkubwa wa dawa katika vituo vyake. Lakini kama unakumbuka Mheshimiwa ilikuwa ni mwaka jana na mwaka jana nimekiri katika swali langu la msingi kwamba kulikuwa na upungufu katika Mahospitali yetu ya madawa.

Lakini katika kipindi hichi nakuthibitishia katika vituo vyako vyote vina dawa za kutosha. Mimi nilitembelea mwezi wa Januari mwisho na niliona kwamba dawa wanazo isipokuwa tu walikuwa wanamepungukiwa na baadhi ya dawa na ilikuwa kipindi chao cha kurudi kwenda kuchukua dawa waliniambia kuwa kimefika kwa hiyo wakati wowote walikwenda kuchukua dawa na kuzipata. Ahsante.

Mhe. Spika: Mheshimiwa nampa nafasi ya upendeleo jirani yake Mheshimiwa Kipole hapo.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya upendeleo.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya wagonjwa wanahitaji upasuaji na kazi hiyo inahitaji dawa ya ganzi na Hospitali ya Kivunge ina tatizo la dawa za ganzi.

Je, suala hilo litaondoka lini katika Hospitali ya Kivunge.

Mhe. Waziri wa Afya: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyengine na ninamshukuru Mhe. Mwakilishi kwa swali lake zuri sana la kuwatetea wananchi ambao wanatapa huduma katika Hospitali ya Kivunge na naomba niseme kwamba hata Mhe. Rais anatambua kwamba sasa hivi Hopsitali ya Kivunge inatoa huduma kwa Mkoa mzima si Wilaya tu inatoa huduma kwa Mkoa mzima na inafanya vizuri sana. Hivi karibuni Mheshimiwa atakuwa anajua kwamba tumefanya mabadiliko makubwa sana pale Hospitali ya Kivunge kwa kubadilisha baadhi ya *staffs* na tumempeleka mtu wa ganzi tatizo ilikuwa mtu wa ganzi au wa kutoa fahamu daktari yule hapatikani pale alikuwa anakwenda mara moja kwa wiki.

Lakini sasa hivi tumeweka daktari pale saa 24 wa ganzi na tunaendelea kufuatilia kwa karibu sana utendaji wao upande wa ganzi na upereshen zinazofanywa pale na yote ni kuipunguzia mzigo Mnazi Mmoja. Kwa sababu idadi ya watoto wanaotoka ama wazazi wanaotoka Kivunge kuja Mnazi Mmoja ni kubwa mno nimeshaeleza kwamba uzazi kule uko mzuri zaidi.(*Makofi*)

(a) Kuhusu dawa ya ganzi kutokana kupatikana kwa huyu mtaalamu tayari *stock* ya awali imepelekwa wiki iliyopita. Kwa hivyo, sasa hivi tunaendela ku-*monitor stock* ambayo inatumika pale kwa sababu dawa ya ganzi pia huwezi kupeleka kwa wingi. Dawa ya ganzi naomba Waheshimiwa Wawakilishi wanifahamu Mhe. Spika, dawa ya ganzi inatumika pia kwa masuala mengine nadhani mnayaelewa nikisema hivyo. Inatumika kwa masuala mengine dawa ya ganzi. Kwa hiyo hatuwezi inaingia katika *Dangerous Drug Act* (*DDA*).

Kwa hivyo, tunatakiwa tupeleke kiwango maalum kila baada ya wakati. Kwa hivyo sasa hivi dawa ya ganzi ipo Bohari na kila baada ya muda inapelekwa. Naomba Mhe. Mwakilishi akipata nafasi apite tena wiki hii kuangalia na kama kuna tatizo lolote awasiliane na sisi na tutalishughulikia mara moja. Ahsante. (*Makofi*)

Nam. 72

Ubovu wa vigari vya kubebea wagonjwa Hospitali

Mhe. Ali Khamis Bakar - Aliuliza**:**

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anastahiki pongezi kwa kujenga Hospitali nyingi nzuri Unguja na Pemba na kutoa huduma nzuri. Lakini hata hivyo kumekuwa na kasoro mbali mbali ikiwemo kutokuwepo kwa vigari vya kutosha vya kubebea wagonjwa vyengine vikiwa vibovu na vichakavu lakini pia kupasuka kwa bomba la maji machafu katika hospitali ya Mnazi Mmoja ambalo linahatarisha afya za watu.

(a) Je, lini vigari hivyo vitapatikana na kutoa huduma.

(b) Ni lini bomba hilo litazibwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza kabisa nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mwakilishi, kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anastahili pongezi na sio tu kwa kujenga Hospitali nyingi na kuboresha huduma za afya. Bali pa kwa uongozi bora na wizara na upendo kwa Wanzazibari wote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ni kweli sekta ya Afya inakabiliwa na changamoto ikiwemo ya kutokuwepo kwa vigari vya kutosha kwa ajili ya kubebea wagonjwa ambapo vilivyopo vingi ni vichakavu na vyengine ni vibovu. Hali hii inachangiwa na ongezeko la wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo wakiwemo wazee, walemavu, wagonjwa wasioweza kutembea, wagonjwa wa ajali n.k.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo mbali mbali inaendelea na juhudi za kutafuta, kupokea na kutoa vigari hivyo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa kutokana na mahitaji ya hospitali zetu.

Mhe. Spika, kufuatia ujenzi wa majengo mapya, uongozi wa hospitali, umekabidhiwa vigari 33 vya kubebea wagonjwa wa aina mbalimbali kwa *clinic* na wodi za majengo mapya ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi na wahisani mbali mbali waendelee kutusaidia kwa kutupatia vifaa hivyo kwa lengo la kutoa huduma kwa wagonjwa wanaohitaji. Aidha Serikali kupitia Wizara ya Afya imo katika mikakati ya kutengeneza na kukarabati miundo mbinu ya majengo ya Hospitali kila panapohitajika kwa ajili ya kupitisha vigari hivyo.

(b) Mhe. Spika, nakubaliana na kauli ya Mhe. Mwakilishi ya kupasuka kwa bomba la maji machafu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Ni kweli hali hii huwa inajitokleza katika hospitali yetu, lakini hurekebishwa na kwa sasa hakuna tatizo la aina hiyo. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Spika, kwanza naipongeza wizara kwa juhudi kubwa inazozichukua kutafuta wahisani ikiwa wanaunga mkono azma za serikali ya Mhe. Rais ili kuwaondolewa wananchi shida.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri wakati akijibu swali mama amesema kwamba wahisani wametoa vitendea kazi vikiwemo vigari na baadhi ya huduma ambazo wamezitoa. Ila amesema kwamba huduma hizi au vigari hivi vitagawanywa katika zile sehemu ambazo sasa hivi ni mpya kwa mfano *clinic* pamoja na wodi mpya.

Je, hizi wodi na *clinic* ambazo ni chakavu au ni kongwe mgao huu unaufikiriaje.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza nakataa kwamba sikusema kwamba vigari hivi vitagaiwa katika wodi mbali mbali. Naomba nirudie, kufuatia ujenzi wa majenzi mapya uongozi wa hospitali umekabidhiwa vigari 33 vya kubebea wagonjwa wa aina mbali mbali kwa *clinic* na wodi za majengo mapya Mnazi Mmoja.

Kwa hivyo, nakuhakikishia hivi ni kwa ajili ya Mnazi Mmoja lakini kutokana na juhudi zinazofanywa na wizara kutafuta vigari hivi zaidi tunakuhakikishia kwamba vikipatikana vitasambaa na kufika katika hospitali zako za Tumbe pamoja na hospitali nyengine. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba pia tutambue wiki iliyopita Taasisi ya Muz-dalfa wametupa msaada mkubwa sana wa hivi vigari ambavyo ndio kwamba tumevipokea vimeingizwa katika ule utaratibu wa serikali wa kupokea mali ambayo inakuwa ni mali ya umma baada ya hapo tutaanza kuvigawa na *inshaalla* Mheshimiwa kwake tutavipeleka. Kwa hivyo, tumepokea kutoka kwa Taasisi ya Muz-dalfa na tunaomba tuishukuru sana taasisi hiyo na tuitambue taasisi hiyo ya Muz-dalfa. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mimi bado naipongeza Wizara ya Afya kwa kuhakikisha kwamba inabeba jukumu kubwa kwa wananchi wetu wa Zanzibar katika sehemu zote za Mjini na Vijijini. Lakini kwa kuzingatia Hospitali ya Mnazi Mmoja hivi sasa ni Hospitali ya Rufaa na tunategemea kwamba katika kitu ambacho kinatakiwa kiwe karibu mafundi wa fani zote wawe tayari kuhimili tatizo lolote linalotokea.

> Je, kwa kuwa bomba lilipasuka ingawa limetengezwa hivyo mpaka linafika suala kuja kuulizwa hapa hawana mpango wa kuweka mafundi katika eneo hilo wa kudumu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja na baadhi ya hospitali zetu tunao mafundi wa fani mbali mbali na mara nyingi huwa wanapita na kuzunguka na kuona maeneo katika zile sehemu. Lakini inawezekana Mheshimiwa alipopita akaiona kadhia hiyo ilikuwa ni wakati limeshaonekana na wizara lakini tunatafuta njia ya kulifanyia ukarabati kwa sababu mabomba mengine huwa inabidi uyazibe lakini mengine huwa inabidi uondoshe kabisa uweke bomba jengine. Kwa hivyo, inawezekana kipindi alichopita Mheshimiwa ilikuwa ni wakati wa kutafuta uwezekano wa kuondosha bomba na kuweka jengine na kwa kweli hilo liliondoshwa na kuweka bomba jengine.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe muda bado tunao lakini maswali yameshakwisha. Sasa kabla hatujaendelea na hoja inayofuata napenda nitoe tangazo kwa Waheshimiwa wale walioko mkono wangu wa kushoto

mstari wa mwisho nimeelezwa na mafundi kwamba kuna tatizo la kiufundi katika *mike* zilizoko katika huo mstari wa mwisho.

Kwa hiyo, yeyote miongoni mwenu ambaye atakayekuwa na nia ya kuchangia wakati tutakapokuwa tunaendelea itabidi asogee angalau huu mstari unaofuata mbele yenu ili kuweza kuzungumza na asikike, mpaka hapo baadae, Litatuliwa tatizo hilo wakati mtakapokuwa mmetoka watu wote humu ndani ya ukumbi.

Baada ya tangazo hilo Waheshimiwa kutokana na idadi ambayo tayari wameshaomba sio kubwa sana kama jana ilivyokuwa. Maana jana wakati kama huu walikuwa tayari wameshaomba watu zaidi ya 10, leo mpaka sasa hivi wako watu 6 tu. Kwa hivyo, tutaendelea kuchangia kwa mujibu wa Kanuni. Lakini kama watu watazidi sana tutaangalia utaratibu wa kupunguza muda baada ya kuchangia robo saa, tuchangie dakika kumi kumi kwa sababu hii hoja inayoletwa sasa hivi ya Kamati ya *PAC* najua ni hoja ambayo inagusa sekta zote.

Baada ya tangazo hilo Katibu kwa shughuli inayofuata.

MUONGOZO

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante nikiri kwamba kwanza nilikuwa nataka utusaidie kwamba ripoti hii ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali Kamati ya *PAC* tulikabidhiwa jana sasa jioni na ripoti kwa kweli ni kubwa mno ina *page* 154. Ukweli hasa mimi mpaka sasa hivi binafsi nimefikia page 25.

Sasa najaribu kufikiria ndio maana hata katika michango ambayo uliokuja kwako hapo ni 6. Sasa mimi ningeomba kwa upande wako kama itawezekana utuahirishie Baraza mpaka jioni ili tuende tukaipitie hii ripoti ambayo ni muhimu sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante nashukuru Mheshimiwa lakini tunaendelea naukataa muongozo wako. Katibu tuendelee.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2016/2017.

Utangulizi:

Mhe. Spika**,** awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema katika kutekeleza majukumu yetu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu.

Mhe. Spika**,** aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma *PAC* uliolenga kwenye Ripoti nne za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama zifuatazo;

i. Sehemu ya Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014;
ii. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2013/2014;
iii. Sehemu ya Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (*CDF*) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi mwaka 2015; na
iv. Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika**,** naomba pia kutoa shukurani za dhati kwa Wizara, Mashirika, Taasisi zote za Serikali na Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa mashikiano makubwa waliyoipatia Kamati wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba.

Mhe. Spika**,** vile vile, tunatoa shukurani za pekee kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuiandalia mafunzo elekezi Kamati hii ili iweze kutekeleza vyema majukumu yake iliyopangiwa.(*Makofi*)

Mhe. Spika**,** pamoja na shukurani hizo, tunaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuitekeleza kwa vitendo ahadi iliyotolewa na Waziri wa Wizara hii mbele ya Baraza hili wakati alipokuwa anachangia Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo mnamo tarehe 23 Februari, 2017 ya kuipatia mafunzo Kamati hii hasa ikizingatiwa kuwa Sheria Mama zinazoifanyia kazi Kamati ya *PAC* zimetungwa upya hivi karibuni na Baraza la Wawakilishi, hivyo, ni busara Kamati hii ikapatiwa mafunzo hayo kuhusiana na Sheria hizo mpya haraka iwezekanavyo ili Kamati ya *PAC* izidi kutekeleza vyema shughuli zake.

Mhe. Spika**,** kwa namna ya pekee tunatoa shukurani zetu za dhati kwako Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza wakiongozwa na Katibu wa Baraza hili kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha kwa Kamati kwa kipindi chote cha kazi za Kamati.

Mhe. Spika**,** nitakuwa mkosefu wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati ya *PAC* kwa mashirikiano na kazi kubwa waliyoifanya ya kuzipitia na kuzichambua Ripoti za Ukaguzi na hatimae kutoa mapendekezo kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Serikali.

Mhe. Spika**,** naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya *PAC* kama ifuatavyo;

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Mjumbe
5. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
6. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
8. Mhe. Shehe Hamad Mattar - Mjumbe
9. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Mjumbe

Vile vile, kwa niaba ya Kamati yetu, natoa shukurani kwa Sekretarieti ya Kamati yenye watendaji wafuatao:

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu

2.	Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu
3.	Ndg. Wahida Mohamed Hafidh	-	Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti

Mhe. Spika**,** kwa hakika Sekretarieti hii imetoa mchango mkubwa sana katika kuhakikisha kuwa Kamati hii inafanya kazi zake bila ya usumbufu wowote.

Maeneo ambayo Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yalilenga

Mhe. Spika**,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Ripoti zake hizo nne alilenga kwenye maeneo yafuatayo:

1. Uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya ukaguzi;
2. Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi mbali mbali za Umma;
3. Ukiukwaji wa taratibu za malipo yaliyofanywa na Wizara na Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;
4. Hali ya Mashirika na Taasisi za Umma zinazojitegemea; na
5. Ukaguzi Yakinifu wa Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka Kwa Ajili ya Ukaguzi

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha Namba 12 ya mwaka 2005 pamoja na kifungu cha 8 cha Sheria hiyo, kila Wizara, Taasisi inayojitegemea na Mashirika ya Umma hutakiwa kuandaa na kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya ukaguzi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 baadhi ya Wizara na Taasisi zinazojitegemea na Mashirika ya Umma yameweza kutekeleza matakwa ya vifungu hivi ipasavyo. Hatua hii ni nzuri na inapaswa kupongezwa, kwani inadhihirishia umma kuwa Wizara, Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zimeanza kufahamu umuhimu wa jambo hilo.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo tulizozitoa, tunazitaka Taasisi za Umma kuendelea kutekeleza matakwa ya vifungu hivyo, kwani bado kuna baadhi ya Taasisi za Umma ingawa huhesabika kuwa zimewasilisha kwa wakati hesabu za mwisho wa mwaka, lakini, huwasilisha taarifa zao siku mbili au siku moja

kabla ya siku ya mwisho. Katika mwaka huo wa fedha, Taasisi zinazotakiwa kuwasilisha taarifa zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu sio zaidi ya tarehe 30 Septemba, 2014 ziliwasilisha hesabu hizo kama ifuatavyo;

- Taasisi 49 kati ya Taasisi 80 ziliwasilisha taarifa zao kabla ya tarehe 29 Septemba, 2014;
- Taasisi 7 kati ya Taasisi 80 ziliwasilisha taarifa zao tarehe 29 Septemba, 2014;
- Taasisi 18 kati ya Taasisi 80 ziliwasilisha taarifa zao tarehe 30 Septemba, 2014; na
- Taasisi 6 kati ya Taasisi 80 ziliwasilisha taarifa zao baada ya tarehe 30 Septemba, 2014;

Mhe. Spika, kwa upande wa Taasisi zinazotakiwa kuwazilisha taarifa zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu sio zaidi ya tarehe 30 Machi, 2014; ni Taasisi 1 tu iliyowasilisha taarifa zake tarehe 29 Machi, 2014 kati ya Taasisi 4 na Taasisi zilizobaki ziliwasilisha taarifa zao kwa wakati muafaka.

Mapato Na Matumizi Ya Wizara Na Taasisi Mbali Mbali Za Umma

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Toleo la 2016 Kamati ya *PAC* ina mamlaka ya kuchunguza hesabu za mwaka ya matumizi ya Fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za serikali na Asasi zake.

Mhe. Spika, cha kusikitisha Taasisi nyingi za Serikali zimekuwa zikiishangaa Kamati hii namna inavyotekeleza majukumu yake haya hususan pale inapohoji kwa upande wa mapato, matumizi ya kawaida na matumizi ya kazi za maendeleo. Mhe. Spika, tumebaini kwamba bado baadhi ya Viongozi wa Taasisi za Serikali wakiwemo Makatibu Wakuu wanahitaji kupatiwa taaluma juu ya utendaji kazi wa Kamati hii muhimu kwa maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Spika, tunadiriki kutamka hivyo kwa kuwa pamoja na maelekezo tunayoyatoa siku ya kuthibitisha ratiba bado baadhi ya Taasisi zinakuwa na uzito na nyengine kutowasilisha kabisa taarifa zake mbele ya Kamati hii kwenye maeneo niliyoyataja hapo kabla. Mhe. Spika, kutokana na kasoro hiyo, tunazitaka Taasisi za umma kwa siku zijazo kuwasilisha taarifa zake hizo kwa Kamati ya *PAC*, kwa kuwa Kamati hii hutekeleza majukumu yake kwa niaba

ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambalo lina mamlaka ya kuisimamia serikali kwa mujibu wa kifungu cha 5A(2) cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, sambamba na hilo, kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa Namba 4 ya 2007, Kamati za Baraza zina mamlaka ya kudai taarifa kwa mtu yeyote ambaye ana miliki taarifa husika pale zinavyohitajika. Hivyo basi, kitendo cha kuzinyima taarifa Kamati za Baraza ni sawa na kulinyima taarifa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, licha ya ugumu ilioupata Kamati hii kwa baadhi ya Taasisi wakati wa kufuatilia hoja ya mapato yaliyokusanywa na Taasisi husika, hata hivyo tumebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 kwa Taasisi tu zilizoorodheshwa katika ukurasa wa 26 hadi 28 wa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali takriban jumla ya Tsh. 1,826,669,000 hazikukusanywa kutokana na sababu mbali mbali.

Mhe. Spika, baadhi ya sababu zilizoelezwa ni pamoja na, kwa mfano;

i. Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

- Wawekezaji kuchelewa kulipa kodi zao na baadhi ya "*lease*" kufutwa;
- Kutokujitokeza kwa wingi waombaji wa hati na nyaraka nyengine za viwanja;
- Watu wachache wamejitokeza kununua nyumba za vijiji zilizokuwa zinauzwa kwa kipindi hicho;
- Uuzaji wa kokoto ulisita na badala yake viwanda vilikodishwa kwa watu binafsi.

ii. **Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto**

- Kukosekana kwa vitendea kazi, hasa vipando kwa Maafisa Ushirika kulipelekea Idara ya Vyama vya Ushirika kushindwa kusajili na kukagua Vyama vya Ushirika;
- Kushindwa kulipa gharama za vibali mbali mbali kama ilivyokadiriwa kikiwemo; Kibali cha kazi, Kibali cha kuongeza muda wa kibali cha kazi, Kibali cha muda mfupi, Kuridhia mkataba ya Wafanyakazi Wageni na vibali vyenginevyo.

iii. **Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

- Idadi pungufu ya watu waliojitokeza kupatiwa huduma ya usajili wa Kampuni, Vizazi, Vifo na Ndoa.

Mhe. Spika, kwa kuwa baadhi ya vianzio vya mapato ufuatiliaji wake sio wa kuridhisha Kamati ya *PAC* iliishauri Serikali kuhakikisha kuwa inavisimamia vyema vianzio vyake vya mapato pamoja na kubuni vianzio vipya ili nchi yetu iweze kutekeleza shughuli zake bila ya kuwategemea Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, ingawa baadhi ya Taasisi zilikusanya mapato yake kwa upungufu lakini pia, kwa mujibu ya Ripoti hiyo ya Ukaguzi katika ukurasa wa 26 hadi 28 zipo Taasisi ambazo zimekusanya mapato yake zaidi ya kile kilichokaridiwa kukusanywa na Baraza la Wawakilishi. Taasisi hizo zimekusanya takriban ziada ya Tsh. 1,640,614,000.

Mhe. Spika, tunazipongeza Taasisi hizo kwa juhudi hiyo walioichukua na tunazishauri ziendelee na jitihada zao hizo. Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati yetu inaamini kwa upande mmoja kuwa mafanikio hayo inawezekana kuwa yamepatikana kwa kuwa hakuna vigezo maalumu vya ukadiriaji wa mapato serikalini. Hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango hushindwa kuzikadiria Taasisi za umma kulingana na uwezo wake wa kukusanya na huonekana kama zimevuka malengo. Mhe. Spika, kwa mnasaba huo, tunaishauri Serikali kuwa na vigezo maalumu vya kukadiria mapato ili kuzibana zile Taasisi ambazo sio aminifu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sambamba na hayo, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa Vikosi vya SMZ huwasilisha Serikalini baadhi tu ya mapato yao wanayoyakusanya na endapo watakusanya zaidi, ziada ya fedha iliyopatikana hutumiwa na vikosi hivyo moja kwa moja.

Mhe. Spika, kwa kuwa mapato yote yanayokusanywa na vikosi hivi ni mapato ya umma, na kwa kuwa mapato na matumizi yote ya serikali yanatakiwa yawe yameidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Hivyo basi, Kamati ya *PAC* imependekeza kuwa mapato yote yanayokusanywa na Vikosi vya SMZ yaidhinishwe na Baraza kama Katiba inavyoelekeza ili kijulikane kiwango halisi cha mapato kinachokusanywa na Kikosi husika. Pamoja na kuainishwa ni kiwango gani cha fedha ambacho Kikosi husika kitawasilisha Serikalini ikiwa ni mchango wake na kiwango gani cha fedha kitatumia kwa ajili ya kuendeshea shughuli zake.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya kawaida, Kamati yetu imebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 matumizi halisi ya fedha za kawaida yamepungua kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Mawizara kwa mwaka husika katika ukurasa wa 30 hadi 32 wa Ripoti hiyo.

Mhe. Spika, tunaelewa kuwa fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha mishahara na maposho ya watendaji pamoja na matumizi mengineyo ya ofisi. Kwa kawaida fedha za matumizi ya mishahara na maposho ya watendaji hupatikana kwa asilimia mia moja, isipokuwa kwamba fedha za matumizi mengineyo ya ofisi hupatikana kwa upungufu, jambo ambalo limewapelekea watendaji wa Taasisi za Umma kushindwa kutekeleza majukumu yao kama walivyojipangia na Taasisi hizo huonekana hazitekelezi majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa msingi huo, tunaishauri serikali kuhakikisha kuwa inakuwa na idadi inayostahiki ya watendaji wake kwa kuwa asilimia kubwa ya matumizi ya kazi za kawaida hutumika kwa ajili ya mishahara na maposho kuliko matumizi ya uendeshaji wa ofisi. Mhe. Spika, tunashauri hili kwa kuwa tumebaini kuwa baadhi ya Taasisi za Umma zina watendaji wengi ambao hawatumiki kwa mfano; Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) pamoja na Mamlaka ya Vitega Uchumi (*ZIPA*).

Mhe. Spika, Kamati yetu imebaini kuwa Mfumo wa Matumizi ya Fedha za Pamoja (*Integrated Financial Management System – IFMS*) tangu ulipoanzishwa haujawahi kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, katika kujiridhisha na matumizi ya Serikali yaliyofanywa, tunamuomba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuufanyia ukaguzi mfumo huo.

Ukiukwaji wa Taratibu za Malipo Yaliyofanywa na Wizara na Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo

Mhe. Spika, Sheria ya Fedha na Kanuni zake na Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake pamoja na Sheria nyengine zimetungwa kwa ajili kusimamia taratibu za fedha na manunuzi ya Serikali. Hata hivyo, kuna baadhi ya Taasisi za Serikali zimekuwa zikikiuka matakwa ya Sheria na Kanuni hizo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 takriban matumizi ya jumla ya Tsh. 8,465,763,758 yaliripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa yamekiuka matakwa ya Sheria na Kanuni nilizozieleza hapo kabla kwa upande wa Mawizara ya SMZ. Ukiukwaji huu umetokea katika mazingira tofauti ikiwemo; kuwepo kwa matumizi yasiyokuwa na vielelezo, kutokutumika kwa bei iliyopangwa ya kukodishwa mali za umma na sababu nyenginezo. Mhe. Spika, kitendo hiki kinawavunja moyo wananchi wetu na hasa ikizingatiwa kuwa zipo Sheria ambazo zinatoa muongozo juu ya masuala hayo.

Mhe. Spika, licha ya Ripoti ya Ukaguzi kubaini mapungufu hayo, Kamati yetu imeridhika na baadhi ya matumizi yaliyofanywa baada ya kufuatilia kwa kina matumizi hayo. Kwa mfano; Kamati yetu baada ya kushindwa kupata taarifa za kutosha juu ya matumizi ya Tsh. 2,988,336,231.60 yaliyofanywa na Wizara ya Afya kwa njia ya *DUMMY* kuhusiana na malipo ya kuwasafirisha wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu zaidi pamoja na malipo ya Tsh. 3,185,912,534.91 yaliyofanywa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa njia hiyo ya *DUMMY* kwa ajili ya matumizi mbali mbali, Kamati hii ilifika Wizara ya Fedha na Mipango na kuridhika na maelezo pamoja na vielelezo ilivyopatiwa.

Mhe. Spika, Kamati yetu imebaini kuwa baadhi ya matumizi huripotiwa kuwa hayako sahihi kutokana na muda mfupi ambao Mkaguzi hutumia kufanya ukaguzi katika Taasisi husika, jambo hili husababishwa na uchache wa raslimali watu unaoukabili Ofisi hii. Vile vile, kukosekana kwa mawasiliano baina ya Mkaguzi na Mkaguliwa hasa kwa kukosekana kwa mkutano wa maagano '*Exit Meeting'* hupelekea Ofisi ya Mdhibiti kukosa baadhi ya taarifa. Mhe. Spika, tunadiriki kutamka hili kwa kuwa Taasisi nyingi zimeilalamikia Kamati yetu kuwa mkutano huo huwa haufanywi na Wakaguzi.

Mhe. Spika, katika kutatua kasoro hiyo, Kamati ya *PAC* inaiomba serikali kuiruhusu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuajiri watendaji ambao watasaidia kufanya ukaguzi ili kurahisisha shughuli hiyo. Mhe. Spika, tunashauri hili kwa kuwa katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2016/2017 ya Kamati hii ililipendekeza suala hili muhimu kwa maendeleo ya Ofisi hii, cha kusikitisha hadi leo hii hakuna uajiri wowote uliofanyika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa upande wa suala la Mkaguzi kutokufanya mkutano wa maagano baada ya kukamilisha ukaguzi wake, tunaishauri Ofisi ya Mdhibiti kumruhusu Afisa wake anaefuatana na Kamati hii wakati wa kazi za Kamati kuchukua kumbukumbu zitakazoonesha kufanyika kwa mkutano huo wa *Exit Meeting* na endapo watendaji wa Taasisi fulani watatoa tuhuma hiyo dhidi ya Ofisi ya Mkaguzi basi kumbukumbu hiyo iweze kutumika kama ni ushahidi dhidi ya tuhuma hiyo.

Mhe. Spika, sanjari na hayo, Kamati yetu imebaini kuwa hakuna utaratibu mzuri kuhusiana na malipo ya fedha yanayofanywa kwa njia ya *DUMMY*. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya nyaraka zinazohusiana na malipo husika zipo chini ya mamlaka ya Wizara ya Fedha na Mipango na nyaraka nyengine zipo chini ya mamlaka ya Taasisi husika. Mhe. Spika, kutokana na kasoro hiyo, tunaishauri Serikali nyaraka zote za matumizi ya jambo husika hata kama

linalipwa kwa njia ya *DUMMY* zihifadhiwe katika Taasisi husika hasa ikizingatiwa kuwa matumizi ya fedha hizo hutoka katika kifungu cha Taasisi hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sambamba na hilo, ili kuondosha utata kwa matumizi ya Serikali, tunaishauri Wizara ya Fedha kuachana na mfumo wa kuyatambua baadhi ya matumizi kwa jina la *DUMMY* kwa kuwa kila kifungu cha matumizi kina jina lake. Vile vile, tunaishauri Serikali kupunguza kiwango cha matumizi ya fedha yanayofanywa kwa njia ya *DUMMY* hasa ikizingatiwa kuwa mfumo huu unatia mashaka.

Mhe. Spika**,** Kamati ya *PAC* imebaini kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali hufanya mawasiliano na Serikali kwa kutumia lugha zinazotumika nchini mwao. Mhe. Spika, Kamati yetu ilipatwa na mshituko mkubwa baada ya kukabidhiwa nyaraka iliyoandikwa kwa lugha ya Kifaransa iliyotumika kwa ajili ya Mradi wa Uwanja wa Ndege unaosimamiwa na Kampuni ya *ADPi*. Kwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya ***PAC*** hawana uelewa na lugha hiyo walimtaka Mhasibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuieleza Kamati hii kilichoandikwa kwenye nyaraka iliyowasilishwa mbele ya Kamati, hata hivyo, mtendaji huyo alishindwa kutoa maelezo hayo. Kutokana na kasoro hiyo tulishindwa kujua kilichoandikwa kwenye nyaraka hizo zilizoandikwa tarehe 06 Februari, 2014 na tarehe 03 Oktoba, 2014 na Kampuni ya *ADPi.*

Mhe. Spika**,** ingawa kanuni ya 47 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 zimeruhusu kutumika lugha nyengine zaidi ya Kiswahili pale itakapolazimika, tunaishauri Serikali kuzitafsiri nyaraka zake ambazo zimeandikwa kwa lugha isiyokuwa ya Kiswahili au Kiingereza ili kuondosha usumbufu kwa watumiaji wa nyaraka hizo.

Mhe. Spika**,** tunaiomba Serikali kuyafuatilia kwa kina na kuyafanyia kazi mapendekezo yote ya Kamati ya *PAC* yaliyoelezwa kwenye ripoti ya Kamati hiyo.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Majimbo, Kamati ya *PAC* ilibahatika kufanya uchunguzi kwa majimbo 9 tu kati ya majimbo 50. Mhe. Spika, Mdhibiti na Mkaguzi alizifanyia ukaguzi Kamati hizi kuanzia mwaka wa 2011 hadi mwaka 2015, ambapo jumla ya Tsh. 60,000,000 ziliingizwa kwa kila Jimbo.

Mhe. Spika, kwa ujumla Kamati ya *PAC* imeridhika kwa kiasi kidogo na matumizi ya fedha yaliyofanywa na baadhi ya majimbo kutokana na sababu zifuatazo;

- Asilimia kubwa ya matumizi yaliyofanywa hayakuwa na vielelezo vya kuthibitisha matumizi hayo ingawa Kamati iliikagua miradi iliyotajwa;

- Kamati za Maendeleo ya Jimbo haitekelezi miradi ambayo imejaza kwenye fomu za maombi ya mradi iliyowasilishwa kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

- Kamati za Maendeleo ya Jimbo zilishindwa kuomba ridhaa kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pale inapobadilisha miradi;

- Kamati za Maendeleo ya Jimbo imetumia fedha za jimbo kwa ile miradi ambayo haikubaliki kisheria.

- Kwa yale majimbo yaliyokuwa na fedha za bakaa yalizitumia fedha hizo kinyume na utaratibu uliowekwa.

Mhe. Spika, sababu nyengine ni kama zinavyoonekana kwenye Ripoti yetu katika kila jimbo husika kwenye eneo la uchunguzi wa Kamati ya *PAC.*

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa kasoro hizo hazijitokezi tena katika awamu hii, Kamati yetu ilipendekeza yafuatayo;

- Kamati za Maendeleo ya Jimbo zitekeleze miradi ambayo imejazwa kwenye fomu ya maombi iliyowasilishwa kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hii ni kutokana na kuwa miradi hiyo hufanyiwa tathmini *"appraisal*" na Ofisi hiyo.

- Kamati za Maendeleo ya Jimbo ziombe ridhaa kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais endapo inahitaji kubadilisha miradi ili kuwa na uwiano wa taarifa wakati wa kuwasilisha ripoti sambamba na kufanyiwa tathmini miradi hiyo.

- Kamati za Maendeleo ya Jimbo zihakikishe kuwa inatumia fedha za jimbo kwa ile miradi inayokubalika tu kisheria.

- Kwa mujibu wa kifungu cha 8(4) cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Namba 2 ya mwaka 2012, Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ibaki na nyaraka asili *"original documents"* na nakala *"copies"* za nyaraka hizo ndizo zinazopaswa kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu - Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

- Kamati za Maendeleo ya Jimbo zisichanganyishe matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo na matumizi mengine yanayofanywa Jimboni hapo kama vile msaada anaotoa Mwakilishi, Mbunge, Diwani nakadhalika.

- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iendelee kutoa mafunzo kwa Kamati za Maendeleo ya Majimbo juu ya matumizi bora ya fedha hizo.

- Serikali ijitahidi kutoa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa wakati ili jimbo liweze kutekeleza miradi yake kwa wakati.

- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ihakikishe kuwa inafanya ukaguzi wa fedha hizi kila mwaka kama inavyofanywa kwa Mawizara, Taasisi na Mashirika ya Umma ili iweze kupata taarifa sahihi juu ya matumizi ya fedha hizo. Hii ni kutokana na kuwa kitendo cha kuchelewa kufanya ukaguzi kinawapelekea watendaji wa Jimbo kushindwa kukumbuka kila taarifa za miradi yao.

- Kwa kuwa tayari Sheria Namba 5 ya 2016 imeshapendekeza kuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Baraza la Mji na Halmashauri awe ndio Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ahakikishe kuwa anateua Wajumbe wa Kamati ambao wana uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iwajengee Ofisi za Majimbo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili Afisi hizo ziweze kutumika kwa kila shughuli ya maendeleo ya jimbo pamoja na kuhifadhi nyaraka mbali mbali zitakazotumika jimboni hapo sambamba na kuepusha usumbufu kwa wale watakaohitaji nyaraka yoyote.

Mhe. Spika, mapendekezo yetu mengine ni kama yanavyoonekana kwenye Ripoti yetu ya Kamati.

Hali Ya Mashirika na Taasisi za Umma Zinazojitegemea

Mhe. Spika, Kamati yetu imebaini kuwa Mashirika na Taasisi za Umma zinazojitegemea kwa asilimia kubwa zimepiga hatua inayoridhisha ukilinganisha na miaka ya nyuma. Kwa mfano, Benki ya Watu wa Zanzibar katika mwaka 2013 ilikusanya jumla ya Tsh. 28,513,741,595 wakati mwaka 2014 ilikusanya Tsh. 36,024,689,561. Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi Taasisi hii ilitumia chini ya mapato ambayo imeyakusanya katika miaka husika ambapo katika mwaka 2013, *PBZ* ilitumia Tsh. 21,469,485,244 na mwaka 2014 ilitumia Tsh. 25,348,749,056.

Mhe. Spika, mfano mwengine wa Taasisi inayojitegemea ambayo imepiga hatua ni Shirika la Utangazaji la Zanzibar *(ZBC)* ambapo mapato ya Shirika hili yameongezeka kutoka Tsh. 1,557,350,432 kwa mwaka 2012/2013 hadi kufikia Tsh. 1,835,771,397 kwa mwaka 2013/2014 kukiwa na ongezeko la Tsh. 278,420,965 sawa na asilimia 18.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi Shirika la Utangazaji la Zanzibar yameonekana kupungua kutoka Tsh. 967,338,554 kwa mwaka 2012/2013 hadi kufikia Tsh. 722,553,940 kwa mwaka 2013/2014 kukiwa na upungufu wa Tsh. 244,784,614 sawa na asilimia 25.

Mhe. Spika, tunazipongeza juhudi hizo za *ZBC* za kuongeza mapato, hata hivyo, Kamati yetu haikubaliani moja kwa moja na maamuzi yake iliyoyafanya ya kupunguza matumizi kwa kutokutekeleza baadhi ya shughuli zake ambazo ilitakiwa kuzitekeleza. Hivyo, tunazishauri Taasisi za Umma kuwa na mipango bora kwa maslahi ya Taasisi husika.

Mambo Yaliyobainika na Kamati Katika Taasisi Mbali Mbali za Umma Ambayo Hayakuibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Spika**,** kama tulivyoeleza kabla kuwa Kamati ya *PAC* ina mamlaka ya kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na Asasi zake. Vile vile, Kamati hii ina mamlaka ya kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati iliyotangulia kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2016. Hivyo basi, Kamati hii iliitumia haki yake hiyo ya Kikanuni kwa kufuatilia mambo mbalimbali na yafuatayo yamebainika:

- Serikali haijatoa muongozo maalumu juu ya namna ya kufanyika 4kwa punguzo la thamani *"depreciation"* kwa mali zake;

- Baadhi ya Taasisi hazina daftari la kumbukumbu za mali za Taasisi husika na Taasisi nyengine zinatunza kumbukumbu zao kwa njia ya elektroniki jambo ambalo linaweza likazipoteza kumbukumbu hizo kwa wepesi, endapo teknolojia hiyo itashindwa kufanya kazi;

- Baadhi ya Taasisi zinatumia *"pro forma invoice"* kwa ajili ya kufanya malipo;

- Mali za Serikali kama vile gari, nyumba, magofu huhamishwa kutoka Taasisi moja kwenda Taasisi nyengine bila ya kuwepo maandishi yoyote;

- Baadhi ya Taasisi za Umma hufunga mikataba bila ya kuishirikisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

- Wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti kushindwa kuyabaini baadhi ya mambo ambayo yapo kinyume na taratibu za fedha kwa baadhi ya Taasisi;

- Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatoi Hati maalumu za Ukaguzi kwa zile Taasisi zilizofanya vyema;

- Serikali kupitia vikao vyake mbali mbali vya Baraza la Mapinduzi huazimia mambo tofauti, kama vile, Wizara ya Fedha na Mipango kutakiwa kubeba madeni ya muda mrefu ya Taasisi fulani, hata hivyo, maazimio hayo hayatekelezwi ipasavyo. Mfano mzuri ni ulipaji wa deni la umeme kwenye vituo vya maji;

- Hakuna mashirikiano ya dhati kwa baadhi ya Taasisi za Serikali;

Mhe. Spika, kwa kuwa haya ni baadhi tu ya mambo tuliyoyabaini, hivyo, tunaiomba Serikali kuisoma Ripoti yote ya Kamati ya *PAC* kwa lengo la kuyazingatia na kuyachukulia hatua yale yote tuliyoyaainisha kwa maslahi ya nchi yetu na Taifa kwa ujumla.

Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

Mhe. Spika, kama inavyofahamika kuwa Mfuko wa Barabara umeanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Mfuko wa Barabara Namba 2 ya mwaka 2001. Lengo la kuanzisha Mfuko huo ni kushughulikia matengenezo ya barabara. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria hiyo, Mfuko wa Barabara unawajibika kuhakikisha kwamba mapato yanayokusanywa na Mfuko yanaingizwa katika hesabu ya Mfuko wa Barabara ambapo mapato hayo hayatoruhusiwa kutumika katika jambo lolote zaidi ya yale yaliyoainishwa katika Sheria hiyo na kuhakikisha kunakuwa na usimamizi, ufuatiliaji na utekelezaji wa matumizi mazuri ya fedha.

Mhe. Spika, kwa upande wake, Idara ya Ujenzi na Utunzaji Brabara (iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji kwa sasa) ina jukumu la kuzijenga na kuzitunza barabara za hapa nchini kupitia Wakandarasi wa ndani na nje ya nchi. Kazi za matengenezo ya barabara hufanywa na husimamiwa na Idara yenyewe kwa kutumia Wakandarasi wazalendo. Idara pia inasimamia uendeshaji na matengenezo ya zana nzito na mitambo ya ujenzi wa barabara zilizopo katika Karakana za Matengenezo ya Mitambo na Zana.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara ya mwaka 2013/2014, barabara zilizokaguliwa zilitengenezwa na iliyokuwa chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano zikijumuishwa na zile zilizotengenezwa na wakandarasi. Katika ukaguzi huo mambo ya msingi na ya kitaalamu yalizingatiwa ikiwemo:- upimaji wa viwango vya barabara, vigezo vilivyotumika na kupitia mikataba ya ujenzi wa barabara hizo. Madhumuni ya kufanya Ukaguzi Yakinifu ni kuhakikisha kwamba fedha inayotolewa kutekeleza miradi inatumika kwa ufanisi pamoja na kuleta tija kwa wananchi na kwamba matumizi yaliyofanywa yalizingatia hali ya uchumi na kuzingatia uwajibikaji katika matumizi ya raslimali za Umma.

Mhe. Spika,Kamati ya *PAC* iliifanyia kazi Ripoti hiyo ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2013/2014 kwa kufanya ziara ya kuikagua miradi mbali mbali iliyoainishwa katika Ripoti hiyo kwa Unguja na Pemba, ilifanya vikao na watendaji husika pamoja na kuzipitia nyaraka mbali mbali zinazohusiana na Miradi hiyo. Katika kutekeleza kazi hiyo Kamati ilifuatana na Mtaalamu maalum wa barabara, Mhandisi David William Bocco aliyepewa kazi na Afisi ya Baraza la Wawakilishi, ya kuisaidia Kamati kitaalam ili iweze kutekeleza kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, katika uchunguzi wake juu ya miradi hiyo, Kamati imebaini masuala mbali mbali ambayo kimsingi yanahitaji kufanyiwa kazi ili utekelezaji wa miradi mengine ijayo iwe na ufanisi zaidi katika kulinda nidhamu ya matumizi ya fedha, utendaji uliotukuka pamoja na kuleta tija zaidi kwa maslahi ya nchi yetu. Maeneo hayo yaliyobainika ni pamoja na;

- Matumizi ya taratibu za manunuzi;
- Uwekaji wa kumbukumbu za miradi;
- Uingizwaji wa fedha za miradi;
- Uchakavu wa vifaa vya kazi vinavyotumika katika ukarabati wa barabara;
- Mabadiliko ya kazi za miradi baada ya kuanza utekelezaji wake;
- Uteuzi wa wakandarasi katika miradi, viwango vinavyotumika katika miradi ya ujenzi wa barabara
- Usimamizi wa miradi iliyokwishakutekelezwa;
- Kukosekana kwa vielelezo wakati wa ukaguzi;

Uwekaji wa Kumbukumbu

Mhe. Naibu Spika, ninaamini Wajumbe wa Baraza lako Tukufu watakubaliana nami kwamba, kumbukumbu ni nyenzo muhimu katika utendaji kazi kwa serikali. Bila ya kuwa na kumbukumbu sahihi hatuwezi kujua tunakotoka na tunakokwenda na hivyo kushindwa kufikia maamuzi sahihi kwa wakati. Kumbukumbu hutumika kama kielelezo katika uwajibikaji na ni nguzo muhimu katika Utawala Bora. Ili serikali iweze kufikia lengo hilo na kuwezesha umma kujua mwenendo wa serikali yao, lazima kuwe na kumbukumbu zinazotunzwa vizuri na zinazopatikana kwa urahisi.

Mhe. Naibu Spika, kukosekana kwa taarifa sahihi na kwa wakati unaofaa kunaweza kuwafanya watendaji wa serikali kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo na hivyo kusababisha ucheleweshwaji wa maamuzi au kutolewa kwa maamuzi yasiyo sahihi na yasiyokidhi matarajio ya wananchi. Aidha, ukosefu wa kumbukumbu hutoa mianya ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, matumizi mabaya ya madaraka na hata kucheleweshe au kuzuia haki kutendeka. Kasoro hizi huchangia sana katika kuzorotesha maendeleo ya uchumi wa Taifa na hupelekea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu Serikali yao na Taasisi zake.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na umuhimu huo mkubwa wa uwekaji wa kumbukumbu, Kamati imebaini kuwa kuna udhaifu mkubwa katika uwekaji wa kumbukumbu za miradi. Aidha, Kamati imebaini kuwa kumbukumbu hizo

hazikuhifadhiwa katika mfumo wa kisasa wa kidigitali na zimo katika majalada mbali mbali. Kamati ilibaini kuwa ilikuwa ni vigumu kupata mchanganuo wa matumizi yaliyotumika wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na gharama za mafuta, ununuzi wa lami pamoja na malipo ya posho kwa watendaji walioshiriki katika miradi iliyotekelezwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, Kamati ya *PAC* ilishtushwa na kauli ya watendaji wa Wizara hii kuwa taarifa na vielelezo muhimu vya Miradi iliyopo Pemba, tangu hatua za awali hadi kutangazwa kwa zabuni, vimekuwa vikikosekana katika Ofisi ya Pemba kwa vile taarifa hizo huwekwa Wizarani (Unguja). Aidha, changamoto hiyo ya uwekaji wa kumbukumbu ilidhihirika hata wakati wa kikao cha Kamati na Wizara kilichopitia nyaraka za miradi iliyotekelezwa Unguja, ambapo nyaraka nyingi zilikosekana katika siku ya mwanzo ya kikao ijapokuwa nyaraka kadhaa zilipatikana katika siku zilizofuata.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hali hiyo, Kamati imeridhika na hatua inayochukuliwa na Wizara ya kuweka kila mradi katika jalada lake pamoja na hatua ya kutenga fedha kwa ajili ya kununua *"Server"* ili kuweka kumbukumbu katika mtandao maalum kwa kuwa mfumo huo wa kidigitali utaimarisha uwekaji wa kumbukumbu na kuepusha kumbukumbu hizo kupotea, kuharibika au kutoonekana kwa urahisi. Hata hivyo, serikali haina budi kutoa kipaumbele maalum katika utekelezaji wa bajeti yake kwa kuingiza fedha zitakazoweza kukidhi mahitaji ya uanzishaji wa mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu kwa njia za kielekroniki ili kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu hizo.

Matumizi ya Taratibu za Ununuzi

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 14(2) ya Kanuni za Manunuzi, Afisa Mas-uli amepewa uwezo wa kuidhinisha manunuzi ya bidhaa, kazi au huduma ambazo gharama zake ni sawa na Dola 10,000 za Kimarekani tu na si zaidi ya hapo. Hii inamaanisha kwamba kwa manunuzi yanayokiuka kiwango hicho cha fedha, Bodi ya Zabuni inayohusika inatakiwa ishirikishwe. Hata hivyo, Kamati imebaini kasoro kadhaa kwenye taratibu za manunuzi, kwa mfano, Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB) inapotekeleza shughuli za ujenzi au Ukarabati wa Barabara kwa njia ambazo gharama zake ni zaidi ya kiwango nilichokianisha, taratibu za manunuzi hazikuwa zikizingatiwa kwa kuwa UUB ilikuwa inakosa idhini ya Bodi ya Zabuni kwa ajili ya shughuli hizo za ujenzi.

Mhe. Naibu Spika, aidha, Kamati imebaini kwamba katika shughuli za ujenzi, gharama za vifaa au huduma ndogo ndogo ambazo jumla yake inapindukia kiwango cha idhini ya manunuzi kupitia Katibu Mkuu wa Wizara – hazikuombewa idhini ya Bodi ya Zabuni.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kasoro hizo Kamati iliitaka Idara ya UUB kuzifuata vizuri taratibu za manunuzi kwa kuitumia kikamilifu Bodi ya Zabuni inayohusika hata kwa ile miradi ambayo inatekelezwa moja kwa moja na Idara hiyo.

Uteuzi wa Wakandarasi

Mhe. Naibu Spika, Kamati imebaini kutofanyika utafiti wa kutosha wa kutambua na kuthibitisha uhalisi, sifa na vigezo stahiki vya wakandarasi wanaopewa kazi za miradi mbali mbali za ujenzi wa barabara hususan wakandarasi wanaotoka nje ya Zanzibar. Kasoro hii inaweza kusababisha athari nyingi ikiwa ni pamoja na udanganyifu na miradi kutotekelezwa katika kiwango kinachostahiki. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kufanya uchunguzi wa kina ili kuthibitisha kuwa Kampuni zinazopewa kazi za utekelezaji wa miradi mbali mbali ndizo halisi zinazostahiki kupewa kazi hizo ili kuepusha udanganyifu unaoweza kutokea.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa wakandarasi wazalendo, Kamati inatambua jitihada mbali mbali zinazofanywa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliaino na Usafirishaji katika kuwajengea uwezo wakandarasi wazalendo wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuwapunguzia masharti magumu ili waweze kushiriki katika Zabuni kama ilivyobainika katika Mradi wa ujenzi wa Ukingo katika barabara ya Amani - Mtoni pamoja na miradi mengine. Hata hivyo, Kamati ya *PAC* inaisisitiza Wizara kuwa mipango inayofanywa ya kuwajengea uwezo wakandarasi wazalendo wa Zanzibar kwa kuwapatia fursa za kazi inapaswa kufanywa bila ya kukiuka taratibu na sheria zilizopo.

Ukosefu wa Viwango vya Zanzibar Katika Sekta ya Ujenzi
(Design Standards Or Specification)

Mhe. Naibu Spika, suala la kuwepo kwa viwango katika sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya ujenzi ni jambo muhimu sana kwa nchi yoyote ile duniani. Katika sekta ya Ujenzi viwango husaidia sana katika kuandaa muongozo kwa shughuli za ujenzi, kuweka utaratibu katika njia, mbinu na pia katika mahitaji ya kitaalamu, mambo ambayo hujenga mazingira salama na endelevu katika nyanja hii ya ujenzi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* imebaini kuwa Zanzibar haina viwango vyake katika sekta ya ujenzi wa barabara *(Design Standards and/or Specifications)* ambavyo vingeweza kutumika katika kazi za Miradi ya Ujenzi wa barabara. Hali hii imepelekea miradi yote ya ujenzi wa barabara kutumia viwango na vigezo vilivyotengenezwa Tanzania Bara *(Standard Specification)* vya mwaka 2000. Mwanya huu wa ukosefu wa viwango vya Zanzibar unaweza kuwakaribisha hata Wakandarasi wa nje wanapopata Zabuni za Ujenzi kutumia, viwango wanavyotaka wao ambavyo havina uwiano wowote na viwango vinavyotumiwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inaihimiza Serikali kuharakisha mpango wa kuandaa viwango vyake katika masuala ya ujenzi ili kuhakikisha kuwa kazi za ujenzi wa barabara zinazofanywa hapa nchini zinapimwa kwa kutumia viwango na vigezo vilivyotengenezwa Zanzibar badala ya kutumia viwango vya Tanzania Bara kama ilivyo hivi sasa.

Uingizwaji wa Fedha kwa Ajili ya Miradi ya Mfuko wa Barabara

Mhe. Naibu Spika, kama inavyofahamika kuwa chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko wa Barabara ni kodi ya mafuta ya dizeli na petroli ambapo kiasi cha Tsh. 100 hutozwa kwa kila lita moja ya mafuta hayo. Aidha, imebainika kuwa asilimia 85 ya fedha hizo hupelekwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na asilimia 15 hupelekwa Tawala za Mikoa. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto ya kuchelewa kuingizwa fedha hizo katika Mfuko wa Barabara. Vile vile, kodi yenyewe inaonekana kutokidhi mahitaji makubwa ya kazi za ukarabati wa barabara, hasa kwa kuwa kazi hizo hugharimu fedha nyingi.

Mhe. Naibu Spika, mtiririko mdogo wa fedha huchangia kwa kiasi kikubwa kuzorota kwa kazi nyingi za ukarabati wa barabara hapa nchini. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa mapato yanayotokana na kodi ya mafuta yanaingizwa katika Mfuko wa Barabara kwa wakati ili kuepusha uzorotoshaji wa kazi za ukarabati wa barabara unaotokana na uchelewaji wa fedha. Aidha, katika kukidhi mahitaji makubwa ya ukarabati wa barabara hapa nchini, Kamati inaitaka serikali kuandaa utaratibu utakaoiwezesha Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara bila ya kumuathiri mwananchi wa kawaida.

Uhaba na Uchakavu wa Zana za Ujenzi na Ukarabati wa Barabara

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ina jukumu pia la kusimamia uendeshaji na matengenezo ya zana nzito na mitambo ya ujenzi wa barabara zilizopo katika karakana za matengenezo ya mitambo na zana. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa idara hii inakabiliwa na uhaba mkubwa wa vifaa vya kazi. Vifaa vyenyewe ni pamoja na mtambo wa kutandazia lami (*paver*) ambao upo mmoja tu kwa Unguja na mwengine mmoja upo Pemba. Aidha, mitambo hiyo pamoja na zana nyenginezo zilizopo, zimekuwa ni chakavu na hivyo kupelekea kuchelewa kukamilika kwa kazi kutokana na kuharibika mara kwa mara kwa mitambo hiyo pamoja na kupungua kwa ufanisi na ubora wa kazi zinazofanywa. Kwa mfano, katika viwango vya unene wa lami katika barabara zilizojengwa, barabara ya Selem na *Kilo Road* zilizopo katika Wilaya ya Wete (Pemba) zilipangiwa kuwa na kiwango cha unene wa lami wa milimita 35 lakini kutokana na uchakavu wa mtambo wa kutandazia lami (*Paver*) kiwango cha unene wa lami katika baadhi ya maeneo ya barabara hizo kilikuwa ni milimita 20 tu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inatambua na kuthamini jitihada na mipango ya serikali ya kutaka kuimarisha utendaji kazi wa UUB ikiwa ni pamoja na kutaka kununua mtambo mpya wa kutandazia lami. Hata hivyo, serikali haina budi kutoa msukumo maalum katika eneo hili kwa kutenga na kuingiza fedha za kutosha kwa ajili ya kununua vifaa mbali mbali vipya pamoja na kuvifanyia matengenezo vifaa vinavyoharibika ambavyo hutumika katika kazi za ujenzi na ukarabati wa barabara ili kuepusha barabara zetu kujengwa chini ya kiwango na kuharibika katika kipindi kifupi tu baada ya kutengenezwa.

Usimamizi na Utunzaji wa Miradi Iliyokamilika

Mhe. Naibu Spika, ujenzi na ukarabati wa barabara na hasa barabara za lami unagharimu fedha nyingi. Aidha, ni jambo la faraja na kupongezwa kuona kuwa miradi hii ya ukarabati wa barabara pamoja na miradi mengine iliyokaguliwa na Kamati kutokana na Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara, imetekelezwa kwa asilimia kubwa kwa kutumia fedha zetu wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, inasikitisha kuona kwamba kinyume na juhudi za serikali za kuimarisha mtandao wa barabara hapa nchini, viko vitendo vingi vinavyofanywa na baadhi ya watumiaji wa barabara ambavyo vinachangia sana katika kuharibika mapema kwa barabara zetu. Baadhi ya vitendo hivi ni kuzidisha uzito wa magari, kujenga ndani ya hifadhi ya barabara, kuburura vitu

vizito barabarani kama vile nondo, nakadhalika, ni lazima tabia za aina hii zikomeshwe.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema sote tuweke umuhimu wa pekee katika kutunza raslimali hii kubwa inayowekezwa kwenye sekta ya barabara. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, vyombo vya usalama pamoja na mamlaka nyengine zinazohusika lazima wawe macho na wawachukulie hatua wale wote wanaojihusisha na makosa haya. Sheria zilizopo zisimamiwe bila kuogopa ili barabara zetu ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mitaro, Kamati ya *PAC* imebaini utupaji ovyo wa taka katika mitaro pamoja na mitaro yenyewe kuota majani na kuonekana kama haina mwenyewe, kama ilivyobainika katika mtaro ulio katika barabara ya Ole-Konde (Pemba). Aidha, Kamati imesikitishwa kuona bomba ya maji safi likiwa katika sehemu ya kiungio limepita kati kati ya mtaro wa maji machafu. Hali hii imeonekana katika Mtaro wa Bububu - Kijichi.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Idara ya UUB kushirikiana na mamlaka zinazohusika katika Wilaya na Shehia katika kuwashajiisha wananchi juu ya umuhimu na namna ya utunzaji wa mitaro hiyo kwa vile serikali imetumia gharama kubwa kuitengeneza. Aidha, Kamati inaiomba Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) kufanya uhakiki wa bomba za maji safi zilizopita katika mitaro ya maji machafu na kushirikiana na Mamlaka zinazohusika kuziondoa bomba hizo na kuzipitisha katika maeneo mengine kwa kuwa kuendelea kuwepo bomba hizo katika mitaro ya maji machafu ni kunahatarisha afya za wananchi wetu katika maeneo hayo.

Kukosekana kwa Vielelezo Wakati wa Ukaguzi

Mhe. Naibu Spika, kama inavyofahamika kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ipo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu cha 112. Aidha, utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii unaongozwa na Sheria ya Ukaguzi Namba 11 ya mwaka 2003 inayohusu uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Sheria ya Fedha Namba 12 ya mwaka 2005, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 9 ya mwaka 2005 pamoja na Sheria nyenginezo hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 26(5) cha Sheria ya Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2005 kimempa uwezo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwengine aliyeidhinishwa na Mdhibiti kuzipitia nyaraka mbali mbali za serikali katika muktadha wa utekelezaji wa kazi zake. Hata hivyo,

Kamati imebaini kuwa baadhi ya nyaraka hazikuweza kuonekana na Mdhibiti wakati alipokuwa akifanya ukaguzi wake katika miradi mbali mbali ya Mfuko wa Barabara wakati ambapo nyaraka hizo ziliweza kuonekana na Kamati ya *PAC* wakati ilipokuwa ikitekeleza kazi zake, ambapo kiutaratibu kazi hizo hufanywa baada ya Mdhibiti kukamilisha ukaguzi wake na kuwasilishwa Ripoti ya Ukaguzi huo hapa Barazani..

Mhe. Spika, wakati Kamati ilipoulizia suala hili la watendaji wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara, ilielezwa kuwa kasoro hiyo ilitokana na kutofanyika kwa vikao baada ya ukaguzi wa miradi hiyo *(exit meeting)* pamoja na muda mfupi unaotumika katika kufanya ukaguzi huo. Hivyo, Kamati inaziomba pande zinazohusika (Taasisi za Serikali na Ofisi ya Mdhibiti) kuhakikisha kuwa zinajitahidi kuziba mianya ya kasoro hizo ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutenga muda wa kutosha kwa Wakaguzi wake kufanya ukaguzi stahiki kwa ufanisi zaidi na bila ya malalamiko kutoka kwa watendaji wa Taasisi za Serikali.

Mhe. Spika, Kamati ya *PAC* ina imani kubwa kwa kasoro mbali mbali zilizoainishwa katika Ripoti ya Kamati zitachukuliwa hatua ya kupatiwa ufumbuzi. Hata hivyo, pamoja na kujitokeza kwa kasoro hizo, kwa ujumla Kamati inawapongeza sana viongozi na watendaji wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hususan watendaji wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kwa kazi kubwa na ngumu wanazozifanya za ujenzi na ukarabati wa barabara zetu. Ni matumaini ya Kamati ya *PAC* kuwa watendaji hao wataendelea na ari na kasi kubwa waliyonayo ya utendaji kazi ili kuhakikisha kuwa barabara zetu zinakuwa katika hali nzuri kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake.(*Makofi*)

HITIMISHO

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo machache naomba kumalizia muhtasari huu wa Kamati kwa kueleza kuwa, ili kuifanya bajeti yetu tunayoipitisha iwe na uhakika katika matumizi halisi basi ni vyema fedha zote zitakazoidhinishwa na Baraza hili zitumike kama zilivyopangwa (yaani kuwe na *discipline* ya matumizi. Lakini pia, Serikali iweze kusimamia vianzio vya mapato vilivyopo pamoja na kubuni vianzio vipya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sambamba na hayo, tunaishauri Serikali kuwachukulia hatua watendaji wote ambao kwa namna moja au nyengine wanakiuka matakwa ya Sheria zilizopo kwa maslahi yao binafsi. Mhe. Spika, kitendo cha Serikali kuendelea kuwa na muhali kwa watendaji hao kinadhoofisha uchumi na maendeleo kwa ujumla kwani nchi yetu itaendelea kuwa tegemezi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wayajadili na hatimae kuyapitisha Mapendekezo ya Kamati ya *PAC* kwa Serikali kwa lengo la kupatikana tija iliyokusudiwa.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja. Ahsante, *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* waheshimiwa wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono na sasa tutaanza kuichangia. Waheshimiwa wajumbe mpaka sasa watu ambao washaomba kuchangia ni karibu watu kumi na mbili ni watu kumi na mbili maana yake tukichangia robo saa kila mtu tutatumia masaa matatu kuchangia watu 12 lakini inaonekana kama watu zaidi watatakiwa kuchangia hii hoja na tunakusudia kuikamilisha leo hoja hii.

Kwa hivyo sasa naomba nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais aiangalie kanuni ya 58(6) ya muda ili tuitengue kanuni hii ili watu wengi zaidi waweze kuichangia hii hoja. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tafadhali.

KUWEKA KANDO KANUNI 58 (6) YA MUDA WA UCHANGIAJI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu wamejitokeza kutaka kuchangia hoja iliyo mbele yetu na kutokana na ratiba tuliyo nayo na tulivyokubaliana kwamba kila ripoti itapata nafasi ya siku moja kutokana na muda huu na kwa ratiba yetu ya Baraza inatubidi tuliombe Baraza lako tukufu tuweke kando kanuni ya 58(6) ambayo inatoa nafasi ya muda kwa wachangiaji ili badala ya kuchangia dakika 15 tuweze kuchangia kwa dakika 10 iweze kutupa nafasi nzuri ya wachangiaji wengi waweze kutoa michango yao.

Kwa hiyo, ningeliomba Baraza lako Mhe. Spika, tuweke kanuni hii kando ili badala ya muda uliowekwa na sasa Wajumbe waweze kuchangia kwa dakika 10 kwa kila mjumbe ataposimama.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana waheshimiwa wajumbe hoja imetolewa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ya kuweka kando ya 58(6) ambayo inasimamia muda kwa hiyo naomba niwahoji wale wote ambao

wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono yao, wanaokataa waliokubali wameshinda. Kwa hiyo, tunachangia kwa dakika 10 na moja kwa moja naomba nianza na mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimuite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf dakika 10.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika Assalamu Alleykum namshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kutujaalia uzima na tunasikitika sana kwamba dakika zimepunguzwa kwenye Ripoti ya *PAC* wakati *PAC* ni mambo ya mahesabu *page* 158 .

Nianze Mhe. Spika,...

Mhe. Spika: Endelea.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi nilianza kutoa maelezo madogo kwasababu kama tunavyoona vitu vyenyewe vizito lakini dakika kidogo, lakini ningeanza katika Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano kwa ufupi kabisa.

Hapa kwenye *page* ya namba 6 kwenye ripoti hii kunaoneshwa kwamba Kamati imesema hati za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi wa Shilingi bilioni tisa milioni mia tisa arubaini nane mia tatu hamsini na nane mia saba na sitini na mbili (9,948,352,762/=), hizi ukaguzi waliofanya wenyewe kamati kwamba hati za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni na hapa zimeelezwa kuna *TP* na masuala mengine ya *payment*.

Lakini ninachotaka kusema Mhe. Spika ningemuomba sana Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika hasa Waziri wa Fedha kwenye masuala kama haya ambayo bilioni tisa (9,000,000,000/=) kwenda bilioni tano (5,000,000,000/=) karibu zikawa *return* zake hazionekani au wakawa wanatoa sababu ambazo hazina msingi kwenye fedha kama hizi kukaribia bilioni tano (5,000,000,000/=). Hii inaonyesha dhahiri kwamba hapa kuna matatizo na matatizo yenyewe hakuna mengine zaidi kwamba kuna watu wachache wanafanya magendo ya kuiba hizi fedha kwa sababu kwenye bilioni tano (5,000,000,000/=) hizi karibu leo kamati inajibiwa hakuna *return* hata ya bilioni mbili na nusu (2,500,000,000/=) kwamba *return* zake hazionekani.

Mhe. Waziri wa Fedha tunamkubali na tukaanza kazi vizuri na masuala haya anze kuyaona kwamba bilioni tano (5,000,000,000/=) kwenye nini kwenye

Wizara ya Mawasiliano kuna bilioni tano (5,000,000,000/=), kwenye kifungu moja tu ukicha vifungu vyengine ambavyo risiti hakuna, *return* nzuri hazipo kwa mujibu wa sheria inavyotakikana. Ningeomba sana hawa wabadhirifu Mhe. Waziri wa Fedha kushirikiana na Serikali na hasa tunavyomfahamu Dk. Ali Mohammed Shein kwamba Rais muaminifu na yuko vizuri kwenye masuala haya katika kusimamia watu ambao hawafanyi kazi zao katika utendaji uliokuwa mzuri.(Makofi).

Mhe. Spika, ni fedha nyingi na nimepiga hesabu tu haraka haraka kwenye ripoti karibu kuna bilioni kumi na mbili (12,000,000,000/=) ukizipiga hesabu kwenye Wizara zote ripoti zake hawajatoa katika *return* zao haziko vizuri karibu *twelve billion shillings* (12,000,000,000), lakini sasa tutakwenda hivyo hivyo kiufupi ufupi kwa sabau hili suala zito. Lakini ukenda kwenye wizara hiyo hiyo ukiacha hizi bilioni karibu tano, kuna kampuni ya ADP ililipwa jumla ya T.Shs. milioni mia saba arubaini na saba mia saba tisini na nane mia mbili na nne na nukta kumi na nne 747,798,204.14, ikiwa ni malipo kwa ajili Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume kwa kipindi cha kutoka Agosti 2013 hadi Januari 2014, malipo hayo ni kwa mwaka mmoja tu milioni mia saba na arubaini na saba. Malipo hayo yalijumuisha *invoice* namba 5 na 10 mwezi wa Juni 2014. Kampuni hiyo pia ililipwa pia juma ya T.Shs. milioni mia saba na thamanini na nane (788,000,000/=). Huyu jamaa kalipwa fedha hizi kwa ajili ya ushauri wa *Airport Terminal Two* mpya lakini cha ajabu zaidi kwamba ushauri huu alioutoa ushauri gani wakati *airport* ile ilifeli mwanzo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, analipwa mtu karibu *one billion* kwenye ushauri wakati ushauri wake umefeli, *airport* ile mwanzo *terminal* ukaingalia hata kwenye *drawing*, mimi ninayo nishapata karatasi zangu nitakuja nazo. Ukiangalia *drawing* ya mwanzo na *drawing* hii mpya ni tofauti, *parking* za mwamzo za ndege zilipokuwa zitakiwa zikae kwa njia ya mbele, sasa hivi kumewekwa na pembeni kwa maana kwamba kulifeli ile sehemu ya *parking* za ndege kila kitu kinaeleza. Lakini mshauri huyu amelipwa hizi fedha kashauri nini wakati kitu kiko-*failure*, kitu ambacho kimesababisha Serikali hasara kubwa Mhe. Waziri wa Fedha ningekuomba sana pamoja na *CAG* hili suala mulisimamie hasa kwenye suala la *Airport Terminal Two*, hapa kuna madudu tena madudu ya kweli kweli na kama watu ambao waliofelisha suala hili, wachache ambao waliokuwemo kama kuna viongozi au watendaji, wakiwemo kama ma *contractor* Wachina ma- *consultant* pamoja na watu waliohusika na wizara hizi, basi serikali isimamie suala hili kwa kuwachunguza na kuwachukulia hatua, haiwezekani serikali ilipe deni la karibuni Dola milioni mia moja na ishirini na nane ukifanya *equivalent* ni Bilioni mia tatu mpaka sasa hivi, itadaiwa si chini ya miaka thalathini ilipe deni hili. Na kuna watu

wamesababisha hasara ndani ya hesabu hii leo unaambiwa mtu kashauri tu analipwa *over billions* ushauri wenyewe uko *failure*.(*Makofi*).

Mhe. Spika, tukenda katika suala jengine la Mkoa wa Kaskazini kwenye Idara Maalum na Vikosi. Kuna gari hapa ambayo imekodishwa. Gari hii wanasema wamelipa milioni ishirini na saba na laki tatu (27,300,000/=) ipo kinyume na utaratibu hakuna mkataba wala hakuna lolote, lakini cha ajabu kwamba kama wizara inahitaji gari kwa utendaji kazi wa Mkoa, gari hii ina thamani mpya *show-room* ukienda milioni arubaini na tano (45,000,000/=) ambayo wanakodi kwa sababu wanakodi hawajanunua mpya, ninia kukodi kwa mtu. Sijui wizara imeshindwa vipi kuweza kununua gari hii milioni arubaini na tano (45,000,000/=) leo inalipa kodi kwa mwaka milioni ishirini na saba na laki tatu (27,300,00/=) ni kitu ambacho unaweza kukifikiria ukaona kuna fedha za serikali zinapotea bure bure kwa watu ambao wanafanya hesabu kwa watu wanavyozitaka wao.

Lakini tukienda kwenye Wizara ya Afya. Wizara ya Afya kuna Bilioni karibu tatu (3,000,000,000/=) zimetumika kwenye kusafirisha watu, wagonjwa lakini *return* zake pia *failure*, ndio nikazungumza kuna *almost twelve billion to thirteen billion shillings* kwamba hazina *return* wakiulizwa hawana majibu kamili, wanarushiana mpira Wizara ya Fedha na Wizara ambazo husika. Leo Mhe. Waziri wa Fedha yupo ningemuomba sana suala hili lichunguzwe leo Billion 2.9 mtu anakuja kujibu kwamba hakuna *return* sijui kwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha akiendewa na yeye atasema ziko Wizara ya Afya. Lakini uzuri zaidi kwamba kwa taarifa hizi zilitolewa hapa kwamba Waziri wahusika wote walikuwa ni wapya hawa ni sio lakini wizara ziko pale pale. Ningeomba sana hesabu hizi za Bilion 2.9 watu waliosafirishwa hakuna *return ticket*, hakuna utapokwenda nje tiketi mtu unatakiwa ulete kopi ulisafiri kweli, umetibiwa lete risiti umetumia bei gari, ulizotumiwa wewe ulopewa bei gani hakuna *return*, hakuna risiti watu wameshafanya mambo yao na ndio maana tukija tukazungumza hapa mimi nilikuwa nizungumze kidogo kidogo maana ninao uwezo wa kuji *control*, lakini kwa masuala huwezi kuji-*control* watu wanakula fedha za serikali wachache na kwa nini wanachiwa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwenye ripoti hii moja tu Bilioni kumi na mbili hizi (12,000,000,000/=) zishakuwa zinaonekana zina madudu, halafu leo tuseme humu ndani tuwambie watu kidogo kidogo hakwambili kidogo kidogo, kwa sababu kuna watu wachache wanataka kuendeshwa kama mapunda sasa hivi wapigwe marungu, hatuwezi kwenda hivi kidogo dogo, fedha nyingi kama hizi kwenye ripoti moja tu mwaka 2013/2014 sikwambii hiyo itakayokuja.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kuna jengine kwenye upande wa SUZA. Hapa na hapa cha kushangaza hapa SUZA inaonekana hii SUZA yote ya mtu mmoja, ukiacha hivyo kuna kompyuta zimenunuliwa milioni mia sita (600,000,000/=). Kompyuta hizi kwenye mahesabu mtu unapoletewa hesabu zielezwe *computer* pieces ngapi, kompyta za aina gani kama kuna *printer*, kama kuna *scanner*, kuna kitu tuelezwe. Lakini leo tunaambiwa kompyuta tu milioni mia sita (600,000,000/=), tutafahamu kompyuta ngapi kompyuta gani. Hili ni changa la macho haya ni mambo ambayo ya watu wabadhirifu tunazungumza kila siku humu ndani ambao wanahusika kwa njia yoyote ile ndani ya Wizara wamo. Na mimi naomba sana tukenda katika suala jengine hapo hapo kwenye SUZA hiyo hiyo, Wizara ya Elimu hiyo vile vile katika uchunguzi wa Kamati ilibaini ukiukwaji wa taratibu za manunuzi uliofanya na Chuo aina ya *JEEP* ya mwaka 2012. *(Makofi).*

Mhe. Spika, *JEEP* hii imenunuliwa milioni sabini na tano (75,000,000/=) takriban mwaka 2012, lakini cha ajabu baada ya muda mdogo imeenda kufanyiwa *service* milioni ishirini na mbili (22,000,000/=) Dar es Salaam kwa ajili ya kubadishwa vi-*spare parts* vidogo vidogo. Lakini *at the same time* haijatoshwa kauziwa huyu huyu mwenye gari milioni tatu (3,000,000/=). *(Makofi).*

Mhe. Spika: Dakika moja imebakia Mheshimiwa

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Naam**!**

Mhe. Spika: Dakika moja imebaki.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Aah**!** Nilifikiria unaniambia nikae.

Ahsante Mhe. Spika, gari hiyo hiyo kauziwa mwenyeji milioni tatu (3,000,000/=), hivi tushajua Serikali kwamba kwanza washauri wanakuwepo wapi kwamba tukishajua gari aina ya *JEEP Range Rover* ni gari za *computerized*, kwa nini inafika hatua watu wananua gari hizi ambazo washajua *service* zake ngumu, na wizara kwa nini itumie magari ya ghali kama hivi milioni sabini na nne (74,000,000/=) kwenye Wizara ya Elimu. Halafu matokeo yake unaambiwa *service* imefanyiwa *twenty two million* ndio yale nilozungumza juzi kwamba hakuna haja ya viongozi kutumia magari ya fedha nyingi zipo gari *Suzuki, Rava Four* ziko za Dola elfu ishirini ($20,000) ambazo za bei nzuri, leo unataka kutumia gari Dola elfu hamsini ($50,000), dola elfu sabini matengenezo yake ndio hayo, hasara kubwa halafu watu wanauziana

milioni tatu tatu (3,000,000/=) hivi vitu vipo. Lakini mimi naamini Serikali inasikia na mambo haya kwenye hiki kitabu tu Bilioni kumi na tatu kwa kumi na nne hazina risiti hazina *return*.

Lakini Mhe. Spika, nakushukuru nishakusikitisha zaidi kabla sijai-*support* ripoti hii kuunga hoja nishaiunga hoja, lakini mara ya pili tunaomba dakika zetu ziwepo kwa sababu mambo muhimu na mengi yanajificha humu ndani.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, hoja hiyo ilipigiwa kura na wewe ulikuwemo humu ndani naomba ukae. Naomba ukae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mimi sija *support* kwa sababu siliungi mkono ninakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ndiyo umeshindwa kwa kura. Naomba ukae. Naomba sasa kumuita Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Zulfa Mmaka Omar ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata: Ahsante sana Mhe. Spika. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata nafasi hii kuchangia Ripoti ya Kamati Uchunguzi wa Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*).

Mhe. Spika, awali ya nyote nikupongeze wewe kwa kunipatia nafasi hii kwa kuchangia kidogo ripoti hii, lakini kwanza kwa dhati kabisa nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati, niwapongeze Wajumbe wote makini kwa kazi nzuri waliofanya humu walotupatia kitabu hiki na kutupa *data* halisi ambazo hazikuficha kitu. Lakini na haya ndio yanotakiwa Mheshimiwa lazima tuwe wawazi kabisa katika mambo yetu Serikali yetu ibane matumizi na kwenda kwa wananchi jambo ambalo tunalitarajia sana kwa maendeleo yetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kufungua ukurasa wa 53 Mahkama Kuu. Mahakama Kuu Mheshimiwa naomba ninukuu kidogo.

Hoja namba 13.31 "Taarifa ya Mapato 2013/2014. Ukaguzi umebaini kwamba Mahakama Kuu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilikadiriwa kukusanya jumla ya Tanzania tisini milioni (90,000,000/=) na hadi kufikia Juni, 2014 ilifanikiwa kukusanya Tanzania shilingi mia moja sitini na tano milioni, mia saba hamsini na mbili elfu (165,752,000/=) kukiwa kumeongezeka lengo la sabini na tano milioni, laki saba na hamsini na mbili (75,752,000/=)". Mheshimiwa niwapongeze sana.

Lakini niwapongeze zaidi kwamba ni watu wa Mahkama watu wa wazi, wanafanya kazi zao ipasavyo kutoa haki kwa yule anayekwenda kutaka wajibu wa kuchangia pato hili, hasa katika kitabu hiki wamejieleza wazi kwamba wao si wafanyabiashara, wao ni watoa haki kwa mwenye kutaka haki yake. Kwa hivyo nawapongeza kwa dhati kabisa kwa hili kwamba wao wafanya kazi zao kwa maadili yanayotakiwa na nchi yetu.

Lakini jengine Mhe. Spika nije katika taarifa ya matumzi ya kazi za kawaida za mwaka 2013/2014 taarifa 13.3.2, taarifa ya matumizi ya kazi za kawaida, ukurasa huo huo. Ukaguzi umebaini kuwa Mahakama Kuu ilikadiriwa kutumia kwa kazi za kawaida jumla ya Tanzania sh. 3,583,000 na hadi kufikia mwaka 2014 imefanikiwa kutumia bilioni 4,100,149,000 kukiwa na ongezeko la Tsh. 517,149. Naomba hapa nije nipatiwe maelezo paliongezeka kwa kitu gani, tunataka ule uwazi wenyewe upatikane.

Mhe. Spika, lakini jengine katika ukurasa wa 3 Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Mhe. Spika, taarifa ya mapato, mimi nakuja kwenye mapato tu kwa sababu ndio uhai wa nchi yetu. Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi umekadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 748,000,000 hadi kufikia Juni, 2014 ilikusanya jumla ya milioni 922,841,000, kukiwa na ongezeko la 174,841,000. Nawapongeza sana kwa hili. Mheshimiwa ni wajibu wa ubinadamu anayefanya vizuri mpongeze, aliyekuwa na kasoro kidogo mpe njia aongeze bidii ili awe kama wenzake. Kwa hivyo, naipongeza Wizara kwa kufikia hilo.

Lakini jengine Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 61 Shirika la Magazeti. Mheshimiwa nawapongeza sana vijana wetu hawa akiwemo Mkurugenzi na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hapa katika taarifa yao ukurasa wa 61 Shirika la Magazeti, hoja Nam. 13.1 mlinganisho wa mapato na matumizi kwa mwaka 2016. Taarifa ya mapato ni kwamba katika Shirika la Magazeti yameonekana kupanda kutoka shilingi 549,470,701 kwa mwaka 2012/2013, hadi kufikia shilingi 629,639,622 kwa mwaka 2013/2014 kukiwa na ongezeko la asilimia 80,168,921, sawa na asilimia 15. Mheshimiwa nawapongeza sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika, hasa nikizingatia mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Wizara hii nimeshuhudia kazi zao wanazofanya na matatizo yanayowakumbuka. Bado naiomba sana serikali na taasisi zote zinazodaiwa na shirika hili wawalipe zaidi ili wafanye kazi zao vizuri, tumekuwepo hapa katika Baraza tunapiga kelele kwamba magazeti haya yanapigwa chapa Bara na tunataka yapigwe hapa. Kwa

hivyo, tuwape uwezo wa kufanya vizuri zaidi ili mambo yao yaende hapa hapa kwa ajili ya kupunguza gharama. Nalipongeza sana shirika hili.

Mhe. Spika, lakini jengine ninataka niseme kijumla tu, mashirika yote nayapongeza kwa kufanya vizuri, mashirika yote kwa ujumla, ukienda benki, bandari, uwanja wa ndege pamoja na matatizo ya hapa na pale lakine wamefanya vizuri. Mheshimiwa wajibu wetu tuhakikishe kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hayo waliyoyapata wenzetu wamebeba mzigo mzito sana, alisimama Mhe. Simai Mohammed Said hapa asubuhi akasema kwamba kitabu hiki mheshimiwa kikubwa kwa siku moja hakitoshi.

Mimi natoa pendekezo tu, natoa kama ombi mheshimiwa kupitia kwako ikija tena taarifa nyengine huko mbele tunakokwenda, *PAC* wapewe siku mbili, waongezewe muda mna mambo mengi sana mheshimiwa humu. Sisi tuna wizara zetu tunakwenda nazo mna mambo humu lakini siyasemi. Lakini natoa ruhusa muangalie ukurasa wa 45 na 46 muyaseme nyinyi, mimi sisemi kwa sababu yananigusa katika wizara, lakini haya wanayoyatoa yako kweli na haya tunataka vipi yaondoke. Lengo la serikali kukusanya mapato na matumizi yanayotumiwa yatumiwe kihalali kwa wananchi wetu.(Makofi).

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi niseme tu mheshimiwa naiunga mkono ripoti hii ya Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wake kwa asilimia mia moja na nawaomba wajumbe wenzangu wote waipitie ripoti hii waiangalie panapo mapungufu kwenye wizara ambazo zinazotuhusu tukafanye kazi zetu tuwasaidie na mapato yapatikane ili kuendesha nchi yetu.

Nashukuru mheshimiwa ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali na ahsante pia kwa kujali muda. Sasa namwita Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa nimesema na Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ya *PAC.*

Mhe. Spika, mimi katika mchango wangu nitaanza ukurasa wa 6 hadi wa 9 nitakaa sana hapo, na sababu ya kunifanya nikae hapo ni jinsi nilivyopata shaka kama walivyoendelea kutangulia kusema wenzangu juu ya matumizi ya fedha za serikali.

Mhe. Spika, hoja ya 28.10 ya kukosekana ripoti ya matumizi halisi ya shilingi Bilioni 4,948,358,000. Mhe. Spika, jambo hili nilishawahi kulizungumza na nikaambiwa tuisubiri wakati itakapokuja hii ripoti. Kifungu hicho kinaonesha jinsi ya malipo ya kampuni ya *MECCO* inaanzia hapo kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Amani/Dunga, Mfenesini/Bumbwini na Madaraja mawili. Kazi hiyo ilifanyika mwaka 2015 lakini katika ripoti haikuoneshwa kwamba huu mradi wa ujenzi wa hizo barabara gharama yake halisi ilikuwa ni kiasi gani. Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haikuonesha kwamba ujenzi huu gharama yake halisi ni kiasi fulani mpaka ikabidi kasoro hizi za shilingi bilioni 4,948.

Mhe. Spika, mimi jambo hili kama walivyotangulia kusema wenzangu nakubaliana nao kwamba ni jambo la kusikitisha juu ya upotevu wa fedha za serikali. Sisi ni kilio chetu. Mimi naamini Rais wetu mpenzi Dkt. Ali Mohammed Shein na wasaidizi wake tunawaona kila wakati wanapokwenda mbio kutafuta misaada kila upande kwa ajili ya kuikomboa nchi hii, kutaka nchi yetu iende mbele kwa ajili ya maslahi ya watu wetu. Sasa inapotokea miongoni mwa watu ambao si waaminifu wakaaza kufanya mambo ya ajabu kama hivi. Mheshimiwa ni jambo la kusitikisha sana, mimi nilikuwa nauliza huu ujenzi gharama yake halisi ilikuwa ni kiasi gani kwanza. Na kwa nini ikatokea mpaka kukosekana kwa risiti kumbukumbu za malipo ambapo tumeelezwa kwamba baadhi ya kumbukumbu zimefutwa kwa wino kwa kutumia *correction fluid*. Hivi kweli jamani mpaka inafika hali stabadhi ya malipo ya shilingi Bilioni 1.6 watu wanaweza kuifuta kwa *correction fluid*. Hata kama hakuna ubadhirifu binadamu wa kawaida utaamini vipi wewe kama hapa mimi sikufanyiwa ubadhirifu.(Makofi).

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha mimi nampongeza sana *CAG* kwa kuliona hili na kulieleza wazi, sisi tunataka watendaji wa serikali wawe wawazi kama hivi kwa ajili maslahi ya serikali hii, sote sisi tunaitumikia serikali hii na hakuna ambaye kwamba anakataa kwamba hapati maslahi kwenye utumishi wake. Sasa leo inakuwaje mtu inafika hadi kwamba unafuta vocha ya shilingi Bilioni 1,600,000,000 kwa kutumia *correction fluid*, au hakuna kumbukumbu mpaka unakuja kuhojiwa ndio unatafuta kumbukumbu unakwenda ku-*attach* pale kumbukumbu mpya, wewe umefanya kazi mwaka 2013 kumbukumbu inakuja watu kukukagua wanaiona leo mpya. Tutakuamini vipi kama wewe ni mkweli ndio miongoni mwa hati zenye shaka ambazo *CAG* amezieleza. Wito wangu mimi kwa watu wenye dhamana hasa wajenzi kwa sababu fedha ya serikali nyingi inapotea hapa kwenye ujenzi wa barabara, madaraja na mambo mengine.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy yeye kazungumzia kuhusu *consultant* kamzungumza vizuri hapa, kamzungumza kwamba kalipwa pesa lakini pia cha kushangaza kwamba hata lugha iliyotumika kwenye mkataba wa kazi aliyopewa umetumika kwa lugha ya Kifaransa sio Kiswahili wala Kiingereza. Hao watu wa hiyo wizara inayohusika tuwaulize wao wakijua hicho Kifaransa, sisi hatukijui hatuwezi kukichangia kwa sababu hatukijui. Lakini wao wanakijua? Kama wanakijua basi wangeleta wakakitafsiri kwa lugha ya Kiingereza au kwa Kiswahili lugha ambayo ni *common language* tunaitumia sote hapa, au ndio hilo walilosema wenzetu tupigwe changa la macho. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha na naomba mimi kwa wizara zinazohusika mambo kama hayo isiwe vizuri kwamba kila wakati lijirejee watu wazima hawasemani kila wakati, mtu anaambiwa jambo mara moja tu kwamba hili ulilolifanya silo na mara ya pili mtu anajitathmini mwenyewe kama kweli mimi nimesemwa kwa hiyo hili halirejei tena. Ni matumaini yangu kwamba ripoti inayokuja itakuja haitokuja na mambo na kasoro kama hizi zilizoelezwa hapa za kukosekana kwa stakabadhi, kwa kukosekana kwa kuwekwa risiti mpya na mambo mengine ambayo hayapendezi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi pia nilikuwa nataka kuzungumzia habari ya huyu Mkandarasi kwenye *page* ya 7, Chapria. Chapria alipewa malipo ya shilingi 105,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Jendele/Cheju/Kaibona/Koani/Jumbi. Sisi kama tunavyojua serikali ilimsimamisha yule kwa kutoweza kukidhi viwango na kuweza kutekeleza ule mradi wa ujenzi wa ile barabara. Sasa malipo yake tumeyaona hapa, lakini jee wakati alipokuwa analipwa hizi fedha alizokuwa amelipwa zilikuwa zinaendana uhalisia na kazi aliyokuwa anaifanya? Mimi naomba kidogo ufafanuzi wa suala hili jee wakati alipokuwa kalipwa huyu hizi fedha alizolipwa zilikuwa zinaendana na ile kazi ambayo alishaifanya pamoja na kuwa sisi tulikuwa na shaka, kwa sababu huyu alikuwa ameshatiliwa shaka toka mwanzo juu ya utendaji wake wa kazi kwamba ni wa kusuasua, vipi waliweza kumlipa fedha kiasi hiki.

Mhe. Spika, la mwisho ni kuhusu suala la ununuzi wa gari hilo lilozungumzwa. Mheshimiwa mimi nilikuwa sitaki nilirejee kwa sababu wenzangu wameshalizungumza kanifilisi hili, lakini si kwa ajili ya hiyo taasisi tu ambayo imeinunua gari hilo la thamani kubwa baadae wakajiuzia. Ni juzi tumepitisha hii sheria ya ununuzi wa mali za umma, lakini mimi naomba kwamba hatua kali zichukuliwe zaidi kwa watu wanaonekana wanafanya ujanja wa namna hii. Huu ni ujanja haiwezekani kwamba kitu cha bei kubwa milioni zote hizo za

pesa, uje uichukue gari hiyo mali ya serikali muuziane kwa shilingi milioni 10, 15 haiwezekani.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi najua wachangiaji watakuwa wengi na kwa ajili ya muda na kwa kutoa nafasi kwa wenzangu natamka kwamba naiunga mkono ripoti hii ya kamati, na ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako na namwita sasa Mhe. Zulfa Mmaka Omar atafuatiwa na Rashid Makame Shamsi na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf ajiandae.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Kamati hii ya *PAC.*

Mhe. Spika, mimi nianze katika Mfuko wa Jimbo. Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili ni wasimamizi katika mfuko huu wa jimbo. Lakini katika mfuko huu wa jimbo Mhe. Spika, kumejitokeza matatizo mengi sana ambayo yanafanywa na Wajumbe wa Mfuko huu bila ya kujijua.

Mhe. Spika, tunaomba katika mfuko huu la kwanza serikali itoe pesa hizi katika muda ambao unastahiki uliopangwa ili watu hawa waweze kuzifanya kazi zao za jimbo na waweze kurikodi kazi zao ambazo wanazifanya waondokane na matatizo ambayo yametukumba katika ukaguzi wetu. Pia Ofisi ya Makamu wa Pili tunawaomba watoe mafunzo zaidi juu ya Wajumbe hawa kuhusiana na matumizi ya pesa hizi, pia tuwaombe Waheshimiwa Wawakilishi pesa hizi wanapozipata wajue kwamba ni kwa ajili ya jimbo, si kwa ajili ya mtu binafsi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, katika mfuko huu tumekuta kwamba kuna baadhi ya Wawakilishi pesa hizi wanazitumia kwa mambo yao binafsi. Mheshimiwa ile haileti sura nzuri, hii pesa ni ya wananchi na ni ya jimbo wakifanya vile kuzitumia kwa maslahi yao binafsi, basi mwisho wa siku tunapata malalamiko serikalini kwamba jimbo halifanyi kitu, kumbe ni Mwakilishi hafanyi yale ambayo amepangiwa kuyafanya. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nikitoka hapo mimi nataka niende katika Chuo cha *SUZA*. Mheshimiwa watu wengi wamezungumzia juu ya chuo hiki. Kamati imebaini ukiukwaji wa matumizi ya fedha za umma na taratibu za manunuzi katika chuo hiki. Mfano, wenzangu wameutoa hapa Mhe. Spika katika Chuo kile tumekwenda tunakuta risiti viongozi wa Chuo wametumia matumizi yao ya kuleta wageni wao kutoka nje, badala ya wageni wale kuwahudumia kwa pesa

zao za mifukoni, tunaona kwamba wakubwa wale wanatumia pesa za Serikali kuwalisha, kuwaweka bila ya taratibu zozote zinazokubalika. (*Makofi*).

Mhe. Spika, pia wakati tumekwenda na Kamati katika Chuo kile tulikitaka Chuo hicho watuletee majibu yanayotosheleza juu ya ununuzi wa gari ya *Jeep*, utumiaji wake na kila kitu kinachohusika pale na gari ile. Kwa sababu gari ile ilitutia mashaka sana lakini lakusikitisha toka tufanye ukaguzi ule hadi leo hapa, majibu juu ya gari ile hatujayapata na bado Kamati inaendelea kusema kwamba ina mashaka makubwa sana juu ya ununuzi wa gari ile pamoja na uuzaji wa gari ile. Kwa hiyo, Kamati inaitaka uongozi wa Chuo cha *SUZA* kubadilika na kufuata Sheria za Matumizi ya Fedha za Umma ipasavyo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Mfuko wa Barabara. Mhe. Spika, hapo mimi nataka nizungumzie barabara za Kikwajuni/*Wireless*, Chukwani/Buyu na Fuoni Kibondeni. Mhe. Spika, barabara hizi tulienda kuzikagua kwa kina tulichukua siku tatu kuzikagua, lakini niseme kwamba kuna masikitiko makubwa kwamba barabara zile zimetumia pesa nyingi lakini ubora wake ni hafifu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo tunaona kwamba msimamizi wa ujenzi ule alikuwa ni *UUB*, mkandarasi wa ujenzi ule ilikuwa ni *Abdalla Contractor Company Ltd*. Thamani iliyotumika pale ni kubwa, urefu wa barabara ni *3.2 kilometer*, lakini Mhe. Spika tulipokwenda kwa ajili ya kumkagua Mkandarasi huyu hatukupata matokeo yoyote, hatuona ofisi yake, hatukuona kasajiliwa vipi, hatukujua anafanya kazi zake zipi. Kwa kweli sisi kama Kamati huyu *contractor* tuna mashaka naye makubwa sana juu ya kusajiliwa kwake. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara husika itutoe katika mashaka juu ya mkandarasi huyu kwa sababu hatujaridhika na utendaji wake wa kazi, tunaomba ishirikiane na sisi kutupa majibu sahihi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika Ofisi ya *CAG*. Mhe. Spika, tumekuta malalamiko mengi sana tukitembea katika ukaguzi wetu kwamba Ofisi ya *CAG* inapeleka watu ambao hawana ujuzi juu ya kukagua maeneo baadhi ya maeneo ambayo wanapelekwa. Kwa mfano, tumekwenda *PBZ*, karatasi ambazo zimeletwa na mkaguzi kwamba ukaguzi ule ulikuwa haufai au hauko sawa, lakini tulipokwenda sisi Kamati ya *PAC* kukagua pale, tulikuta kwamba majibu yake tuliyopewa na *CAG* na majibu ambayo tumepewa kule yako tofauti. Katika uchunguzi wetu tumebaini kwamba majibu yale ambayo tumeyakuta sisi yako sawa.

Suala hilo hilo tunakumba nalo katika ofisi mbali mbali, unakuta kwamba Mkaguzi anakwenda kufanya ukaguzi wake sijui kwamba hapati mashirikiano ama sijui kwamba akienda pale anakuwa hana elimu ya kutosha juu ya lile ambalo analolifanya. Kwa hivyo, tunamuomba *CAG* atumie watu ambao wanaweza kumsaidia katika kufanya chunguzi hizi kama za mahesabu ambazo yeye hana utaalamu nazo kama tulivyotumia sisi katika kuchunguza barabara. Mhe. Spika, sisi hatujui barabara inatengenezwa vipi, lakini Baraza limeamua kutafuta mtu kwa ajili ya kutusaidia kazi ile na naamini kazi ile tuliifanya vizuri na matokeo yake umeyaona. Kwa hivyo, nimshauri *CAG* katika maeneo ambayo anahisi hayafahamu, si vibaya kupata msaidizi ili na sisi tuweze kufanya kazi zetu bila ya lawama ambazo tunaambatana nazo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende katika madeni. Mhe. Spika, tunakuta kuna baadhi ya madeni ambayo yanazifanya baadhi ya wizara kushindwa kufanya kazi zake. Kuna madeni mengi ambayo yamebebwa na Wizara ya Fedha na Mipango lakini madeni yale hayalipwi kwa wakati, kutokulipwa madeni yale kwa wakati, kunasababisha kwamba serikali kutokufanya kazi zake au wizara ambavyo imejipangia. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha aliangalie sana suala hili la madeni na awafikishie watu wale pesa zile za madeni kwa wakati wao waliopangiwa ili nazo wizara zile ziweze kujiendesha katika kazi zake.

Mhe. Spika, nakuhisi kama unataka kunambia kuwa muda wangu umekwisha. Mheshimiwa nikitoka hapo niende katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Spika, niipongeze Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa ukusanyaji bora wa fedha ambazo zinapatia pato letu la nchi na kuweza kujikwamua kimaisha. Lakini katika Mamlaka hii kuna malalamiko ambayo tumeyapata.

Mhe. Spika, pesa hizo wanazozikusanya inaonekana kwamba asilimia 80 haiendi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, asilimia 80 hii huchukuliwa serikalini kupitia *ZRB*. Mhe. Spika, kuchukuliwa kwa asilimia hii 80 inaifanya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kutokufanya mambo yake kama inavyotakiwa. Mamlaka kuna baadhi ya ndege zinakuja pale, kwa hivyo wakati wa kuja ndege zile ni lazima wawatengee sehemu ya ofisi na sehemu ile pesa ambazo zinatumika kutengeneza ni pesa hii ambayo wao wanaikusanya. Lakini pesa ile wanakuta kwamba wanaikusanya lakini hawaitumii wao na baadae inakwenda katika Mfuko huu wa Serikali kupitia *ZRB*. Kwa hivyo, wanaiomba serikali pesa zile warejeshewe wao ili waweze kufanya maendeleo katika viwanja vile vya ndege ili maendeleo yaonekane kutokana na wanachokikusanya.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja na zaidi na nawaomba Wajumbe waiunge mkono ili tuweze kufanya kazi vizuri ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar, ahsante kwa mchango wako ulikuwa mzuri. Sasa namwita Mhe. Rashid Makame Shamsi atafutiwa na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na Mhe. Ali Salum Haji ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Spika, ahsane sana na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuweka mwega katika ripoti hii ya Kamati yangu ya *PAC* kwenye mustakabali mzima wa maendeleo ya taifa hili.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kuweza kuipongeza Kamati kwa utendaji wake lakini vile vile nichukue fursa hii kuweza kuwapongeza watendaji wote wa wizara, mashirika, taasisi za umma na Kamati za Majimbo kwa mashirikiano makubwa na mazuri ambayo wameipatia Kamati. Nashukuru sana kwamba watendaji wengi walitupa mashirikiano niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi kwanza nikazie katika suala zima la taratibu za ununuzi. Mheshimiwa mengi yameelezwa na Kamati imeeleza, lakini sio vibaya kuweza kuweka mkazo zaidi katika suala zima la taratibu za unuuzi ambazo ni sehemu ambayo wakati mwengine inachangia mianya hii ya mapato ya serikali kuweza kuvuja. Mhe. Spika, katika matembezi yetu tumeweza kugundua kwamba masuala ya Bodi za Zabuni, kuna haja kubwa sana ya wizara inayohusika, Wizara ya Fedha kuweza kutoa taaluma juu ya masuala ya Bodi za Zabuni. Kwanza kuna kasoro ya hata uteuzi wa wajumbe, nina imani kwamba kutokana na sheria mpya ambayo tumeipitisha hivi karibuni ya ununuzi, basi nina imani kwamba elimu ikitolewa itasaidia sana kwanza uteuzi ambao unaendana na taratibu za kisheria. *(Makofi).*

Mhe. Spika, unaweza ukakuta kwamba Mjumbe ameingia katika Bodi ya Zabuni lakini kumbe kwa taratibu hawezi au hahusiki kuingia katika bodi hiyo. Lakini vile vile nikija katika Bodi ya Zabuni wakati mwingi baadhi ya taasisi tunakuta kwamba zinahodhiwa maamuzi yake na baadhi ya viongozi katika baadhi ya taasisi. Kwa hivyo, kiongozi wa taasisi anakuwa yuko juu kuliko Bodi ya Ununuzi, kwa tafsiri hiyo ununuzi unaweza ukafanyika bila ya kufuata taratibu na hii ni hatari kubwa kwa taifa letu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, suala zima la kuwashirikisha wataalamu katika Bodi ya Zabuni, nina imani kwamba Bodi ya Zabuni ina nafasi ya kuweza kumualika mtaalamu

pale wanapopitisha baadhi ya zabuni ambazo bodi inahisi hazina utaalamu nazo. Kwa kweli tumeona baadhi ya matatizo kwa sababu vinanunuliwa vifaa au vyombo kutokana na maamuzi ya Wajumbe wa Bodi ambao wengi wao wanakuwa hawana utaalamu. Kwa tafsiri hiyo utakuta kwamba kitu au bidhaa inayonunuliwa inakuwa haiendani na vigezo ambavyo pengine vilikuwa vinastahiki. Kwa mfano, nikija upande wa barabara. Mpaka hivi sasa serikali yetu haina *specification* au kiwango hasa cha barabara ambazo tunazitaka. Kwa hivyo, wakati umefika sasa serikali kwa kushirikiana na wizara ianayohusika kuweza kuwa na vigezo vya barabara gani tunazitaka tuweze kujengewa, ili hata wakandarasi wanapokuja kutoka nje maana yake sisi wenyewe tuna vigezo. Hivi sasa tunatumia vigezo vya Tanzania Bara, mimi nafikiri bado hatuko sahihi. Kwa sababu mazingira ya ardhi yanatofautiana, unapojenga barabara tuseme ya Mahonda na barabara ya Makunduchi ni vitu viwli tofauti vigezo vyake vinatofautiana.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa nije kwenye suala la bajeti. Tumeona kwamba changamoto nyingi ambazo zimejionesha kwa wenzetu ni kwamba miradi mingi ya maendeleo haikutekelezeka vizuri, fedha nyingi zilitumika zaidi katika matumizi ya kawaida yanayogusa mishahara na maposho mengine. Niiombe sana serikali katika bajeti hii kuweza kufikiria kuongeza bajeti kwa wizara hizi kadri hali ya fedha inavyoruhusu ili kuona kwamba miradi ya maendeleo nayo inapata fedha zinazokidhi haja, ili kuona kwamba zile changamoto za wananchi zilizoko vijijini zinatekelezwa ili wananchi nao wawe na imani juu ya serikali yao kuhusiana na maendeleo yao.

Mhe. Spika, nije sasa katika masuala ya mali za seriali. Ni ukweli usiopingika kwamba umefika wakati hivi sasa kuwa na daftari la kumbukumbu za mali zake, *asset register* ya serikali. Lakini changamoto iliopo ni kwamba hata ukienda katika hizo baadhi za taasisi za serikali, basi utazikuta nyengine hazina kumbukumbu za mali zake. Nyengine utakuta kwamba uwekaji wa taarifa haukukamilika lakini kubwa zaidi vifaa vingi katika baadhi ya taasisi unavikuta havina *code number.* Hii ni hatari kwa sababu ina maana vifaa vile au vitu vile ina maana havifahamiki, kwa hivyo hata mtu aikiiba maana yake hajulikani au hakijulikani.

Kwa hiyo, suala hili ningeomba sana Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma kuweza kulikazia sana suala la kuwa na kumbukumbu ya mali zake, lakini vile vile vifaa vyote vinavyohusika na taasisi ile kuwa vina *code number*. Lakini hata wakati mwengine tunakuta kwamba hakuna hati miliki za maeneo au vyombo ambavyo vimo katika taasisi, tumetembelea kwa mfano Pemba unakuta gari zinatumika katika wizara Pemba lakini utaambiwa kumbukumbu

zake au hati zake ziko Makao Makuu Zanzibar. Hii ni hatari, tunapendekeza sana taasisi hizi ambazo zinakabidhiwa vifaa au mali basi na hati zake ziwepo pale pale, ili wakaguzi wanapopita basi waone kwamba hati zile zipo zinasomeka vizuri.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa nije katika suala zima la Mfuko wa Maendeleo. Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo una changamoto mbali mbali tumeziona. Lakini nichukue fursa hii kuwapongea Wawakilishi wote ambao tumewatembelea katika majimbo tisa. Ni ukweli usipingika kwamba Wawakilishi wanatumia pesa nyingi zaidi kuliko zile wanazotiliwa katika Mfuko wa Majimbo. Hilo tunawapongeza miradi mingi waliyoifanya ina thamani kubwa kuliko pesa walizotiliwa. Changamoto iliyopo ni utunzaji mzuri wa kumbukumbu na hili nichukue fursa hii nimuombe sana Waziri katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais muda huu ni muafaka tukisubiri kuingiziwa pesa hizo kuweza kuwafanyia semina Wawakilishi wote juu ya taratibu za kuendesha Mfuko wa Jimbo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukweli usiopingika kwamba kazi za miradi zinakwenda pamoja na kasoro mbali mbali na hususan tukiangalia pale mwaka 2011/2012 Mfuko bado ulikuwa hauna taratibu, kwa hiyo pale matumizi yake yalikwenda varange varange. Lakini nafikiri hivi sasa Kanuni na Sheria zipo, ni vyema sasa tuweze kupata semina ili kuweza kuondosha kasoro Wawakilishi wapya walioingia, na nina imani kwamba tukipatiwa semina basi kasoro hizi zitapungua kwa kiasi kikubwa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa nije katika suala zima la sheria mpya ya ununuzi, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha kuweza kuwapa mafunzo watendaji wote wanaohusika na masuala ya usimamizi wa fedha ili kuona kwamba sheria hii inafanya kazi vizuri na kuweza kupunguza zile kasoro mbali mbali ambazo tumezibaini katika ziara zetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na machache hayo ya kuweza kuelezea nishukuru sana kwa kunipa nafasi hii na niwaombe pamoja na muda mchache, kwanza niombe radhi sana kwa Kamati kwamba kwa kweli muda ambao tumeupata ulikuwa ni mdogo, leo ilikuwa ni siku ya kuwasilisha Sekta ya Mawasiliano.

Kwa hivyo, najua muda wenu ulikuwa ni mdogo wa kuweza kupitia hata hivyo niwaombe wajumbe kwa muda huo huo mfupi kuweza kupitia na kuichangia ripoti hii na kuweza kuipitisha na mimi ninaipitisha kwa asilimia moja ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa namwita Mhe. Mtumwa Peya Yussuf atafuatiwa na Mhe. Ali Salum Haji na Mhe. Asha Abdalla Mussa ajiandae.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati hii ya *PAC.*

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na wenzangu lakini na mimi nitagusia baadhi ya mambo. Kwanza niwashukuru sana mawizara, mashirika na taasisi za serikali kwa kutupa mashirikiano katika kufanya kazi hii kwenye Kamati ya *PAC.* Pia nipongeze kwa dhati kabisa Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa kazi ngumu ambayo tumeifanya, lakini kuhakikisha mawizara, mashirika na taasisi za serikali pale tunapoingia kwenda kufanya kazi hii ya ukaguzi wasione kwamba labda tunakwenda kuwashtaki au kuwachunguza kiasi gani. Ni wajiu wetu kwa sababu sote tunajenga nyumba moja, kwa hivyo lazima tukusoane, tuambizane na tuweze kuyafanyia kazi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi naanza na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Katika ukaguzi wetu tulifika kwenye Kikosi cha Valantia. Kikosi hiki kwa kweli kinafanya kazi kubwa na ngumu, lakini mbali ya kazi zake zinazofanya za ulinzi, Kikosi hiki kinafanya kazi ya kutoa huduma kwenye taasisi za serikali pia taasisi za watu binafsi kwa makubaliano na mikataba maalum ya utendaji kazi huo.

Mheshimiwa cha kushangaza na kustaajabisha kuna madeni makubwa ambayo wanadai kwenye taasisi za serikali na taasisis za watu binafsi. Mhe. Spika, niombe sana wale wote ambao wanajua wanadaiwa na kikosi hiki, basi wafanye haraka warejeshe hizi fedha ili waweze kuendeleza huduma zao kwa ukamilifu.(*Makofi*).

Suala jengine kuna huu utaratibu wa *tender.* Kwa kweli utaratibu huu baadhi ya maeneo mengi utaratibu huu haufuatwi utakuta ni mtu mmoja au wawili wanatoa maamuzi kupitisha kitu chochote bila ya kupitisha kwenye *tender.* Niwashauri tu, mashirika na mawizara hii *tender* ifuatwe kama taratibu zilivyopangwa kama sheria inavyoruhusu.

Halafu jengine kila taasisi inatakiwa iwe na *store ledger,* lakini kwa bahati nzuri au mbaya sehemu nyingi tulizopita hakuna *store ledger* wala hiyo *store* yenyewe hakuna. Nawaomba wote wnaohusika wahakikishe kwamba *store* zinakuwepo na hii *store ledger* pia inapatikana. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Spik, nije kwenye suala jengine la *assets register*. Maeneo mengi tuliyopita hakuna daftali hili la kuwekea kumbukumbu na tunaambiwa siku zote, "mali bila daftari hughibu bila ya habari". Kwa hivyo, mali nyingi za taasisi zinapotea kwa sababu hakuna kumbukumbu yoyote ambayo imewekwa. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kulikuwa na gari ambapo Kamati ya *PAC* iliopita gari hii ilisema irudishwe, lakini bahati nzuri Kamati ya *PAC* hii tumekwenda gari hili halipo na tuliambiwa gari hili lilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Tumelifuatilia gari hili hatukulijua wapi lipo. Naiomba serikali gari hili lijulikane wapi lipo na baadae tuje tupewa taarifa gari hili liko wapi na lirejeshwe wizara husika.(*Makofi*)

Mhe. Spika, halafu kuna jambo jengine hili Mkoa wa Kusini. Ndani ya Mkoa wa Kusini kuna magofu ambayo yametakiwa yarejeshwe serikalini lakini magofu haya ndio kama tunavyosema wameambiwa kwa mdomo hakuna maandishi yoyote ambayo yameandikwa pale, ndio pale ninaposema kwamba kila mali basi inatakiwa iandikwe na inapohamishwa pia kuwe na maelezo ya maandishi.

Mhe. Spika, jengine nakuja tena kama wenzangu walivyogusia Ofisi ya *CAG*. Kwa kweli ofisi hii kwanza tumefanya kazi nayo vizuri, wametupa mashirikiano makubwa, lakini baadhi ya maeneo kama walivyoeleza wenzangu, tuliokuwa maofisa tunakwenda nao walikuwa hawana utaalamu wa kutosha kuweza kujua yale matatizo ambayo yako pale. Kwa hivyo, namuomba *CAG* yule ambaye anampeleka kwa mara ya kwanza kufanya ukaguzi ikiwa ni mtaalamu na hii Kamati ya *PAC* inapokwenda, basi ni vizuri kwenda naye yule anaweza akatupa tukapata uhakika wa lile eneo na ile kazi ambayo tumekwenda kuifanya.

Mhe. Spika, chengine cha kusikitisha hii Wizara ya Ujenzi, kuna vocha ya malipo ambayo huyu aliyelipwa *donors assistance project* kwa kweli imesikitisha, hii vocha imefutwa kwa wino mweupe na tumeiona kwamba imefutwa, ina maanisha dhahiri kwamba hili hata kama hukuiba lakini inaonesha kwamba hili suala moja kwa moja sio sahihi, hata kama kuna makosa umefuta kwa wino angalau basi uweke *sign* ya kuonesha kwamba hapa mimi ndiye niliyerekebisha hili, lakini wewe unafuta kwa wino hakuna maelezo yoyote pale mbele ambayo yanajionesha. Kwa kweli hilo ni tatizo naomba tujirekebishe tubadilike tusifanye kazi kwa mazowea.(*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine la mwisho nalizungumzia suala la mitaro. Tulipokwenad kwenye ziara zetu tulikwenda Bububu Kijichi kwenye mtaro ule kuna bomba ya maji safi na bomba hiyo ina kiungo na kiungo chake kinapitisha maji,

inaponyesha mvua mtaro ule unajaa maji na bomba lile wananchi wengi wanatumia. Kwa hivyo, pale ni hatari kwa wananchi wetu wa eneo lile. Niombe tu Mamlaka ya Maji ishughulikie suala hile ndani ya mitaro na kuona kwamba yale mabomba ya maji safi basi yanakuwa katika ya hali ya salama ili wananchi wetu kuepuka kupata matatizo ya kiafya.

Kwa hayo, machache Mhe. Spika, mengi yameshazungumzwa na mimi niliona nigusie hayo, lakini pia niwaombe Wajumbe wezangu kuiunga mkono taarifa ya Kamati hii ya *PAC* na mimi naiunga mkono asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, sasa ninakwita Mhe. Ali Salum Haji atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ajiandae.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia ripoti hii ya kamati ya *PAC*.

Mhe. Spika, kabla sijachangia chochote nianze kwa kushukuru sana Wajumbe wa Kamati ya *PAC* na sababu ya kuwashukuru kwa namna walivyotumia ujasiri wao katika utendani wa kazi, kwa sababu serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inahimiza Utawala Bora wa haki na wa kisheria. Kikawaida sio sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hata wananchi kwa jumla wasingetarajia kwamba Kamati hii inaweza kuwapitia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wenzao wa karibu sana, wakaweza kuwatia *quiry* katika matumizi bora ya fedha za serikali. (*Makofi*).

Sasa ndio maana nawapongeza kwa dhati kwa namna walifanya ujasiri wao katika kutekeleza wajibu wao kikazi katika taratibu za kisheria. Nawaomba wasichoke na yale Majimbo ambayo yaliyobakia hayajakaguliwa basi tukimaliza kikao vikao hivi wamalizie ili tupate taswira iliyokuwa nzuri katika utendaji bora.(*Makofi*).

Mhe. Spika, tunapokaa hapa tukapiga kelele namna ya matumizi bora ya serikali katika kusimamia pesa hizi za wavuja jasho. Sasa tujijue kwamba watu wanasema msumeno huu una pande mbili, unakwenda na kurudi kwamba na sisi kwamba na sisi tutapokuwa hatuafati utaratibu basi tuwe tuna haki ya kufuatiliwa taratibu zote zinazostahiki.

Lakini katika hili Mhe. Spika, nataka nije nimuombe Mhe. Mwanasheria hili litakuwa lake yeye, kwa sababu unajua tunajenga utaratibu wa kisheria katika

kufanya kazi zetu za Baraza hili katika kusimamia hali nzima ya mapato. Hebu atusaidie taratibu za kisheria zikoje kwa sababu kuna kipindi Baraza lililopita tulihoji sana hapa kwamba *CAG* anakagua Taasisi za Serikali, lakini yeye anakaguliwa na nani, kwa sababu hofu yangu Kamati ya *PAC* sina mashaka na Wajumbe Mhe. Spika, lakini hofu yangu utaratibu wa kisheria itakapofikia wakati kwa sababu Mjumbe huyu ni mpya Jimbo alilokwenda kulikagua safari hii lilikuwa la Mhe. Machano Othman, lakini awamu inayokuja litakuwa lake yeye, utakapofikia wakati Jimbo la Mwenyekiti wa *PAC* linataka kukaguliwa na Wajumbe ni watu wake ambao wako chini yake. Hivi taratibu za kisheria zinatupelekaje kuja kulikagua Jimbo la Mwenyekiti wa *PAC* kisheria ili nayo serikali kwa jumla iridhike katika namna bora ya ukaguzi wa jimbo hili.(*Makofi*).

Mhe. Spika, leo tuna Mhe, Miraji Khamis Mussa tunajua ni muadilifu, mtenda haki na ndio maana katumia busara hizo. Lakini siku nyengine anaweza kuja mtu kwa sababu Kamati hizi zinaongozwa na wapinzani kiutaratibu wa kisheria, tunapokuwa tumo ndani ya Baraza ambalo lina wapinzani ndani Mwenyekiti wa *PAC* anakuwa ni Mwenyekiti wa *opposition*. Leo kwa bahati tuko asilimia 99 ni wana CCM, wana CCM wote wanakuwa wako safi hata kama Mwenyekiti wa *PAC* hajakaguliwa hakuna tatizo.

Lakini itakapokuja kutokezea pahala mpinzani na kwa sababu tuna historia mbaya Mhe. Spika, katika kutumia pesa za Mfuko wa Jimbo kwa wapinzani, kwa sababu miongoni mwa watu ambao waliofanya vibaya na hawakuwatendea haki wananchi wa jimbo hili, basi ilikuwa ni Jimbo la Mji Mkongwe. Jimbo la Mji Mkongwe aliyekuwa Mwakilishi pale katika vipindi vyote hakwenda kuchukua pesa zile kuwapelekea wananchi. Sasa inakuwa ndio tatizo na ndio maana nikasema tutafute namna bora katika kuziangalia pesa hizi za maendeleo ya Mfuko wa Jimbo katika majimbo yote kwa taratibu na sheria.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba niendelee kidogo tu kwa sababu leo Kamati ya *PAC* imekuja na *design* iliyokuwa ni nzuri sana, kwa sababu wao ndio waliotuletea hoja kutaka Wajumbe tuichangie, lakini hoja zote wamebeba wenyewe wameanza kuchangia wenyewe kuanzia mwanzo mpaka sasa hivi. Sasa kwetu sisi tutapitia pitia tu yale ambayo wametuachilia machache sana kuweza kuboresha mle ambamo wametuachia.(*Makofi*).

Mhe. Spika, tunakazia tu kwa sababu mimi nitazangumzia lile suala la gari ile la Wizara ya Kilimo ambalo mtendaji pale kama alivyozungumzwa kwenye ripoti alikuwa ni Mkurugenzi akapata uteuzi akenda Afisi ya Makamu wa

Kwanza ya Rais katika nafasi ya Naibu Katibu, akahama na gari lake lakini nayo serikali hii anayomalizia ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ameteuliwa tena kuwa Naibu Katibu Mkuu Kilimo. Lakini cha kushangaza alipokwenda kwa Makamu wa Kwanza kenda na gari, lakini aliporudi Kilimo kule ambako gari kalichukua hakurudi nalo.(*Makofi*).

Sasa sababu za msingi ninazozitaka kuzungumza hapa kwamba hizi mali za serikali zinakuwa na utaaratibu wake na zinakuwa katika maandiko. Leo mali ina maandiko kwenye Wizara ya Kilimo, mali hiyo hiyo leo sasa hivi imetoka imeenda kwa Makamu wa Kwanza wa Rais ambapo hiyo wizara yenyewe haipo. Sasa tuna hofu kwamba gari hii inaweza ikajakufikia ikaja ikauzwa wao wenyewe watu wa Kilimo hawafahamu na pasipofuatwa utaratibu uliokuwa mzuri Mhe. Spika. Sasa na mimi niombe tu kwamba tunapoamua kufanya masuala ya kisheria basi taratibu za kisheria ziwe zinafuatwa ili tuone kwamba mali za serikali Mhe. Spika, zinakwenda katika utaratibu uliokuwa mzuri.

Mhe. Spika, maeneo mengine ambayo nataka kuyazungumzia katika ukurasa wa 24 Mkoa wa Kaskazini kuna jambo ambalo limeelezewa katika mantiki nzima ya wenzetu wale walioamua kukodi gari kitaratibu na kisheria na walifunga mkataba katika gari lile la kupeleka wafanyakazi. Lakini kinachoonekana baada ya mkataba ule kumalizika Afisi ile ya Mkoa wa Kaskazini iliendelea kutumia gari ile pasipo na mkataba na lilendelea kufanya malipo bila ya taratibu za kisheria zinazofuatwa.

Mhe. Spika, hili nilikuwa naomba nilitolee indhari sana, katika maeneo mengi ya serikali kinachoonekana kwamba tunapoamua ama kukodisha majengo ama vyombo masuala ya mikataba maeneo mengi yanakuwa hayafati utaratibu. Nazungumza hivyo Mhe. Spika, kwa sababu ya ushahidi wa kutosha. Katika Kamati yangu ya Fedha tumegubikwa na tatizo la ufungaji wa mikataba katika suala zima la ukodishwaji wa maghala, na Kamati ilijaribu kuomba taarifa za ukodishwaji ule wa maghala. Taarifa zile Mhe. Spika, pamoja na kuja kwake lakini zinaonekana kwamba bado zimekumbwa na ukwakwasi wa hali ya juu katika kuonesha haki wapi imetendeka. Kuna waliomaliza mikataba maghala wanaendelea kuwa nayo, hakuna *review* watu wanaendelea kukaa na majengo, majengo yale yamekodishwa kwa kipindi kirefu kwa bei ya chini wengine waliokodishwa wamekodisha mara mbili, anayekodishwa anakodisha kwa mtu mwengine.

Sasa hili Mhe. Spika, nilikuwa nataka nitoe indhari tu kwa serikali katika masuala mazima ya kuangalia mikataba tunayofunga katika kusimamia mali za serikali. Na niombe Kamati ya *PAC* kabisa, najua utaratibu utakuja lakini nalo

hili wajaribu kuliangalia kulifuatilia, wafuatlie majengo ya serikali maghala ambayo yalikuwa yakitumika katika shughuli mbali mbali ambayo yako katika Wizara ya Biashara ambayo sasa hivi mikataba yake inaonekana imekuwa ina utata ndani yake.(*Makofi*).

Mhe. Spika, chengine ambacho nataka nikizungumzie wakati napitia taarifa ya Kamati ya *PAC* niliona jambo katika Wizara ya Afya na jambo ambalo nimeliona ni suala zima la kusafirisha wagonjwa wanaokwenda nje. Jambo hili ukisoma taarifa linaonekana kwamba kidogo lina mchanganyiko ndani yake katika kupata taarifa, kwa sababu ni jambo ambalo linagusa pande mbili, linagusa Wizara ya Afya lakini linagusa Wizara ya Fedha katika utoaji wa fedha. Sasa niombe basi kutafuta namna bora ya ushirikiano katika kuliweka sawa jambo hili. Hili jambo Mheshimiwa tulisipoliangalia kwa makini hili eneo linachukua pesa nyingi za walipa kodi na ndio maana wenzetu Tanzania Bara wameamua kutafuta namna bora ya kupunguza kuwapeleka wagonjwa nje ili wawatibu ndani ili kupunguza gharama. Sasa sisi hatujafikia katika uwezo huo wa kuwatibu wagonjwa wetu ndani ili kupunguza gharama tunaendelea na huu utaratibu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri akubali kwamba hapa pana mazonge ndani yake. Lazima akubali na mimi mara nyingi ninapozungumza Mhe. Spika, huwa napenda nitoe ushahidi sana tu kwamba kuwa watu wanafika pahala mtu anapewa *visa*, maana yake *visa* tayari ameshalipia afikia hatua wakati mwengine za kulipwa, lakini anakuja ku-*cancel* safari kati kati na wakati wengine wanakuwa wao wenyewe hawajui, kwa sababu Wizara ya Afya sio wao wanalipa. Sasa inakuwa ule ukweli wenyewe huupati, inawezekana mtu akapewa pesa za kwenda India akaamua kwenda Bara kwa sababu ya ile hali yake na kwa sababu hata hizo *return* zenyewe hazipatikani kwamba mtu huyu amekwenda kutibiwa India amerudi na tiketi ya kwendea na tiketi ya kurejea lakini pamoja na malipo ambayo yamefanyika kule.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nakushukuru nimemaliza na naomba nilinde muda wako Mhe. Spika. Lakini kulikuwa na kadhia ile gari ya *SUZA* watu wengi wameizungumza na hususan Wajumbe naomba tu bado tuendeleze katika kuitumikia serikali hii kwa kufuata maadili mema na kutumia pesa za serikali kwa vile ambavyo inastaki na kufuata taratibu zote za kisheria

Mhe. Spika, nashukuru. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Salum Haji. Sasa ninamwita Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajiandae.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili na mimi kuzungumza machache.

Mhe. Spika, mimi nitatumia nadhani dakika moja tu na kwa kuwa Wajumbe wengi ambao wamo kwenye Kamati hii wametutolea ufafanuzi wa kutosha na tumeweza kufahamu zaidi na kama walivyosema wenzangu kitabu hichi ni kikubwa, lakini tumepata muda mchache wa kupitia baadhi ya maeneo.(*Makofi*).

Mimi nilipopitia ukurasa wa 46 mpaka 48 kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Wanawake na Watoto nimeona hapa baada ya kuisoma nimebaini kwamba baadhi ya Taasisi nyingi za serikali ambazo zimo katika mahesabu yao tumeona kwamba udhibiti mkubwa wa kumbukumbu pamoja na risiti zile tumegundua kwamba haupo na hii kuna msemo kwamba unasemwa " Ukimuonea haya mke ndugu huzai naye".(*Makofi*).

Mhe. Spika, nimesema hivi kwa sababu Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mawaziri wake wanawajibisha watendaji wao ambao hawawezi kuwajibika vizuri katika kazi zao, na nimesema haya kwa uchungu, tunatizama kwamba sisi sote tunalilia mapato ya Zanzibar yapatikane ili kuendesha nchi yetu kwa vizuri.

Mhe. Spika, lakini na sisi tunaomba hapa Zanzibar tunaye Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali, hawa wahasibu pamoja na watendaji wanaofanya ubadhirifu huu basi na wao watumbuliwe majipu. Na tukifanya haya Mhe. Spika, basi tutaondosha muhali na tutaweza kufanya kazi zetu ipasavyo na ndio maana kama tusipofanya hivi kila siku au kila mwaka Kamati ya *PAC* itatuletea hapa changamoto ambazo wamekabiliano nazo lakini tutabakia vile vile.(*Makofi*)

Mhe. Spika, niseme nimalizie kwa kuwapongeza sana Kamati hii ya *PAC* na isivunjike moyo, lakini izidishe juhudi ya kufuatilia fedha za umma ambazo tunazitegemea.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa. Sasa ninakwita Mhe. Hussein Ibrahim Makungu atafuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Suleiman Sarahan Said jiandae.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsanate Mhe. Spika, mie kunipa nafasi hii kuchangia ripoti hii.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu kufika hapa salama katika Baraza lako tukufu, pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kunipa nafasi pia na mimi kuchangia ripoti hii ya Kamati ya *PAC* Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika, *PAC* Baraza la Wawakilishi 2016/17.

Lakini niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi kubwa iliyofanya mbali na changamoto, lakini kwa kusema ukweli Serikali hii ya Dkt Ali Mohammed Shein kwa 2010/2015 mpka 2017 nafikiri imefanya kazi kubwa sana na changamoto kubwa sana tumeweza kuziondosha. Mimi nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kazi yake kubwa na mbali ya hapo Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Rais kwa miaka mitano iliyopita alifany kazi na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo kazi ilikuwa ngumu. Lakini kwa hekma zake na busara zake aliweza kufanyakazi miaka mitano na Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa jukumu kubwa aliokuwa nalo na busara na hekma aliotumia kwa muda ule namshukuru na nampongeza na Mwenyezi Mungu amzidishie hekima hizo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi nianze tu katika ukurasa wa 8 wa kitabu hichi cha *PAC* katika ripoti yao nianze katika Wizara ya Mawasiliano kuhusiana Uwanja wa Ndege katika ripoti yao unaosimamiwa na Kampuni ya *ADPI*. Mhe. Spika, mimi niipongeze serikali sana kwa juhudi zake kubwa kwa kufanya kila njia na juhudi zote ule uwanja wetu wa kimataifa wa Abeid Aman Karume *terminal II* unafanyakazi.

Mhe. Spika, mimi niseme mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano miaka mitatu iliyopita nyuma. Kwa kweli tulikuwa tunafatilia ujenzi ule. Mhe. Spika, kwanza ujenzi ule ulikuwa umeshasimama na ushafeli kwa mujibu wa *structure* na lile jengo lenyewe lilivyokuwa. Lakini kwa juhudi kubwa ya serikali kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Fedha, ilifanya kazi kubwa kutafuta mkandarasi mwengine ambaye yule wa mwanzo alishindwa kuendeleza jengo lile alifeli nataka kusema, lakini akatafutwa mkandarasi wengine kupitia kwa Serikali yetu ya Zanzibar na ikampata mkandarasi huyu Mfaransa Kampuni ya *ADPI*.

Sasa mimi niseme Mhe. Spika, ripoti ya *PAC* imesema humu kama mkandarasi mikabata yote iliyokuja pale ya lugha ya Kifaransa. Mimi niseme kwamba Wafaransa mara nyingi hawapendelei kuzungumzia lugha nyengine isipokuwa yao wao. Na huyu Mkandarasi Mhe. Spika, tuliyempata kipindi kile na mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati nilijiridhisha na nilikwenda kutembelea na michoro yote niliiona, huyu ni Mkandarasi *International* ameshajenga viwanja vya ndege vingi katika dunia, sio kiwanja cha kwanza kile.

Kwa hivyo, uwanja ule mkandarasi huyu kaubadilisha ile ramani, michoro kwa uzoefu wake na kuufahamu. Mimi nashangaa sana Mhe. Spika, kuna Wajumbe wanasema ndege zitakuwa haziwezi kukaa. Pale Mhe. Spika, ndege zitaweza kukaa labda itakuwa hiyo *three eighty* ambayo haiwezi kuja kufunga pale kwa sababu ina midomo miwili, lakini ndege zote *Air bus* zitatua pale na zitafunga bila ya matatizo yoyote. Kwa sababu tusingefanya hivyo Mhe. Spika, fedha nyingi serikali ingepoteza na zile ni fedha za mkopo wa *Exim Bank* kutoka China.(Makofi).

Kwa hiyo, mkopo ule ulianza kwa Dola sabini na nane milioni, tukaja mia moja na ishirini na nne, sasa hivi iko mia moja arubaini na sita na sasa hivi tunaingia kwenye hatua ya mwisho hata juzi Mhe. Rais aliweka jiwe la msingi kufungua ujenzi wa *Airport* ile. Kwa hivyo, mimi naamini hili suala la lugha sio sababu, kwa sababu mkataba unawea ukatafsiriwa na mtu yeyote lugha ya Kifaransa ukimpa mtu anajua mkalimali atakutafsiria.

Kwa hivyo, hii sio sababu ya kumfelisha huyu mkandarasi au kuwafelisha Mamlaka kusema kama wamefanya ubadhirifu. Mimi nasema nawapongeza na ile *Airport* siku baada ya siku inajengwa na nashukuru kwa serikali yetu hii kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutaifungua *Airport* ile na ndege kubwa zinatua na juzi nilisema hapa kuwa changamoto zilizokuwepo kwa baadhi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar lakini tumeanza kuzitatua, hasa nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) alikwenda Bara akatutafutia kibali sisi Kamati ilikuwa inataka kutua ndege yeye akenda kwa juhudi zake na kwa udugu wetu tuliokuwa nao ndege zinatua Qatar inatua Turkish inatua ndenge nyengine zinataka zituwe ili tuweze kuulipa huu mkopo wa *Exim Bank*. Kwa sababu bila ndege kutua hatuwezi kupata fedha.(Makofi)

Kwa hiyo, mimi napongeza mkataba si sababu ya kuwavunja moyo wenzetu mkandarasi huyu ni hodari na anatumalizia *Airport* yetu kwa umakini mkubwa na ndege zitafunga pale tena uwanja wa kisasa hata uwanja ule Mhe. Spika, nilisema ulikuwa hauna madirisha, lakini mkandarasi huyu kwa mazingira ya

Zanzibar tuliona madirisha yawepo ili umeme ukizimika waweze abiria kupata upepo. Kwa hivyo ilibadilishwa ile *Airport* ili iwe *Airport* ambayo inakidhi mahitaji yetu.

Kwa hiyo, mimi naamini ujenzi ule mpaka sasa hivi uko salama na unakwenda vizuri wananchi wasubiri tufungue *Airport* kwa sababu *Airport* ni suala la miundombinu ni mikubwa sana katika nchi ni maendeleo makubwa sana katika nchi. Tunaposema sehemu ya *runway* ni nzuri, *taxiway* na *Apron* yote ni nzuri kabisa imejengwa ya kileo, ndege yoyote inaweza kutua hata hiyo three eight inaweza kutua Zanzibar ikitaka. Kwa hivyo, mimi naipongeza serikali kwa juhudi zake tena kubwa sana, naipongeza kwa dhati na Mwenyezi Mungu anatusaidia Uwanja wa Ndege ule utakwisha.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika kifungu cha 4 kuhusu Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mfuko wa maendeleo wa jimbo *CDF* kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 mpaka 2015. Mimi niishukuru sana *PAC* imefanya kazi nzuri, wamekwenda majimboni kukagua. Mimi sisemi wasiende, haya majimbo 9 wamekagua, lakini kuna majimbo 54, naomba wote wende wakaangalie hizi fedha zinazotoa serikali. Maana yake kwanza ilikuwa shilingi milioni 10, ikaja milioni 15 na mwisho ikaja milioni 20. Kwa hivyo, mimi naipongeza serikali kwanza kwa kutoa fedha hizi, kwa sababu zinawasaidia wananchi wetu maskini na wanyonge kwa ajili ya kuwajengea miraji katika majimbo yao, hasa suala la maji safi na salama ni shida kubwa katika majimbo yetu. Kwa hivyo, mimi naipongeza serikali ya Zanzibar kwa kutupa fedha hizi ili kuweza kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi niseme mpaka sasa hivi tangu uchaguzi umekwisha naiomba serikali ijitahidi sana fedha hizi tupate kupewa Wawakilishi zije kutusaidia, mpaka sasa hivi huu ni mwaka mzima bado fedha hizi hatujakabidhiwa. Kwa hivyo, mimi naomba ifanywe upesi, kwa sababu kuna changamoto nyingi na fedha hizi zitatusaidia ili kuwasaidia wananchi wetu kuwakwamua katika matatizo waliyokuwanayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nisikitike sana kwa upande mmoja nisikitike na ripoti hii, nilisema ripoti hii mimi sitoiunga mkono leo kabisa, kwa sababu kuna mambo humu yamenigusa mimi binafsi na kitu ambacho kichotokezea humu ni mashirikiano baina ya Kamati ya Maendeleo ya Jimbo na Mwenyekiti na Katibu, mimi sijapata kukaa na hiyo Kamati ya Mfuko wa Jimbo. Naweza kukaa na Katibu wangu wa jimbo. Mimi nilikuwa sipo nilikuwa Dodoma katika vikao vya Bunge, kwa hivyo sijapata bahati ya kukaa nao, nasikitika sana. Sasa kilichotokezea humu kwenye ripoti hii katika ukurasa wa 9. Nimetajwa sana

mimi kwamba nilikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, nimekwenda kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni.

Kwanza niseme Mhe. Spika, geographia ya Jimbo la Bububu, jina la Bububu limebakia jina la Bububu, lakini Shehia moja imetoka imekuwa Jimbo la Bububu. Shehia tatu Kibweni, Sharifumsa, Mwanyanya imebakia kwenye Jimbo la Mtoni. Kwa hivyo Shehia moja sawa na asilimia 25 ndio imetoka na asilimia 75 iko pale pale kwenye Jimbo la Bububu, wananchi wapiga kura waliopiga mwaka 2012 ndio wale waliopiga kura sasa hivi. Kwa hivyo, iliyotoka ni Shehia moja tu ambayo ndio ipo Jimbo la Bububu. Kwa hivyo mimi nimekwenda kwenye Shehia ambayo wapiga kura wangu wapo kule ambao ni Kibweni, Sharifumsa na Mwanyanya imeongzwa na Shehia ya Mtoni kidogo. Kwa hivyo, naamini wapiga kura ndio wale wale imebadilika jina kidogo tu.

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi niseme mambo yaliyoelezwa humu mashirikiano baina ya Katibu wa zamani na Katibu tuliokuwa naye sasa wa Mtoni ni tofauti na haiendani sawa, mashirikiano hayako mazuri. Katibu yule aliye sasa hivi Bububu anataka kuwa Katibu wa Mtoni kuwa Katibu wangu wa Kamati ya Maendeleo. Kisheria na kitaratibu ya mfuko huu haiwezekani. Katibu yule atoke Bububu aje kuwa Katibu katika Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mtoni, hivyo nimewaambia suala hilo haliwezekani, Katibu wa Mtoni yupo na ndio atakuwa yeye ndiye Katibu wa Mfuko wa Maendeleo ambaye ndio nitafanyakazi naye mimi kwa nia njema na safi kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo kwenye fedha hizi za mfuko wa *CDF*.

Kwa hivyo, mimi niseme Mhe. Spika, masuala yaliyoandikwa humu kwenye ripoti hii, mimi sijakubaliana nayo, naweza kusema ni ya uongo. Mambo yote yaliyofanyika kwenye jimbo hayajaoneshwa humu, kuna mambo yameelezwa sawa, kuna mambo hayajaelezwa sawa, siwezi kukubaliana na ripoti hii na *Hansard* iendelee kukaa. Naomba Kamati ya *PAC* ikiwa wako tayari kuanzia leo au kesho nikawaoneshe miradi niliyoifanya yote, kuanzia Mfuko wa Jimbo na fedha zangu mfukoni nimeongeza. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nimekuja na utekelezaji wa ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi hii hapa. Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha Novemba, 2016 hadi Februari, 2017. Mambo yote nimeyaandika hapa na hii nimepeleka Wilayani inapelekwa kwenye Ofisi Kuu. Suala hili limetekelezwa miezi mitatu, kwa ukweli na uwazi milioni 33,815,000, kwa muda wa miezi mitatu kutoka Novemba mpaka leo Februari na ushahidi upo, na kama hatuaminiani twende

kwa wananchi kimoja baada ya kimoja kitaonekana kilichofanyika ndani ya miezi mitatu.

Sasa leo Kamati ya *PAC* inaandika miradi ambayo niliyoifanya siyo, kitu ambacho hakiwezekani. Mimi nataka kusema humu imeandikwa Skuli ya Kibweni tumeweza kuchangia milioni 2 katika ujenzi wa skuli ile, lakini Katibu anasema nimechangia milioni 8, kitu ambacho kamati imekwenda kutizama Mwalimu Mkuu kasema hapa milioni 2 ndio zimeingizwa katika mradi huu. Sasa nani mkweli hapo, mimi mwenyewe nasema sio milioni 8 ni milioni 2. Kwa hivyo, hapa naomba iwekwe sawa, Katibu kasema kitu cha uongo. *(Makofi)*

Jambo jengine imezungumzwa mpaka mabasi ya wanafunzi humu. Kwanza mabasi ya wanafunzi sio pesa ya Mfuko wa Jimbo, ni pesa zangu mwenyewe. Mhe. Spika, mabasi niliyonunua sio Mfuko wa Jimbo ni fedha nyingi kuliko zile fedha zote za miaka mitatu zote hazifikii mabasi mawili. Humu imeandikwa Mwenyekiti ambaye ni mimi. Kasema kwamba hizi pesa za Mfuko wa Jimbo anashughulikia kutengeneza mabasi, ambapo ni kitu cha uongo. Mimi nasema mabasi ni mradi wangu mwenyewe nawasaidia wanafunzi wangu, kuanzia mafuta mpaka mambo mengine na madereva nawalipa mwenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niseme huduma ile siifanyi kwa ajili ya jimbo langu, nafanya kuanzia Kijichi, kama jimbo langu lilivyokuwa zamani. Kijichi mpaka mjini, asubuhi, mchana na jioni, watoto ni wengi, lakini na huduma hii ni muhimu sana kwa nchi yetu, ili wanafunzi wale wapate kusoma, mpaka yale mabasi nimeyaandika kwamba tushirikiane kulea elimu ndio msingi wa maisha na maendeleo. (*Makofi)*

Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mtoni tunafanyakazi hiyo kubwa, tunashirikiana na wazee ili watoto wale wende skuli asubuhi, mchana na jioni na tunawapeleka na kurudi.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe, muda wako umekwisha.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (BHAA): Mhe. Spika, nakushukuru sana. Lakini mimi siungi mkono mpaka Kamati ya *PAC* ijiridhishe kwa miradi niliyoifanya hasa suala la maji safi na salama.

Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Naomba nimwite sasa Mhe. Shehe Hamad Mattar, na muda kama utaruhusu Mhe. Suleiman Sarahan Said atachangia.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii. Kwanza nianze katika ripoti hii kabla sijaendelea ripoti ambayo Wajumbe wengi waunga mkono kwa jitihada iliyofanywa na kamati hii na mimi naiunga mkono ripoti hii mia juu ya mia.

Mhe. Spika, lakini na mimi kuna mambo tu baadhi yao naomba nikazie katika ripoti hii ambayo kuwa nimeyaona ni vyema tuelezane katika Baraza hili. Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Mwenyekiti kwa uwasilishaji wake lakini pia Kamati kwa kazi kubwa iliyofanya ambayo imeipitia takriban serikali nzima, kuona kwamba kazi hii iliyopewa inaifanya kwa muda mchache ambao haukutosha lakini ilijitahidi sana.

Mhe. Spika, pamoja na kazi tuliyofanya Kamati hii naipongeza kwa kupitia wizara ya ujenzi. Wizara hii ya Ujenzi ilifanyakazi kubwa sana ya ujenzi wa barabara zetu za ndani, kwa kutumia pesa zetu za ndani kupitia Mfuko wa Barabara. Kwa kweli kazi waliyoifanya kwa kupitia pesa zetu za ndani ni nzuri sana, tena kwa kiwango kidogo cha fedha tofauti ukiangalia fedha ambazo kuwa zimetumiwa na wakandarasi wa nje.

Kwa hivyo, naomba sana serikali kwa kupitia Mfuko huu wa Barabara au Mfuko Mkuu wa Serikali kuwapatia vifaa vya kisasa ili waweze kutengeneza barabara zetu kwa ustadi mzuri, kwani hivi sasa vifaa walivyonavyo wanaungaunga kushikilia mpaka uwezo wa barabara kufika kiwango kinachotakiwa. Hata hivyo, nyengine inakosekana kufanya hivyo kutokana na mitambo yenyewe ambayo imekwishachakaa. Kwa hivyo, naiomba serikali ifanye juhudi za makusudi kuweza kuvipatia vifaa hivi, ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, pia niiombe serikali wakati pale inapotoa amri ya kutengeneza barabara ambazo kuwa hazimo katika mpango wake wa utengenezaji kwa *UUB* wale, basi hawa wenzetu wanapata tabu sana. Kwa sababu wakati mwengine wamo katika kutengeneza barabara ambazo zimo katika mpango, matokeo yake mara wanaambiwa nenda katengeneze barabara hii baada ya siku tatu ipatikane au baada ya wiki mbili ipatikane, fedha hawajawapa. Sasa leo utamuambia vipi mtu akutengenezee kitu kizuri ambapo nyenzo hujampa. Naomba serikali inapotoa amri kama hii nayo iwawezeshe ipasavyo na kazi ile waweze kuitengeneza vizuri ili isije ikatokea lawama mmoja wapo akaweza kuambiwa atawajibika kwa kushindwa kufanyakazi ipasavyo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, kuunda kikosi kazi ambacho kitaweza kuzitunza hizi barabara zetu, kwa sababu barabara nyengine zinazotengenezwa zimo katika mazingira mabaya, miteremko. Kwa hivyo, kuwe na utaratibu wa kuzikagua mara kwa mara isichukuwe muda mrefu kabla hazijaathirika barabara zile ziweze kutengenezwa mara moja, kwani usipoziba ufa utajenga ukuta.

Mhe. Spika, naendelea kuishauri serikali ianzishe mpango maalum wa kuwachukua vijana wetu ambao wamo katika skuli kama zile za amali wanaoshughulika na mambo ya ujenzi, au skuli zetu kama zile za Mikunguni, kuwachukua na kuwaingiza katika yale makampuni yanayokuja hapa nchini na kufanyakazi kama za ukandarasi wa barabara, ujenzi wa majumba, ujenzi wa mabandari yetu haya, basi vijana wale kama tutakuwa tunawaingiza katika makampuni makubwa kama yale, basi wanaweza kuchota ujuzi ambao kuwa baadae hawa wataweza kujikusanya na kufanya kampuni zao na baadae kuwa makampuni ya wazalendo, na wao wakaweza kushindana na makampuni ya nje kuweza kuingia katika ukandarasi wa kazi zetu zilizomo nchini.

Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi pia vile vile naitilia mkazo kwa Serikali ya Mapinduzi kuona kwamba ipo haja ya kubadilisha vile viwango na kuanzisha viwango vyetu vya ndani, badala ya kutumia viwango ambavyo vimependekezwa Tanzania Bara kule kama ilivyosema ripoti hiyo, tuwe na viwango vyetu vya Zanzibar kama vile tulivyofanya kwa vitu mbali mbali kutegemea *ZBS*. Kwa hivyo, na sisi tuandae viwango vyetu tutakavyoona vinafaa, haidhuru kukopi baadhi ya mambo, maisha ni kuigana, lakini tuige yale mazuri ambayo kuwa yatatuletea faida kwa nchi yetu. Kwa hivyo, tuanzishe na sisi viwango vyetu, kwa sababu ripoti zetu hizi tunaona kwamba kila unapokwenda inatumia kiwango ambacho kinatumika Tanzania Bara, tufanye cha kwetu. Kama tunavyobadilisha sheria ziendane na nchi yetu. Kwa hivyo, na viwango tutengeneze vinavyoendana na nchi yetu.

Mhe. Spika, naendelea kuishauri serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuanzisha mfumo wa matumizi ya *US Dollar* katika mfumo mzima ule wa *IFMS*, hii itaondoa ule usumbufu kwa wizara ambazo zinahitaji kutumia Dola kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao kama vile Wizara ya Afya, tumeona wizara ya ujenzi Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, wataweza kuandaa bajeti kama Wizara ya Afya kwamba mwaka huu tutakuwa tuna wagonjwa kiasi gani na tunategemea kutumia kiasi fulani, kulingana na *ceiling* watakayopewa ile ili waweze kuweka Dola ngapi. Sasa fedha ile ikitokezea wakati wa matumizi wataweza kutumia katika wizara yao na kumbukumbu zitabakia pale pale.

Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita tuliona usumbufu, mpaka tunaanza kutiliana mashaka, lakaini baadae tulijiridhisha. Lakini ikiwa mfumo wa *IFMS* nao utaanza utumiaji wa US *Dollar* nao nadhani yataondoka matatizo kama hayo.

Mhe. Spika, niende katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ofisi hii ina majukumu makubwa sana majimboni kwetu na kwa nchi nzima. Lakini naishauri sana kuongeza posho serikali kwa ajili ya kuweza kuweka watumishi ambao kuwa, kama serikali imekubali kuweka zile ofisi za majimbo basi waweze kutunza nyaraka zitakazofanyika katika majimbo yetu, pindi wakiongezewa Wawakilishi posho hii, basi itawasaidia wale watumishi ambao watakuwepo pale ili na wao waweze kufanyakazi kwa utulivu na amani kabisa.

Jambo jengine Mhe. Spika, nimeona katika ripoti ambayo tumekabidhiwa hapa ya vitabu vyetu vyote ambavyo Wajumbe wote wanaona, basi nimeona kuna kasoro kubwa sana. Ni majimbo yote ambayo ni mengi sana yaliyopo Pemba ambayo yalikuwa yanashikiliwa na upinzani, katika utumizi wa fedha hizi zilizopewa ni mbovu sana na nyengine hazikutumika kabisa. Ni mfano ulio hai, katika ripoti iliyopitiwa na mkaguzi katika Jimbo langu la Mgogoni, hakuna hata mradi mmoja uliothibitishwa kwamba umefanya vizuri. Hapa ni dhahiri kwamba fedha ya serikali haikutumika vizuri na kwa sababu maalum. Wenzetu hawa walikuwa hawazitumii fedha za serikali hii kwa sababu kama wangefanya vizuri basi sisi tungekuwa na kazi ndogo sana, na pia kama wangefanya vizuri basi ingepata sifa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, kwa makusudi walifanya kutokuzitumia fedha hizi na wakatumia kwa mambo yao binafsi. Kwa hivyo, naiomba sana serikali yale majimbo yote ambayo kuwa hayakutoa kazi iliyotegemewa basi fedha hizo zirudishwe, hasa ukizingatia fedha hizi za mwisho zilizotolewa katika kipindi cha Juni, nyingi zao hazikutumika. Fedha hizi tunaomba zirudi tena majimboni tupewe zikiungana na hizi hapa, ili tuzifanyie kazi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi naendelea kuiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar. Waheshimiwa Wajumbe, muda uliobaki haumtoshi mchangiaji anayefuata, kwa hivyo waliobaki wataendelea kuchangia jioni.

Waheshimiwa Wajumbe, nina tangazo moja kutoka kwa Mnadhimu, anawaomba Wawakilishi wote wa CCM, mara baada ya kuahirisha hapa sasa

hivi, tukisitisha hizi shughuli zetu kwa mchana basi wabakie humu ukumbini kuna jambo muhimu anataka kuzungumza nao.

Baada ya hayo machache sasa naomba nisitishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka saa 11:00 za jioni

(Saa 7:00 mchana kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa hii kutoa maoni yangu mawili matatu katika kuchangia ripoti ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya PAC ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, nimepata muda mdogo wa kulipitia hili jalada lakini hata hivyo nitatoa mchango wangu ambao na mimi nimeona hivyo nilivyoona, mimi katika ukaguzi wa ripoti hii kitu cha kwanza ambacho nilikuwa nakitilia maanani sana nilikuwa nasema kwamba Sheria ni kitu muhimu sana katika kukabiliana na jambo lolote, hii ingekuwa tunafuata sheria na nidhamu tulizonazo makazini na ukweli wa hali halisi ya uwajibikaji kiutendaji basi matatizo mengi yasingetukuta, ni nia njema ya Serikali kuwawezesha Wizara ili kufanya mambo lakini baadae Wizara zikafanya mambo wanayotaka kwa kutokuwajibika vizuri katika kutokuona sheria inaweza ikamchukulia hatua gani au ikafanya kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, niishukuru sana kamati ya PAC jinsi ilivyo kuwa imefuatilia kwa kina maana yake mtu anapotaka hata risiti yoyote ile ina maana kafika pahala pa kufuatilia kwa kina, lakini kama mjumbe yoyote muhusika anafahamu Serikali kitu chake chochote kinataka risiti, kinataka makabidhiano sifikirii kama tungefika maeneo haya ya kuonyeshana vidole tukajua kwamba mtu huyu ana matatizo gani au ana matatizo gani. Kwa hivyo ningewaomba sana watendaji Makatibu Wakuu na viongozi wengine kuanzia Mawaziri tukafanya wajibu wetu ili kuepukana na tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, tuna misemo au tuna kawaida ya kwamba pesa ya Serikali inaonekana kama sio haramu ni halali kuitumia wewe unavyotaka mwenyewe, lakini pesa ya mtu basi ndio inaonekana ya haramu utakuta watu wana vilemba humu lakini kwa kuiba pesa ya Serikali hatari. Ukikimuuliza anasema pesa hii

labda haina mwenyewe si kweli zile ni nguvu za umma kila aina ya kitu kimechangiwa mule hata mlemavu kachangia mule, basi mpaka mlemavu na wewe unamla. Sasa ningeomba Serikali ikaangalia sana watu hawa ni wahujumu wa uchumi si lazima mtu mhujumu uchumi awe na sifa gani mtu yoyote anayeweza kuidanganya Serikali lazima na huyo ana matatizo yake pesa ya Serikali sio pesa ya kuchezea ni pesa ya umma inahitajika itumike pale ilivyokusudiwa. Nachangia hilo kuiweka wazi tu kwamba pesa ya serikali isionekane kama ni pesa ya shamba la bibi anavyotaka kuitumia mtu yoyote aitumie.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kamati hii lakini hii kamati wakati imeshaleta ripoti yake ili kuitendea haki kamati hii basi ifuatiliwe mambo yake ambayo amesema itizame isimuonee mtu, lakini mwisho wa habari yake basi utendaji wake uonekane kwamba umefanya *otherwise* itakuwa kama tumewatolea kafara hawa watu, kwamba waache waende wakaseme halafu tuwaweke ubayani lakini utendaji utakuwa hauonekani. Wakati mwengine tukija tukikaa hapa tukizisoma tena Ripoti za Kamati za mwaka mwengine tutakuwa kama tunatonesha kidonda pale pahali ambapo pameumia, kwa sababu hili suala limeshapita unalirudisha tena lakini matokeo yake hapana. Ningeshauri Mhe. Naibu Spika, hizi habari zilizosemwa humu ni mali ya umma ikafuatiliwa kwa kina na sisi kama Serikali ni kwamba inavuna pesa kama inatia pakachani inatia maji kwenye pakacha yanatokea pahali pengine.

Kwa hivyo Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Rais wanajitahidi kadiri ya uwezo wao kuzitafuta pesa popote zilipo kuziingiza katika sekta za Wizara ili ziende zikasaidie watu na maendeleo. Matokeo yake kama zinavuja zikiwa hazishughulikiwi basi kwa watendaji waliokuwa si waaminifu inakuwa ni tatizo.

Lakini Mheshimiwa mimi niseme baada ya kusoma ripoti kuna vitu ambavyo vinaniumiza kichwa, tunazungumza kwamba hii ripoti mambo yote ya Serikali yanakwenda kwa makabidhiano akiondoka kwenda Waziri utasikia leo Waziri anamkabidhi Waziri mwengine. Siku ya siku ikifika ukamwambia waziri kulipotea kitu fulani Waziri anakwambia nilikuwa sipo mie wewe ulivyokabidhiwa haya hukuyaona au mnakabidhiana kupeyana mikono tu, kwa sababu hili jambo mpaka lifikie kuja kuchomolewa huko miaka mitatu ishapita, miaka mingapi imepita yule mtu ameshakufa hayupo tena hawezi tena kuchukuliwa hatua tunapomfikisha huko tunakwenda kumuonea kwa sababu tulishampongeza na siku nyengine wakati wa kuagwa kama atakuwa amemaliza muda wake tunamfanyia shangwe kwamba utendaji wake ulikuwa mzuri kumbe uoza wake aliokuwa nao huku ulikuwa na hatari kubwa.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nasema hiyo Wizara haina ulazima kwamba lazima aje Mdhibiti wa Serikali kukuchukua wewe, wewe kama umeona mwenzako alivyoondoka sio salama wewe sema. Mwenzangu kaondoka lakini alichonikabidhi sio salama lakini unanyamaza kimya mpaka muda unafika anakuja Mdhibiti wa Serikali wa Mahesabu ndio anakuja kukwambia wewe kwamba kitu kilichofanywa huku, sasa yale makabidhiano ulikuwa wa kitu gani. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nasema sana kwamba mambo haya tulitakiwa sisi tuyatizame vizuri.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kwenye mikataba mibovu Serikali yetu mikataba mibovu maana yake tumeizoea na ndio iliyotufikisha hapa kila unapokwenda kwenye tenda unaambiwa barabara imeachwa nusu, nyumba mwenyewe kaikimbia, uwanja wa ndege haujulikani ulivyo lakini tunafika kusema hayo tu hatujifunzi tumemchukulia hatua nani wakanona mwenzao kachukuliwa hatua. Sasa ripoti hata ikisema mambo mia hii kama inakuwa haichukuliwi hatua hili linakuwa linaumiza na anayekuja mwengine nae anatafuta mpango wake wa kufanya, kwa sababu inaonekana huu mtindo unaendelea hakuna mtu anayeulizwa. Sasa Serikali hapa itabidi ijikaze kweli kweli lazima ifunue macho kwa wale watu ambao sio waaminifu iwachukulie hatua.

Mhe. Naibu Spika, nasema pia kila sekta humu niliyoisoma kuna watendaji maalum wanapoteza pesa kwa kila tofauti, siku nyengine kunataka kujengwa barabara ambayo pengine labda thamani yake ni bilioni moja basi mtu mmoja anaweza akafanya tenda ile ikapotea potea mpaka kuja kuitisha tena tenda ukaambiwa ni bilioni mbili na nusu, tumekataa bilioni moja tunakuja kuikubali tenda bilioni mbili na nusu. Sasa tunatoka wapi tunakwenda wapi, tumekataa moja tunakubali mbili. Hawa wote tusichukue tu kwamba huyu alikataa tutizame na yeye katika Serikali aliteuliwa Mhe. Rais anapomteua mtu anataka amsaidie sio aje ambomowe. Sasa Mhe. Rais kila siku anaposimama kwenye viriri anasema barabara yenu nitaitengeneza kitu gani nitawafanyia lakini akishusha pesa au akishusha mambo ya kule pesa zile hazitoshi.

Mhe. Naibu Spika, leo kama Uwanja wa Ndege ulipigwa thamani wataalam wote, watu gani wakasema bwana kima hichi kinatosha Uwanja wa Ndege hakikutosha, imepigwa thamani mara ya pili hakikutosha, imepigwa thamani mara ya tatu haijatosha sasa tunakwenda wapi. Tumebakisha tu tunakwenda pesa hazitoshi hazitoshi lazima Mhe. Rais kwa kweli tumsaidieni tusimuangushe, yeye anapochagua viongozi anahisi kwamba hawa watanisaidia lakini viongozi wengine wanakuwa sio waadilifu.

Mhe. Naibu Spika, jengine nataka niseme kwamba mambo mengi nayo huwa yanachangiana mimi ningeishauri Serikali mtindo wa risiti za mikononi ukapungua, risiti za mikononi zinakuwa zinazidi kila siku mtindo wa kupata *computerise* mambo yetu ambayo mtu anatia kadi anaondoka wizi unaweza ukaupungua risiti kila pahali shika mkononi, wengine wana vitabu viwili viwili, wengine wana mipango chungu nzima, mwengine anafanya jambo risiti anakwenda kuchukua baada ya miaka mingapi. Sasa hii nayo tungejitahidi haidhuru tungekata pahala lakini mitambo yetu ikaweza kufanya kazi ili kupunguza matatizo haya Mheshimiwa ya kuvuja kwa mapato.

Nataka nije kidogo kwenye Mfuko wa Jimbo, Mfuko wa Jimbo matatizo yake kila mmoja anautafakari vyengine, kila mmoja anaujua vyengine hasa huko nyuma mtu alikuwa akitia pesa mfukoni sasa umetungiwa sheria, umetungiwa mambo lakini nina wasiwasi kwamba inawezekana sote ni wageni wageni hatujajua maana halisi. Ningeshauri sana Waziri anayehisika na mfuko huu asichoke kuwafanyia semina wawakilishi kwenda kujua ule mfuko utatumika vipi baada ya kwenda kufanya migongano, kila mmoja kula ana uhuru wake pesa hizi zipo za Mwakilishi zipo za Mbunge, za Mbunge kule ni zake si za Serikali anafanya anavyotaka mwenyewe anazichukua pesa anafanya mwenyewe anavyotaka unamkamata mwakilishi, yeye anachukua zile pesa akitaka kwenda kusaidia timu za mpira anasaidia, akitaka kwenda kusaidia kitu gani anasaidia anasema hizi pesa zangu.

Lakini pesa ya Mwakilishi ya jimbo ndiyo mnayomkaba roho ikafanya mambo ambayo mumeshirikiana lakini nataka niseme na pesa ya jimbo Mbunge peke yake haitoi inaonekana na watu wa Halmashauri wanakula pamoja. Kwa sababu hawa lazima wangezuiyana kama unataka kutumia kwa hili lisingetumika, haidhuru yeye ndio anakuwa mwenyekiti lakini pamoja na yote lazima zile pesa ziende zilikolengwa sasa mmoja mnamkamata mikono mmoja mnamwachia ampige mwenzake hivi hatwendi lazima tuangalie kwamba na zile pesa sio za Mbunge, zile pesa za kuptia tu kwa jina la Mbunge lakini ni pesa za Wananchi kwa hivyo lazima utaratibu ufanyike.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia una dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Hamna shida Mheshimiwa tutakwenda tu vizuri, kwa kweli sisi wakati mwengine tunapata misaada lakini mtu kama anatupa misaada uliokuwa msaada wake una masharti mengi basi huo msaada hauna maana. Kwa sababu tayari keshajitia jina kama tumepokea msaada, msaada wenyewe unakuja na matatizo hivyo tokea lini Zanzibar kujua kifaransa. Mkataba umeandikwa kifaransa umeletwa wa kiarabu hapa umekaa

miaka kumi haujatafsiriwa lakini wa kifaransa ndio unaofanya kila kitu ni nani utasema mfaransa hapa ataweza kutizama mkataba ulivyokwenda.

Mhe. Naibu Spika, tunajenga jengo la Uwanja wa Ndege mikataba hairuhusu kumshirikisha Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ambaye ndiye atakayekuja kukabidhiwa kuja kuutumia, unajengwa Uwanja wa Ndege una vifaa vya umeme na kila kitu fundi wetu mkuu haruhusiwi kukaribia pale siku ikizima taa pale Uwanja wa Ndege tukamtafute Mchina ndio aje atuwashie taa. Sasa haya si madhila haya anayotufanyia lazima vitu vyengine tuweze kujua uwanja ukishajengwa huu basi….

Mhe. Naibu Spika: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Hewalla Mheshimiwa basi mimi naunga mkono hoja.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa muda angalau mchache wa kukazia Kamati hii, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati yetu hii kwa uwasilishaji wake mzuri wa kimahiri kabisa na wa uwazi kabisa naomba nimpongeze.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni mmoja mwana Kamati naomba nikazie kazie baadhi ya mambo tu kidogo, kwanza kabisa naanza na maslahi ya watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, maslahi ya wakaguzi ni kilio cha muda mrefu sana na nathubutu kusema kwamba kuwabana kimaslahi wakaguzi au watendaji wa Mdhibiti ni kuleta mwanya wa kuweza kufanya ubadhirifu wa watendaji wale. Watendaji wa Mdhibiti wana kazi ngumu kubwa kazi ya kwenda kukagua na kuchunguza hisabu za Serikali ili Mawizara na Mashirika yaweze kutumia fedha zile ipasavyo, unapombana mtendaji kimaslahi na nathubutu kusema tena kwamba hichi ni kilio cha muda mrefu kwa sababu mimi katika kipindi kilichopita nilikuwa kwenye kamati hii na hali halisi nilikuwa naiona wamekuwa wakiomba sana lakini mpaka leo bado maslahi yao hayaridhishi.

Mhe. Naibu Spika, Mhasibu na Mkaguzi wanasoma darasa moja wanasoma masomo sawa sawa lakini kimaslahi Mhasibu anakuwa na maslahi ya juu lakini mkaguzi maslahi yake hayaridhishi, wakati mkaguzi ndio anatakiwa awe na maslahi ya juu ili aweze kufanya kazi yake kwa uadilifu. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri hili aliangalia kwa jicho la huruma.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakwenda kwenye watendaji wa Mawizara ambao hawatoi ushirikiano na kamati kumekuwa na utaratibu na nadhani katika ripoti yetu tumetoa na tumeeleza kanuni na sheria ambayo inaturuhusu kwenda kukagua, kwenda kuchunguza na pia kutaka jambo lolote ambalo tunaliona linafaa katika Wizara husika, lakini bado kuna watendaji wanakuwa wagumu wanaona kama sisi tunafanya kiroja kwenda kuomba baadhi ya nyaraka katika mawizara. Kwa hivyo mimi naomba watendaji watoe ushirikiano na kamati ili na sisi tuweze kufanya kazi zetu vizuri, kwa sababu wao wakitoa ushirikiano ni kwa maslahi zaidi yao wao na ya jamii kwa jumla. Mhe. Naibu Spika, tumeona mfano jana hapa kutokupata ushirikiano baina ya kamati na Wizara ya Wanawake tumeona yaliyotokea, kwa hivyo nadhani kama watashirikiana na sisi mbele tukawa kitu kimoja na ndio tukaweza kufanya kazi vizuri na tunaweza kushirikiana na tukaelewana vizuri.

Mhe. Naibu Spika, halafu nikitoka hapo naomba nizipongeze taasisi zote za Serikali ambazo zimeweza kuwasilisha taarifa zake kwa Mdhibiti kwa wakati hili lilikuwa ni tatizo sugu kwani kuna baadhi ya taasisi nyingi ambazo zilikuwa hazioni umuhimu wa kuwasilisha ripoti zake kwa Mdhibiti kwa wakati, na tulipokuwa tukienda kwenye taasisi mbali mbali tulikuwa tunapata shida sana kuna taasisi wanaipa Afisi ya *CAG* wakati mgumu wa kutayarisha ripoti za kuwasilisha hapa Barazani, lakini kutokana na jitihada ya Kamati ya *PAC* ya kuwaelimisha na kuwaelewesha imekuwa sasa hivi kwa kiasi kikubwa Afisi nyingi zimeweza kuitikia wito nazipongeza na naomba sana ziendelee na msimamo huu ili kuweza kuirahisishia Afisi ya *CAG.*

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa kama nilivyosema nakazia kazia kwa sababu haya ni maoni ya kamati yangu nakazia kuhusu suala la matumizi ya Wizara kwa kutumia utaratibu wa *dummy.* Utaratibu huu nathubutu kusema ni mgeni kwa sababu mimi kipindi kilichopita nilikuwa mjumbe wa kamati ya *PAC* na kipindi hichi nimekuwa tena lakini utaratibu huu ndio kwanza mara hii tunaukuta katika matumizi haya. Sasa ninachokiomba mimi kwa kuwa huu utaratibu unaleta mashaka fedha zinatumika kwengine *Document* zinakaa Wizara ya Fedha ni maamuzi ya kamati lakini naomba nikazie kwamba utaratibu huu bora usitumike kwa sababu unaonekana ni utaratibu ambao unatia mashaka katika matumizi yake.

Mhe. Naibu Spika, mengi yameshazungumzwa lakini kwa kuwa na mimi ni mwanakamati nilikuwa naomba nikazie hayo. Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji wa ripoti hii ya PAC ya Baraza la Wawakilishi. Mimi nianze kwa kuipongeza Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuandika ripoti hii. Ripoti hii chanzo chake ni hoja za Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, hicho ndio chanzo chake kikubwa. Kufuatia kwa hoja hizi alizozitoa Mdhibiti ndivyo ambavyo tumekwenda tukapata masuala ya kuuliza, tukataka maelezo tukapata maelezo mengi tu, ndio tukaandaa kitabu hichi ambacho tunacho.

Niwapongeze wote wale ambao tulishirikiana nao wafanyakazi wa Wizara zote, ambao walitupatia taarifa muhimu ambazo tulizihitaji wakati wote. Mimi nitazungumzia masuala mawili matatu. Kwanza suala la bajeti ambalo ndilo tulilolifatilia. Halafu nitazungumzia suala la *procurement*, baadae tena nitazungumzia mambo ya majengo ambayo yanaendelea kujengwa.

Tukianza na *budgeting* kwanza kuna mapato na matumizi, sasa haya yote tunayafanyia bajeti, tunakusanya kiasi kadhaa na tutatumia kiasi kadhaa. Mara nyingi sana tumegundua kwamba mapato ama yanazidi kuliko vile yalivyolengwa au yanapungua. Hii sio mbaya kabisa, zaidi ikizidi ni faida kwa serikali na kwa nchi nzima kwa jumla. Lakini sasa inapozidi huwa tunataka maelezo kwa nini yamezidi ili tupate mambo ya kupendekeza, wazidishe nguvu zaidi. Hapa kidogo maelezo ambayo tulikuwa tunayapata mengine yanaweza yakatosheleza mengine hayatoshelezi sasa tukawagundua kwamba kuna upungufu wa ile ku-*budjet* yaani *smart budget*.

Bajeti tunazozifanya hazipo *smart* kwa maana ya *specific*, *manageable*, na *accurate.* Sasa utazikuta bajeti hizo kwa sababu haziko *accurate* ndio hivyo kwamba labda mtu anakaa mezani anakisia ntakusanya kiasi hiki matokeo yake ama kinazidi zaidi ya mara mbili au kinapungua zaidi mara mbili. Kwa hivyo tunashauri sana wakae waviangalie vianzio vyao vizuri halafu wafanye bajeti ambazo kwa kweli zitakua *realistic*. Pia wajue kwamba hata wakifanya hiyo *realistic budgeting* pia itakuwa na maswali, muhimu ni kwamba wawe tayari kujibu maswali kama vile ambavyo inatakiwa. Sasa nikiingia kwenye *procurement system* huku wenzangu washazungumzia mambo ya *tender*, mambo ya manunuzi mengine, wakazungumzia mambo ya *asset registration*, wakazungumzia ndani yake mambo ya *depreciation* kwa hizo *asset* wakazungumzia *store ledger* na *stock register* kwenye *store*.

Sasa mimi naweza kusema tu kwamba *tendering system* kama walivyosema wenzangu ni kwamba haiko vizuri ingawa sheria zipo, sheria za *tender* zipo lakini haiko vizuri, kuna baadhi ya wakati watu wanajiamulia tu kununua kwa

kukaa kikao ambacho si kile *tendable* ila wanakaa wanaamua kununua na wanatumia pesa ambayo ni kinyume na utaratibu ule unaotakiwa. Kwa hiyo tunashauri tu ile *tendering system* yote ifatwe kikamilifu, kama *tender* yenyewe ina *involve* kununua vitu kutoka nje basi zifatwe sheria za kununua vitu vya nje kwa kuwa na *tender* ambayo itakuwa ifuata masharti yote ya *tender* za nje.

Ikiwa *tender* zenyewe za ndani basi zikae *tendering committee* kama zilivyo ainishwa. *Tendering committee* nyingi sana utakuta hazijakamilika, ama hakuna mwenyekiti au hakuna kamati au hakuna mambo mengine wala hazikutani, sasa hili linakuwa ni tatizo. Tukiingia kwenye mambo ya *asset register* tunasema hakuna *proper asset register* tunaipendekezea Wizara ya Fedha ni afadhali watoe mfumo maalum wa ku-*register* hii *asset* ziwe aina moja, kuna wengine wanaandika tu kwenye karatasi za kawaida kwa mkono, wengine wanaandika kwa *type* sawa sawa, wengine sawa wanatia kwenye *electronic* sawa sawa kuna wengine wana mabuku maalum ma-*ledger* maalum.

Kwa mfano wenzetu wa *ZIPA* tuliona kwa kweli wale wamerikodi vizuri sana wana buku kubwa lina kila *register*, kila kitu chao wameki-*register* pale tatizo liliopo tu ile *depreciation method* kidogo haiko sawa kwa sababu *depreciation method* wanachukua ile *linear* ambayo *twenty five percent*, kila mwaka *twenty five percent* kila mwaka, miaka minne unakuta bidhaa haina thamani tena iko *ziro*. Tukapendekeza kwa wote Wizara ya Fedha, wasimamie wafanye *re-evaluation* kila baada ya mwaka au baada ya miaka miwili ifanyiwe *re-evaluation* iwekwe thamani upya halafu itafutwe *percent* ya ku *depreciate* ili mali ya serikali isipotee bure.

Kitu kingine ambacho tumekifatilia kwenye shughuli zetu hizi kwa mfano, wametoa kiasi fulani kutumia fedha kwa ajili ya pesa za kuwapa watu likizo. Ukitaka kupata maelezo au hizo barua zilizotoa likizo utakuta barua hizo ziko kwenye faili la kitu kingine kabisa, yaani hakuna ile *proper file system.* Kwa hivyo tutashauri kwamba kuwe na *proper file system* ambapo mambo ya likizo basi yaweko, likizo waliolipwa fedha zao wanaoneshwa pale ili ukaguzi uwe rahisi badala la kwenda kutafuta *file* labda limetiwa kwenye *file* hili au *file* hili ma-*file* kumi utayatafuta huwezi kupata kitu kimoja unachokitaka. Kwa hivyo tunapendekeza sana *filing system* iwe *proper*.

Halafu jengine mambo ya *record management*. *Record* nyingi sana hazitunzwi ipasavyo, utakuta risiti ukiitafuta haionekani lakini baada ya muda inakuja kuonekana, sasa tunajiuliza inakuwaje? Hii ni ukosefu wa kuweka *record* vizuri ili kila kitu kikitakiwa kipatikane kinavyotakiwa. Kwa hiyo pia tunaomba wizara husika itowe mfumo wa *record management* ambayo kila

wizara itaipata, mtu akitaka kitu fulani kimetumika vipi basi anavutiwa *file* anaangalia anaondoka.

Hii itapunguza kupoteza *time*, *time* siku zote kwenye *time management* tunaambia *time* ni *perishable time* ni kitu kinachooza, *time* hiyo hiyo huwezi kuibena na *time* hiyo hiyo inakuwa *irreplaceable,* ikikutoka imekutoka. Kwa hiyo wajaribu kurikodi kila kitu chao kiko *propert* ili akenda Mdhibiti anakuta vitu vyote sawa, ikenda PAC inakuta vitu vyote sawa, hatimae mambo haya yote pengine yanaweza kwenda ni *routine* tu lakini mambo yote yanakwenda sawa.

Halafu sasa mambo ya majenzi kuna majengo ambayo yanajengwa na sekta tofauti. Tunapendekeza kwamba usimamizi wa majengo haya uende vizuri ili pasiwa na upotevu wa fedha kwa kujenga majengo ambayo hayana kiwango. Pia tunapendekeza kwamba Wizara ya Fedha inapotoa ruhusa ya kujenga jengo fulani basi lifatilie na wao waone kwamba *value for money* inapatikana.

Mhe. Naibu Spika, mengine ambayo ningependa sana niyasisitize, kwenye kitabu hapa tune-note kwamba katika huu mfuko wa majimbo ile Kamati za Maendeleo inaonekana wengi hawapo pamoja na Wawakilishi wao waliowateuwa. Matokeo yake unaweza ukapewa maelezo ambayo yapo kinyume na matarajio ya mwakilishi. Mfano mdogo hapa mwenzetu alikuwa analalamika kwamba ile ripoti iliyoelezwa kwamba siyo sahihi. Ukweli ni kwamba tumekutana na wote waliokuwepo pale na wametoa maelezo hayo, tukayaandika tukayaleta hapa. Sasa ni vizuri sana wakae na watu wao wajue kitu gani wanaeleza Kamati yoyote inayokwenda ili itakapoelezwa tena isijekuwa kuna mgongano hili silo, hili sio, hili litaleta mtafaruku kidogo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza hayo Mheshimiwa kwa sababu mimi haya ndiyo tuliyoyatunga tukayaeleza, tuliyoyaandika na yameshazungumzwa yote naona nisichafue ladha iliyokuwemo kwenye kitabu hichi. Niseme nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 juu ya mia.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniona na mimi pia. Nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Tunguu ikiwa mimi leo nipo hapa kwa ajili ya kura zao walizonitilia mimi. Lakini pia kwa kuniamini ili mimi niwe msemaji wao hapa. Pia Wazungu wanasema *most of all* kuwa mtetezi wao katika hili Baraza la Kutunga Sheria.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza rafiki yangu Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi mahiri wa Jimbo la Chumbuni, kwa kuwasilisha ripoti yake kwa niaba ya kamati yao kwa ujasiri mkubwa na uthibitisho kuwa walifanya kazi kama Baraza na Mhe. Spika, anavyohitaji wao kuyatekeleza majukumu yao.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa mawazo yangu na fikra zangu baada ya kuipitia hii ripoti. Kwa kweli kama nilivyoeleza asubuhi kwamba ripoti hii ni nzito sana na mara yetu wengi wa kwanza kuipitia, asubuhi leo watu wa kuchangia walikuwa watu sita. Kwa mujibu wa Mabunge yanavyoenda ripoti kama hizi zinapokuja za PAC mara nyingi unakuta kunakuwa kunawaka moto, mapungufu mengi yanakuwepo. Kwa sababu hapa ndipo matumizi ya mapato mengi baina ya serikali tunapata kuyachambua na kuyaona.

Lakini ukiangalia kwa hali ilivyoenda tangu asubuhi huwezi ukasema kwamba yale yote yalivyokwenda kwamba ndivyo ilivyokuwa matarajio. Lakini naamini katika uzoefu tutakaojenga katika miaka ya mbele na sisi pia kwa ajili ya kuisaidia serikali na kuishauri na kufanya wajibu wetu basi tutazidi kusaidiana kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, mwakilishi wa Chakechake Mhe. Suleiman Sarahan alizungumza suala la risiti, ambalo na mimi pia nataka niligusie. Katika eneo moja ambalo serikali linafurahia sana ambalo wamefanikiwa katika kazi wanazozifanya ni kwenye Wizara ya Fedha kutumia *program* na *IFEM* hizi *program* zao. Lakini pia katika mnasaba huo huo ili kuendeleza utamaduni huo wa kutumia aidha katika masuala ya *electronic system* juu ya mapato, ukiangalia kuna suala moja muhimu sana inabidi tulizingatia ni suala la umeme na *back up unit.*

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi ukenda katika taasisi ya serikali unakuta wakati mwengine yapo maeneo pesa za kutia umeme au fedha hawana na umeme umekatika. Kuna maeneo unakwenda unakuta fedha za kununulia ile *ink* ya *photocopy* hamna. Kwa sababu kwenye *OC* au jambo kitu kimetokezea, sasa tunapotaka kujitayarishe katika mwenendo wa kwenda kuhakikisha kwamba tutakuwa tuko sawa, basi tuhakikishe katika maeneo yote tutakuwa tupo sawa kwa mia juu ya mia. Kwa hili ningeshauri sana kuwa kuna *strategy* ya moja kwa moja kwa mpango huu wa serikali ambao umekusudia kuuweka wa *e-government* ambao umekuwa ni gumzo ndani ya Baraza hili lakini pia Baraza lililopita. Naamini katika bajeti ya mwaka 2017 kuelekea 2018 suala la *E-Government* tena litakuja na itakuwa mjadala.

Baada ya hapo nataka nizungumzia suala la *Airport tax. Airport tax* kwa mujibu wa utaratibu nikisoma katika *Airport* nyingi sana duniani, fedha hizi zinazokusanywa katika *Airport* mara nyingi hubakia *as a retainer* ili kujiendeleza wao katika masuala mbali mbali. Lakini *Airport Tax* hii inapotoka pale *Airport* inakwenda zake moja kwa moja mpaka Hazina. Hii naamini haina tofauti pamoja na ile *infrastructure tax* ambayo iko upande wa Shirika la *ZECO* ambayo inakwenda zake Hazina pamoja na *skill develoment levy* pia kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, fedha mara nyingi hizi sheria zake tunatunga kwa ajili ya malengo fulani lakini mwisho wake zinakwenda Hazina hizo. Nakumbuka Mhe. Dokholo alisema juzi alitumia neno la kipepeo hapa lakini sitaki kutaja alikusudia kwa maana gani, lakini hizi pesa zinaondoka zake moja kwa moja. Ukiangalia leo *Airport Tax* pale *Airport* katika mazingira ambayo wanayoyahitaji na kwa kazi ambazo wanazifanya kwa kweli inasikitisha sana na mengi wameweza kufanya. Yaani kila eneo wanahitaji fedha za ziada ili yule ng'ombe anayetoa maziwa aweze kuzidi lakini ukiangalia panakuwa pana hali ngumu, mazingira wanafanya kwa tabu kabisa, leo panapigwa tofali hapa, huku ukiangalia *Airport* ambayo ni *Terminal II* bado ina muda mpaka serikali ije kukamilisha na ufunguo wawakabidhi wale. Lakini pia nina wasiwasi hapa kuna mikataba ya Kimataifa tutakuwa tunaivunja. Kwa sababu kitendo cha hii fedha kuondoka hapa kwenda zake Hazina, ningeishauri serikali waiangalie vizuri sana, isiwe tunafanya jambo halafu baadae likaja kutuumiza sisi katika mikataba huku ya kimataifa tunojifunga.

Suala la tatu nataka nilizungumzie suala la la *Prison Island* ambayo ni maarufu. Wageni wengi wanakwenda kule kwenda kuangalia kobe. Kisiwa cha *Prison Island* wamepewa wawekezaji muda mrefu kwa lengo la kukiendeleza pamoja na wale wanyama wetu tuliokuwa tunao kule kama kobe. Kule wageni wanapenda kwenda kutembea kwenda kufanya *snorkelling* kuburudika na maji na kupumzika. Lakini nawaamini wakati walipopewa mkataba huu walikuwa wahakikishe kwamba wanaendeleza na hoteli. Hoteli imefungwa, lakini hoteli inapofungwa ina maana serikali inakosa mapato, lakini pia katika suala la *job creation* kwamba sisi tunaamini kwamba kazi ni muhimu pia lakini pia na kupata mapato. Naamini ingekuwa leo hoteli inaendelea kwenye kisiwa cha *Prison Island* ingekuwa kuna zaidi ya watu 100 wameajiriwa moja kwa moja. Karibu ya ajira 100 tumezikosa *just like that*, hoteli imefungwa mara inafunguliwa mara inafungwa muda mrefu.

Ukiangalia kwa mujibu wa majibu niliyopewa na Mhe. Waziri wa Ardhi juu ya fedha ambazo zinalipwa katika kukodishwa kile kisiwa kwa kweli nilisikitika

sana. Mimi namshauri sana Mhe. Waziri pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili waliangalie suala hili. Kwa sababu hichi Kisiwa tunasema sisi *it an asset for Zanzibar, it is the beautiful Island,* lakini pia kumkuta muwekezaji anafaidika na makobe wetu, anatengeneza pesa zaidi kuliko hata pesa ambazo sisi tunamlipa yeye kweli hii tunamtendea mtu haki na wananchi wa Zanzibar. Hebu maeneo kama haya yapitieni tena, tunawakamua wawekezaji huko maeneo mengine lakini maeneo ambayo serikali inatakiwa iyafatilie tunayaachia. Unamkuta mtu kama nilivyosema jana, mtu analipa dola 30 kwa chumba mnakwenda mnamkamua dola 9 kwa *per head* kwa hivyo dola 18 zinabakiwa dola 12 abakiwe nazo yeye. Sasa haya ndiyo maeneo serikali inabidi iangalie upya kwa kupita moja kwa moja juu ya mapato yao na matumizi wanayo kwenda nayo kwa pamoja.

Lakini nataka nizungumzie suala la *SUZA* limezungumzwa suala la gari. Hapa Mhe. Naibu Spika naomba ni *declare conflict of interest* kwamba mimi haya maneno nitakayotoa hapa ni kwa ajili ya faida ya Baraza kwa sababu mimi ni mjumbe wa lile Baraza la Chuo Kikuu cha *SUZA* na pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya *Auditing* ya *SUZA* na mjumbe wa Kamati ya Fedha, japokuwa kuna kikao kilichopita sijahudhuria lakini naomba nitoe taarifa kulisaidia Baraza lako.

Kwanza niseme kwamba hakuna utaratibu wowote ulovunjwa kutokana na hii ripoti ilivyowekwa hapa na hakuna fedha zilizopotea za Serikali *issue* iko ni hivi gari lilinunuliwa mwaka 2012/2013 ni *Jeep Shells* ni gari ya kimarekani lakini kila muda ulivyoenda ilikuwa inapata matatizo kwenye *computer* kutokana na uhaba wa mafundi Kamati ya *Auditing* yetu tukaishauri Baraza tukapeleka ripoti kwamba tunaishauri Baraza hii gari labda tuiuze ili tuweze kupata gari ya kijapani inaweza kutusaidia moja kwa moja pamoja na VC wetu. Baraza likapitisha hiyo gari kwamba tukapata baraka za Baraza tukaelekezwa tuwandikie barua Wizara ya Fedha, barua ikaandikwa Wizara ya Fedha na Uongozi wa Chuo barua ikarudi tukaletewa maelekezo kwa utaratibu wa sheria za serikali jinsi ile sheria inasema ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali na gari ilipigwa mnada pale *American Corner* pembeni ya *Ben Bella* ilikuwa jioni saa 10:30 mpaka 11:00 mwezi uliopita na mimi mwenyewe nilikwenda nikaona.

Gari ile ilinunuliwa mwaka 2012 kwa milioni sabini na nne(74,000,000) siku ya mnada gari imeuzwa kwa milioni hamsini na nane (58,000,000) kwa hiyo Chuo cha SUZA wanastahiki kupewa pongezi ukiangalia kwa *depreciation* ya gari Uongozi wa SUZA unatakiwa upongezwe kwa sababu imechukua maamuzi haraka kabla ile gari haijakuwa mzigo. Sasa jee hizo fedha

zimelipwa au hazijaliwa hadi hivi sasa pesa zililipwa kati ya tarehe 19/10/2016 na tarehe 6/12/2016 milioni hamsini na saba (57,000,000) zimeshalipwa ndani ya chuo kabisa, na hili nimeli-*confirm* mimi leo kabisa, kwa hivyo naomba taarifa hizi nilisaidie Baraza lako tukufu ili kuweka rekodi sawa na gari hii ili kupitia utarazatibu wa kisheria kama ripoti inavyosema kwamba ilibidi bodi ishirikishwe ya zabuni hiyo sio utaratibu ni Wizara ya Fedha wenye mamlaka wao ndio wanaaotowa maelekezo yote juu ya mali ya serikali. Kwa hiyo baada ya maelekezo hayo sasa napenda nende moja kwa moja katika swala la *ZANTEL* naamini hizo taarifa nilizotoa Baraza lako watafaidika nazo.

Nilikuwa nataka niulize suala la *ZANTEL* Mhe. Naibu Spika juzi Mhe. Waziri wa Fedha hapa alijibu kwa manjonjo sana kwamba moja kwa moja kwamba sababu hizi *share* zetu kushuka kutoka 18 mpaka 15 ni kwamba Kampuni ya *MILLCOM* iliekeza ndani ya moja kwa moja kuhakikisha kwamba ili kuendeleza kampuni, lakini Mhe. Naibu Spika na waheshimiwa wajumbe mimi hadi leo najiuliza kitu kimoja miaka 15 *ZANTEL* imekuwa ikitoa huduma na *share* zetu zilikuwa ziko 18 katika miaka 15 *share* zetu zimebakia 18 hakuna hata mwaka mmoja isipokuwa mara moja tumepokea *dividend* tukalipwa sisi fidia yetu ni mara moja.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha

Mhe. Simai Mohammed Said: Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika katika yote 15 na *ZANTEL* imelipa serikali fidia mara moja lakini *share* zetu hazijawahi kunyanyuka hata mara moja zikaenda 25 kwa hivyo hili serikali iangalie na itupe majibu kwamba japokuwa hata kama waliekeza lakini nao pia wajumbe wetu ambao wanaoshiriki katika bodi ya *ZANTEL* ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Katibu Mkuu wa Mawasiliano wawe wakali walinde hizi *share* za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya niliyoyatoa hapa niseme ahsante sana nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na niseme naunga mkono hoja na naamini ripoti hii itatusaida sisi sana wakati wa bajeti. Aahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai nimepata mchangiaji mwengine hapa kwa upande wa *back benchers* nitampatia Mhe. Raza kabla ya Mhe. Said Soud, Mhe. Raza nakupa dakika tano Mheshimiwa nafikiri zinakutosha.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye hii kamati ya ripoti ambayo iliyosomwa mbele yetu niwapongeze kwa hekima zao, busara zao na usikivu wao na niipongeze wizara inayohusika yote.

Mhe. Naibu Spika, hii kamati ni nzito ni kamati ambayo ndiyo inayosimamia bajeti mimi ushauri wangu Mhe. Naibu Spika wakati tunapata nafasi ya kamati hii kuijadili ni uzuri wawakilishi wenzangu siku kama ya leo au siku kama ambayo kamati hii inawasilisha kwetu sisi ningelitoa tu mawazo kwa wawakilishi wenzangu wote siku hiyo isiwe siku ya masuala na majibu, kwa sababu tukiingia kwenye masuala na majibu tunafika mpaka saa tano na matokeo yake tunakuwa na muda mdogo na wakati mwengine sisi ni wataalamu kwa hivyo Mhe. Naibu Spika mie ushauri wangu tu kwa wenzangu kwamba vitu kama hivi vinavyokuja hasa kamati hii ningeliomba tukubaliane na wenzangu wawakilishi huku mbele kwamba siku ile tukubaliane sote isiwe siku ya maswali na majibu tunaingia saa tatu Mwenyezi Mungu akitupa uhai na uzima tunakwenda moja kwa moja kuteremka na kamati hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kamati hii imezungumza mengi lakini hili tatizo ni kubwa tumeshuhudia ripoti hii imezungumza mambo mengi ya wizara mbali mbali lakini Mhe. Naibu Spika haya yote yanatokana na ule umimi umimi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi ningetaka kutoa rai kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ninampongenze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Naibu Spika, tusije tukaruhusu hata siku moja tukaachia wizara zote zikatafuta pesa halafu zikajiamulia mwenyewe mimi bado nasema namuomba Rais pesa zote ziingie kwenye hazina. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kukosekana hivyo Serikali hii tutadaiwa baadaye zaidi ya miaka mia kwa hivyo ushauri wangu Mhe. Naibu Spika kwa Serikali hii tusije tukaweka mteremko wa kusema kila wizara ichukuwe, matokeo yake pesa za mishahara tutakuwa hatulipi kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba, na ushahidi huu ninao.

Mhe. Naibu Spika, sisi sisi tuliokuwemo humu ndani na sisi sisi tulikuwemo mawizarani kuna watu *special* hutengeneza tu mikataba husema inakuja kuidai Serikali bilioni nne, bilioni tano tena unafika mpaka kwa Rais wanafika mpaka kwa viongozi.

Mhe. Naibu Spika, ushahidi huu upo lakini kama sio ukakamavu wa Wizara ya Fedha, sio ukakamavu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Mhe. Naibu Spika,

Serikali hii ingekuwa leo tunadaiwa. Kuna watu hapa kazi yao kutengeneza tu mikataba hewa awamu iliyopita wanakuja wanasema wanadai bilioni sita hakuna bilioni watu wanatembea kwenye *briefcase* na milioni mia nne mia nne. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika miye niwapongeze na tujipongeze lazima tuwe na uchungu na nchi.

Mhe. Naibu Spika, vitu hivi utakuta watu wengi kwenye sehemu mbali mbali huenda kwa Kamati ya Ufundi kutaka kuwakomoa tu watu wachache wenye uchungu na nchi. Mhe. Naibu Spika, hayo tumekuta katika mradi huu wa wizara kwa awamu iliyopita mawaziri waliotangulia siyo Maalim Rashid, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetumia mabilioni ya AGAPE sijui EPA, maana hata kuzitaja mheshimiwa mpaka ule vidonge mimi nina ushahidi wa kutosha *billions* zimelipwa pale kwa sababu Mhe. Naibu Spika, Rais wetu Dk. Shein ni mtu msikivu anapenda maendeleo, anapenda hekma, anapenda maendeleo ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, waziri anapanga jambo anakwenda kwenye Baraza anatisha anasema sasa hivi nchi nzima umeme utazimwa wa AGAPE sasa unapokwenda unajua sicho unamshtua Mhe. Rais, Baraza matokeo yake pesa zinaruhusika Mheshimiwa zaidi ya milioni tano dola zimetumika ripoti hiyo ninayo na wakati wote naweza kutoa ushahidi huo na nilikuwa mjumbe wa kamati.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunachokipata ndio tunachokitumia kwa hiyo miye nashauri Mhe. Naibu Spika, fedha hizi lazima tuwe waangalifu ile pale leo tumesoma kwenye ripoti imeandikwa, wanasema ripoti imeletwa kifaransa hayo umepata kusikia wapi Mhe. Naibu Spika, Zanzibar hii tunaletewa mkataba wa lugha ya kifaransa maana ingelikuwa humu ndani kuna wafaransa tungekubali tungeletewa lugha za kihindi na sisi tukaweza kufahamu hii lugha ya kihindi. Lakini humu mfaransa hayumo, sasa unapokea mkataba kwa lugha ya kifaransa ambao mkataba haupo matokeo yake ile pale mimi nimshukuru sana Rais wa Zanzibar na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria bila yao ile *Airport* inayotaka kuja kujengwa Mhe. Naibu Spika tungelikaa miaka hamsini. Lakini kwa hekima ya Rais wa Zanzibar kwa hekima ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu leo *Alhamdulillah* lile jengo litafidiwa bila hasara yote.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, miye nimalizie kwa kusema kwamba lazima tuwe watulivu, lazima tuwe na hekma, lakini lazima tujuwe tunachokopata ndio tunachokitumia.

Mhe. Naibu Spika, ripoti zote hizi tusipoangzalia Mhe. Naibu Spika, tutakaa tunamalizika tu tunakaa kwenye bajeti ya miezi miwili tunazungumza ripoti sasa ripoti hii tusipopata muda na tusipozungumza Mhe. Naibu Spika, tutakuwa tunaumia kwa hivyo kuna sehemu nyingi mikataba mibovu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Raza malizia.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, mimi niishukuru Serikali kwa jumla nimshukuru Rais wa Zanzibar na uongozi lakini nasema tusije tukafanya kosa tukaziruhusu hizi kodi ndogo ndogo hizi za barabara za nini tukasema tuje tuwaachilie wenyewe tutakuja hapa mshahara hata sisi posho yetu tutashindwa kupewa Mhe. Naibu Spika, na sisi ndio wa kwanza kupiga kelele.

Mheshimiwa mimi naunga mkono lakini tuwe watulivu kamati kama hii, ripoti kama hii lazima ipewe muda wa kujadili naunga mkono asilimia mia kwa niaba ya wananchi wa Uzini. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Raza mchangiaje mwengine anayefata ni Mhe. Waziri asiye na Wizara Maalum Mhe. Said Soud baada ya Mhe. Said Soud atafuata Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mhe. Mohamed Ahmada.

Mhe. Said Soud Said (Waziri asiye na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kwanza nichukue nafasi ya kuwashukuru wajumbe wa kamati ya PAC na napenda kusema kwamba naunga mkono ripoti yao mia kwa mia.

Lakini pia ningetaka tu niseme kwamba niwapongeze kwanza kwa kusema kweli wamejitahidi sana kusema kweli katika ripoti yao hata pale walipoona mapungufu basi pia na yake mapungufu wameyasema sasa hii moja katika sifa ya kamati hii kwamba wamefanya kweli.

Lakini pia ningetaka niseme kwamba Dira ya Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Ilani ya Uchaguzi, kama tunataka maendeleo ndani ya Zanzibar hii lazima twende na Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika mazingira ya kuwatumikia Wanzazibari.

Mhe. Naibu Spika, ningetaka niahidi katika Baraza hili kwamba hoja hii ya PAC nitaipeleka kwenye Baraza la Mapinduzi kwa maana ya kuwaombea kuwa na meno yaani nataka wawe na meno wanapokwenda kumuhoji mtu hataki

kuhojiwa wamchukuwe kwa polisi. Kwa sababu kinachotumika hapa ni pesa za Wazanzibari wengine wanaziingiza kwa mifuko ya nyuma inatokea mbele halafu wawakilishi wanapiga kelele hapa kwa vile, kimsingi haiwezekani mtu anaitwa na Ofisi ya Makamu wa Pili halafu anarudi hapatikani mtu hiyo ofisi ya Makamu wa Pili inashindwa kupata ripoti ya pesa zile ambazo zimepelekwa katika jimbo. kwa hivyo ni vizuri tukasema kwamba Baraza la Mapinduzi litaombwa na nitaliomba mimi litoe meno kwa kamati hii ili watu kama hawa ambao hawataki kushirikiana na Kamati ya *PAC* wadhibitiwe mara moja.

Mhe. Naibu Spika, ningetaka nisema kwamba maendeleo katika majimbo yasingojee pesa za mfuko wa maendeleo, maendeleo katika majimbo yanahitaji kuzalishwa na mbinu muafaka za wawakilishi wenyewe kwa vile sisi wawakilishi tusiwe wavivu wa kufikiri kupeleka maendeleo katika majimbo yetu, kwa kisingizio cha kungojea pesa kutoka Serikalini.

Mhe. Naibu Spika, wawakilishi ndio changamoto na ndiyo chemchem ya maendeleo katika majimbo ambao wangeweza kuzalisha pesa na pesa hizo zingeweza kutunisha mfuko wa maendeleo wa jimbo. Ningetoa mfano ulio hai kwa mfano mzima kabisa Jimbo langu la Wawi kama kutarudishwa mchezo wa ng'ombe na watu wakauziwa tiketi za kutizama ng'ombe pesa ile ikachukuliwa ikaingizwa katika mfuko wa jimbo maana yake maendeleo katika Jimbo la Wawi yatakuwa na yataongezeka. Kwa misingi hiyo ni vizuri sasa tukakubaliana kama sisi ndio wawakilishi tukawa tayari kuanzisha mambo mbali mbali katika majimbo yetu yatakayowezesha kukuza mfuko huu wa maendeleo ya jimbo na baadaye tukaweza kupeleka maendeleo ya jimbo licha ya kutaka pesa hizi labda ziingie katika mikono ya wawakilishi badala ya kutumika katika mfuko wa maendeleo ya jimbo ukaingia katika mfuko wa wawakilishi wananchi watapiga kelele zile zile.

Lakini kama zitaingizwa katika mfuko wa maendeleo ya jimbo na Kamati ya PAC ikapewa meno pesa hizi zitatumika kihalali. Kwa vile ni vizuri sasa Mhe. Naibu Spika tukawa tayari kuwatumikia wananchi kwa namna mbali mbali ambazo tumeagizwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika mazingira ya kuwapelekea maendeleo.

Changamoto ambazo zinajitokeza mbali mbali katika majimbo Mhe. Naibu Spika ni kukosekana kwa mashirikiano kati ya wawakilishi na wananchi, mwakilishi anakuja hapa anasema kwamba kwa niaba ya wananchi wangu lakini hana hata siku moja alowita akawahoji akawaeleza au akawambia tufanye nini katika jimbo hili ili tuweze kuleta maendeleo. Licha ya kwamba Chama cha Mapinduzi kesho na keshokutwa pamoja na vyama vyengine

vinakabiliwa na uchaguzi wa mwaka 2020 natoa tahadhari kwa wawakilishi wenzangu kwamba bila ya kuifanyia uhalali ilani ya Chama cha Mapinduzi tutakabiliwa na kazi ngumu. Kimsingi ilani ya Chama cha Mapinduzi na Katiba ya Zanzibar imetoa uhuru kwa mwakilishi kuwa tayari kuhakikisha kuwa jimbo lake analitumikia usiku na mchana. Sasa leo inakuwa kuwaje tuwe tunasubiri mfuko wa Serikali milioni kumi, milioni kumi kumbe sisi katika mwezi pale kwenye jimbo tunaweza kuzalisha milioni hamsini.

Ng'ombe wakitoka Wawi wakachezwa Vitongoji, wakachezwa Unguja, wakachezwa Dar es Salaam pesa itaingia Wawi, beni likitoka hapa likaja likapigwa Chake Chake pale pesa itapatikana. Wakichukuliwa wale ambao wanauwezo wa kupiga taarab wakapelekwa katika mahoteli makubwa makubwa wawakilishi mkisimamia pesa itapatikana. Lakini hakuna maana ya kungojea mfuko wa Serikali kumbe sisi tunaweza kuzalisha mifuko mbali mbali na hatimaye mifuko ya jimbo ikatanuka na maendeleo yakapatikana, penye uhaba wa barabara, penye uhaba wa maji, penye uhaba wa umeme mambo yakaendelea kupatikana leo inakuwa kuwaje katika mazingira kama haya ndugu wawakilishi kwamba sisi kazi yetu tunangojea kifungu cha pesa cha serikali halafu hicho hicho tukipigie danadana.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Said Soud, waheshimiwa nafirikia nazungumzia zaidi Waheshimiwa Mawaziri ni baada ya Mhe. Mohamed Ahmada ambaye kuna baadhi ya ufafanuzi atautoa lakini ni matarajio yangu kwamba kutakuwa na mawaziri wengine ambao wameguswa moja kwa moja wizara zao katika ripoti hii watakuwa labda na ufafanuzi kama upo sawa kama haupo basi tutaendelea na shughuli nyengine. Hapa sijapata jina la waziri hata mmoja, nimepata tu Naibu Waziri. Kwa hiyo, namwita Mhe. Ahmada Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii adhimu angalau kuchangia japo kwa muhtasari ripoti hii tuliyowasilishiwa hapa leo na Mwenyekiti wetu mahiri Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ripoti yao hii nzuri ambayo kwa kiasi fulani imegusa hisia za wajumbe wengi hapa na vile vile imeweza kugusia wizara mbali mbali katika yale masuala ambayo walikuwa wana shaka nayo na wameyaleta katika kamati yao

na taarifa yetu hapa leo ili wapate kuwasilisha na vile vile wapate ufafanuzi kutoka kwetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitokuwa na mengi ya kuchangia isipokuwa tu nitakuwa na mambo machache ambayo yanahusu wizara yetu. Kulikuwa na baadhi ya wajumbe walielezea kuhusu hizi bilioni 4.94. Je, hizi pesa zilitumika vipi? Kwa ufupi Mhe. Naibu Spika katika hii ripoti utaona kwamba pale inaoneshwa nani aliyelipwa na kuna *D.P Shapryia* na vile vile kuna *Dummy*. Sasa kuhusu nini maana ya *Dummy* nina imani kubwa sana Mhe. Waziri wa Fedha akija hapa atawaelezea kwa urefu zaidi wapate kufahamu wajumbe na wapate kutolewa shaka kuhusu matumizi haya ya Tsh. Bilioni 4.9.

Kuhusu *D.P Shapriya* sisi tulikuwa tunamlipa kwa mujibu wa ushauri tulivyopewa na Mshauri Elekezi. Kwa hiyo, baada ya kupata ushauri wake sisi ndio tulikuwa tunafanya hayo malipo kupitia sekta husika.

Vile vile Waheshimiwa Wajumbe, waligusia kuhusu viwango vya barabara zetu za ndani na barabara nyengine. Kusema la kweli viwango hivi ni viwango ambavyo vinawekwa na sisi tunafata *standard* za Uingereza. Lakini kwa ufupi tu tunapenda kuwaambia wajumbe kwamba wenzetu Tanzania Bara mfano *TANROAD* wameanza kuweka viwango fulani ambavyo wanatakiwa wale wakandarasi wanapokuja kufanya kazi za ujenzi hasa barabara basi wawe wanazifuata. Sisi tutauchukua huu ushauri na kuangalia namna gani ya kufanyia kazi, lakini kwa mujibu wa sheria yetu ya ununuzi na uondoshaji wa mali za serikali ni lazima hizi zabuni zitangazwe kwa tenda iliyo wazi na tena yenye kufuata masharti ya uhalisia.

Sasa inapokuja tenda ya wazi tunakuta kwamba inakuwa vigumu kama sisi kuweka *specification* maalum za kusema barabara fulani tutaijenga kwa kiwango cha pesa fulani. Hii inategemea mazingira ya sehemu husika barabara zinazojengwa zikiwa fupi au zikiwa refu au zikiwa pana Mikoa ya Pemba itatofautiana na Mikoa ya Unguja na Mkoa mmoja utatofautiana na Mkoa mwengine kutokana na mazingira ya sehemu husika. Zipo sehemu unaweza kukuta kuna milima, kuna sehemu unaweza kukuta mito, kuna sehemu kunataka kujengwa madaraja. Lakini ushauri wao sisi tutauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile lilizungumziwa suala moja hapa ambalo kusema la kweli kuhusu uwanja wetu wa ndege ambao *Terminal II* hivi sasa tunaijenga. Sote ni mashahidi kwamba Mkandarasi wa Kichina alipata mkataba ule baada ya kufuata taratibu zote zilizowekwa na ule ulikuwa ni mkopo wa *Exim Bank*.

Mshauri Elekezi wa mwanzo kulitokea matatizo fulani ikabidi tusitishe mkataba wake ndio baadae aje huyu Mshauri Elekezi kutoka Ufaransa. Mimi napenda kuchukua nafasi hii mbele ya Baraza lako tukufu kumshukuru sana huyu Mshauri Elekezi, katusaidia sana mpaka lile jengo likafika pale na vile vile kuweza kwenda mpaka hatua ambayo sisi tunategemea baada ya jengo lile kumalizika basi tutaleta tija kubwa sana kwa wananchi wa Zanzibar.

Huyu Mshauri Elekezi alitushauri vile vile kwamba lile jengo liongezwe zaidi badala ya kuchukua watu 1,200.000 bali liwe na uwezo wa kuchukua mpaka watu 1,600.000. Kusema la kweli hili ni jambo la kupigiwa mfano na linahitaji pongezi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mshauri Elekezi huyu katusaidia ku-*redesign* ile michoro ambayo waheshimiwa walisema na hivi sasa ile michoro imekuwa ni michoro ya ki-*standard* kabisa na iwapo jengo lile litamalizika basi litakuwa ni jengo la kupigiwa mfano katika Afrika Mashariki.

Mhe. Naibu Spika, niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna nia ya dhati kutaka kuhakikisha kwamba ule mradi unamaliza tena kwa viwango vile vile vinavyotakiwa na vile vile tuhakikishe kwamba kila senti inayotumika pale basi iwe inatumika kwa uadilifu mkubwa sana na hakuna hatua yoyote ile kinyume na sheria yetu ya ununuzi na vile vile uondoshaji wa mali za serikali. Mimi nataka kuwatoa wasi wasi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, uongozi huu uko chini ya Dkt. Ali Mohammed Shein uko imara, uko kufanya kazi kwa ajili ya wananchi na tutahakikisha kwamba tunazitumia pesa zile kwa uadilifu mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nije kuzungumzia suala la mkataba wa uwanja wa ndege. Mimi napenda kuwatoa wasiwasi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuna makosa yamefanyika hapa katika kuandika hii taarifa, lakini mkataba ule upo katika lugha ya Kiingereza na hauna matatizo yoyote. Hapa kitu kilichotokezea ni vipi? Wakati analipwa pesa Mshauri Elekezi yeye alileta barua ya shukurani na kukiri kwamba tayari amepokea pesa za malipo fulani ambazo tarehe hizi zilizotajwa katika ripoti hii. Kwa hiyo, si nyaraka wala si *document* ambayo imeandikwa kwa lugha ya Kifaransa, mikataba yote *AG* anajua utaratibu tunaingia kwa lugha ya Kiingereza.

Mhe. Naibu Spika, sitokuwa na mengi sana kuzungumza kwa sababu hata kesho tuna kamati yetu ya Ujenzi na Mawasiliano, nina imani kubwa sana wajumbe watachangia mengi kuhusu wizara yetu hii na mimi niwatoe wasiwasi kwamba tuko tayari kushirikiana na wao katika kuhakikisha kwamba

tunasukuma mbele gurudumu letu la maendeleo la nchi yetu. Inawezekana iwapo tutatimiza wajibu wetu, iwapo tutafanya kazi kwa pamoja, iwapo tutashirikiana na pale ambapo kutakuwa na kasoro zozote au changamoto nitaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wasisubiri kamati au wasisubiri kuja kuuliza masuala, waje wizarani kwetu tuko tayari kushirikiana nao na kujibu changamoto zao.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ya *PAC* na niwahakikishie kwamba tulikuwa bega kwa bega katika kufuatilia masuala haya yote. Ninawahakikishia mbele ya Baraza lako tukufu tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja na kwa kushirikiana kwa hali ya juu na vile vile niwashukuru sana kwa ushauri wao waliokuwa wakitupa ambao utasaidia sana katika kufanya kazi zetu za kila siku ili yale makosa yaliyotokezea hapa tunakiri, yapo baadhi ya makosa yasijitokeze tena. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufika salama wakati huu na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tumalize salama.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na waliyotuletea hapa. Naomba Mheshimiwa kwa ufupi kabisa niwahakikishie Wajumbe wa Kamati na Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba maelezo kamili ya taarifa ya ripoti hii tutayaleta mwezi wa Septemba. Katika hoja zilizojitokeza katika Wizara yetu ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulikuwa na hoja tisa, kati ya tisa, tatu zilipatiwa jawabu, moja katika hoja zilizokuja zilikuwa zinahusu Wizara ya Biashara na Tawala za Mikoa. Kwa hivyo, nawaahidi kwamba nitazipeleka kwenye wizara zinazohusika na mambo mengine ni ya kawaida nakiri kwamba kunakuwa na makosa ya kibinadamu na sisi tutachukua hatua ya kurekebisha kasoro hizo, wasiwe na mashaka nimuhakikishie Mwenyekiti kwamba sisi tumepokea maelekezo yao na naomba sana kila wakati wanapokuja basi tushirikiane na sisi tutakuwa tayari kushirikiana na wao. Baada ya hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini pili nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni. Nimpongeze yeye na kamati yake yote kwa ujumla kwa kuandika ripoti nzuri ambayo ina maelezo mengi ya kina

nafikiri kwamba itatusaidia sana katika utendaji wetu wa kazi katika mawizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, nitazungumza kwa uchache lakini katika yale maeneo muhimu yaliyoguswa na Waheshimiwa Wajumbe na nianze moja kwa moja na suala la mafunzo kuhusiana na sheria yetu ya ununuzi na uondoshaji wa mali za serikali. Nilisema katika kikao hiki na wajumbe naamini wanakumbuka kwamba ahadi yetu ya kutoa mafunzo kwa watendaji wote wanaohusika na masuala ya ununuzi na uondoshwaji wa mali za serikali yapo pale pale. Ahadi hiyo tutaitekeleza lakini vile vile tutatoa mafunzo maalum kwa Kamati ya *PAC*, tutatoa mafunzo kwa Ofisi ya *CAG* kwa watendaji wake, lakini nilisema kwamba tutatoa mafunzo kwa vyombo vinavyohusika na ununuzi kama *PMU* na *Ministerial Tender Board* zote hizi tutawapatia mafunzo. Wahasibu tutawapatia mafunzo kuhusiana na sheria ya usimamizi wa fedha za umma pamoja na wasaidizi na zile *audit committee*. Kwa hivyo, ahadi hii ipo na *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia tutaitekeleza kama tulivyoahidi.

Lilizungumzwa suala la malipo kwa njia ya *Dummy* na hili lilijitokeza sana katika Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Hili kwanza niseme malipo yote kwa wizara yanafanyika kutumia *Integrated Financial Management System (IFMS)* na hadi sasa *IFMS* inatumika kwa malipo ya *currency* ya *Tanzania Shilling*. Bado hatujaingia katika kuifanya *IFMS* yetu iweze kutumia *currency* mbali mbali, inatumia *currency* ya *Tanzania Shillings*. Na kutokana na hilo malipo yote yanayopaswa kulipwa kwa fedha za kigeni hulazimika yalipwe nje ya utaratibu huu. Kwa mfano, malipo ya wagonjwa wanaopelekwa India yanalipwa kwa fedha za kigeni, yatalipwa nje ya *IFMS*.

Malipo kwa mfano tuliyomlipa *Consultant* wa ujenzi wa *Terminal II Building, ADPI* yamelipwa kwa utaratibu wa nje ya *IFMS*. Kwa hivyo, huo utaratibu sasa ndio unalazimisha kuwekwa hizo *Dummy* katika ule mfumo wetu wa malipo wa *IFMS*, na una faida yake kwa sababu usipoweka *Dummy* inaonekana kwamba malipo yamefanyika lakini nje ya *system*, lakini malipo yale hayatokuwa *reflected* kwenye ile sekta husika na kwa namna hiyo kutakuwepo na *under estimation* ya matumizi ya sekta husika. Kwa hivyo, ile *Dummy* inakuwa ni *conversion* ya fedha zile zile zilizotumika za kigeni ambazo inaingizwa kwenye mtandao wa *IFMS* kwa ajili ya kuweka sawa masuala mazima ya ulipaji.

Kwa hivyo, hilo niliomba sana Waheshimiwa Wajumbe walielewe hivyo, lakini wizara yetu hivi sasa iko katika jitihada za kuufanya mfumo huu uweze

sasa kutumika kwa malipo ya *currency* mbali mbali, yaani uweze kuwa *Multi Currency IFMS*. Kwa hivyo, linafanyika na Mwenyezi Mungu akitujaalia si muda mrefu sana kwa sababu tayari tuna *Consultant* wa kazi hii anashirikiana na wataalamu wetu wa ndani wanalifanyia kazi suala hili ili suala hili liweze kuondoka na tatizo hili liweze kurekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, pia lilizungumzwa suala la *document*. Ni kweli walilikuta hilo Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ni kweli sahihi kabisa *voucher* zilikuwa zipo Wizara ya Fedha lakini zile *original document* zilikuwepo katika wizara zinazohusika. Kwa hivyo, hilo nalo tunalichukua na tutalifanyia marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, suala la ununuzi wa *Jeep SUZA* hili limezungumzwa vizuri sana na namshukuru sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa kusaidia kulitolea ufafanuzi. Lakini na taarifa tulizonazo ni kwamba kweli malipo yamelipwa ya milioni 57,000,000 na yalilipwa kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ilikuwa ni 14,000,000 na ya pili ilikuwa ni 14,000,000 na baadae ni 28,000,000 kila kitu. Kwa hiyo, hizi zimelipwa na sio 3,000.000 kama ilivyozungumzwa na katika kikao hiki.

Lakini tuseme tu kwamba Wizara ya Fedha ndio iliyosimamia masuala ya mnada, masuala mengine yote yalibaki kwa *SUZA* lakini mnada ulisimamiwa na Wizara ya Fedha na kulikuwepo na Kampuni ya *Majembe Auction Mart* ndio iliyosimamia mnada huo.

Suala la *asset register* Mhe. Naibu Spika, ni kwamba suala hili linafanyiwa kazi na Wizara ya Fedha hivi sasa imeshakamilisha kuweka *asset register* kwa wizara tano. Na hizo zilifanyiwa kwa njia ya majaribio kuna Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tayari imeshawekewa *asset register* yake tena *electronically*. Lakini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekamilika, Wizara ya Afya, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Wizara ya Fedha na Mipango. Kinachoendelea sasa hivi ni kuliendeleza daftari hilo la mali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niseme tu kwamba kupitia mradi wa mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma, (*Public Finance Management Reform Program*) ambayo sasa inatekelezwa katika awamu ya tano na inafadhiliwa na wafadhili tofauti ikiwemo Norway, *JAICA*, *DFID* na *World Bank* tunakusudia kuendeleza daftari hili kwa wizara nyengine zote zilizobakia. Kwa hivyo, hili sasa si tatizo. Lakini pili kupitia *program* hiyo hiyo tunakusudia daftari hili liweze kuoainishwa na hii *IFMS* (*Integrated Financial Management System*) ili

kuruhusu Muhasibu Mkuu kuweza kuziona mali za serikali na hasa zimsaidie wakati wa kutayarisha *balance sheet* mwishoni mwa mwaka. Kwa hivyo, yeye sasa tukiziunganisha atakuwa na uwezo wa kujua mali zote za serikali na thamani yake na hivyo kuweza kumsaidia sana katika matayarisho wakati wa kufunga hesabu mwishoni mwa mwaka.

Lakini kupitia *program* hiyo hiyo tunakusudia kutayarisha *Asset Management Policy* sera ya usimamizi wa mali za serikali, na hii itasaidia sana. Lilizungumzwa suala la *depreciation cost* tukiwa na sera hii itatusaidia sana kuweka mfumo mmoja wa matayarisho ya *depreciation cost* kwa mali zote za serikali, na hiyo itaweka uwiano ulio sawa kwa taasisi zote lakini pia utatusaidia katika kufanya tathmini ya mali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, lilizungumzwa suala la kuchelewa kuingizwa fedha katika mfuko wa barabara. Hapa nikumbushe tu kwamba ripoti hii tunayoijadili ni ya mwaka 2013/2014, tatizo hili linaweza likawa lilikuwepo wakati huo lakini kwa sasa tatizo hili halipo tena. Fedha zote zinaingizwa katika mfuko huu kwa wakati, lakini niseme tu ni kweli kwamba fedha zinazoingizwa bado ni chache na hiyo lazima tukiri kwa sababu mahitaji yetu ni makubwa na fedha zinagaiwa katika wizara mbili zinazohusika na masuala ya ujenzi wa barabara zetu. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa asilimia ile ya 85%, lakini Tawala za Mikoa nao wanapata kwa asilimia 15.

Tunajitahidi na naomba Waheshimiwa Wajumbe wote na wananchi tushirikiane katika kuhakikisha mapato yote ya serikali yanapatikana kwa ukamilifu wake, yatakayosaidia kuchochea kukua kwa uchumi wetu na kwa namna hiyo uwezo wa serikali utaongezeka tukifanya hivyo na kwa namna hiyo fedha nyingi sana zaidi zitapatikana kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miundombinu.

Mhe. Naibu Spika, suala la ununuzi wa mitambo kulizungumzwa mitambo ya lami na mitambo ya kutengenezea barabara na ilielezwa kwamba imechakaa. Ni kweli na niseme serikali hivi sasa inachuka juhudi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba tunanunua mitambo ya kisasa kabisa ya kutengenezea barabara ukiwemo mtambo wa lami. Kazi hii tayari tumeshapewa maagizo na tunashirikiana na wenzetu wa wizara inayohusika na hivi karibuni tayari wametupatia *specification* kwa baadhi ya vifaa, tunachoendelea kukifanyia kazi sasa hivi ni mtambo wa kutengeneza lami.

Suala la *Terminal II* nadhani hili limezungumzwa vizuri sana na Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na naomba niiache hivyo hivyo kwa sababu imezungumzwa vizuri sana.

Lipo suala la marejesho ya fedha zinazotumika kupeleka wagonjwa wetu India. Hapa Mheshimiwa lazima niseme kwamba, serikali inafanya hivyo kwa kuthamini wananchi wake, lazima nikiri kwamba ni mzigo mkubwa sana lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein inawajali sana wananchi wake na kwa namna hiyo, pamoja na ugumu na mzigo mkubwa uliopo basi pale inapotokea haja ya kupeleka wagonjwa wetu India linafanyika hilo. Na niseme tu, jana kwa mfano tulihitaji kutumia Dola laki moja sitini na nne elfu (US$ 164,000) kwa ajili ya kupeleka wagonjwa wetu India na kwa mwaka tunatumia karibu shilingi bilioni moja kwa kugharamia wagonjwa wetu kuwapeleka India. Lakini hatuwezi kuwaacha kwa sababu hawa ni vijana wetu, ni ndugu zetu, ni wazee wetu, ni wananchi wetu lazima inapotokea haja ya kufanya hivyo basi ni wajibu wa serikali yoyote iliyo makini kuhakikisha wananchi wake wanapata matibabu bora, ama iwe ndani ama nje. Lakini hii haiondoshi jitihada za serikali za kuimarisha uwezo wetu wa ndani ili kuhakikisha kwamba wagonjwa magonjwa mengi yanaweza kutibiwa humu humu ndani.

Tatizo lililotokea ambalo limezungumzwa hapa kwamba kuna baadhi ya watu wanapewa fedha hizi lakini hawendi kwenye matibabu au hakuna marejesho. Niseme kwamba mwanzoni kabisa Wizara ya Fedha ilikuwa inafanya malipo kwa matibabu ya wagonjwa wetu kupitia mikopo kwa Hospitali ya MIOT iliopo Chennai**.** Lakini mikopo hii ilirundikana sana ikawa mikubwa na wenzetu hawa walivunja mkataba, walisema kwamba tunavunja mkataba hadi hapo deni lote litakapokamilika kulipwa.

Mhe. Naibu Spika, nina furaha kulijuilisha Baraza lako na wananchi kwa ujumla kwamba deni lote lile limeshalipwa na serikali na sasa hivi Hospitali ya MIOT haitudai hata shilingi moja na tuko katika kukamilisha mkataba mpya wa kuhakikisha tunarudi na mfumo wetu ule wa zamani wa kulipa kwa njia ya mkopo. Hii itaondosha sasa wananchi wetu wanaokwenda kule kupewa fedha taslim. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lipo suala lilizungumzwa la mapato yote yanayotokana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa maana ya asilimia 80 yanachukuliwa na Hazina. Niseme tu kwamba, Hazina kwa mujibu wa sheria zilizopo inachukua kodi tu za serikali kwa mujibu wa sheria zilizotungwa na Baraza hili, kodi hizo ni pamoja na *airport service charge*, ada ya usalama, *visa* na ushuru kwa

bidhaa zinazotoka na kuingia kupitia uwanja wa ndege. Lakini ada nyengine zote kwa mfano *landing fee* za kuegesha ndege wanachukua wenyewe, lakini *packing fee* zinachukuliwa na mamlaka, *rent* zote za ndani na nje zinachukuliwa na mamlaka na kwa maeneo haya wana *retention* ya 100%, isipokuwa kwa zile kodi ambazo nimezizungumza. Lakini isitoshe, sehemu ya *sect fee* pia inabakishwa kwa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege.

Hili Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba investment zote zinazofanywa pale zinafanywa na serikali na ni pesa nyingi sana, nikichukua mfano mdogo ujezi wa *apron* ulichukua katibu Dola 57 milioni, lakini ujenzi wa hii *Terminal II building* inayoendelea ni karibu Dola za Kimarekani 128 milioni. Fedha zote hizi zinatokana na serikali na ni mkopo ambao utahitaji kurudishwa. Kwa hivyo, si vyema tukafikiria kwamba wananyang'anywa fedha hizi lakini fedha hizo zinatumika kwa ajili ya kuwa baadae kuja kurudishwa kwa wanaotudai kutokana na *development* iliyofanywa katika kiwango hiki.

Suala la *ZANTEL* na kushuka kwa *share* za serikali. Suala hili linazungumzwa siku zote katika Baraza hili na tukirudia kwenye *Hansard* kuna majibu mengi yametolewa kuhusiana na suala hili na sidhani kwamba majibu hayo yatabadilika. Ni kwamba ili uongeze *share* yako ni lazima pale inapohitajika *investment* zaidi na wewe uongeze mtaji wako, kama huwezi kuongeza mtaji *share* yako haitaongezeka na kama mbiya mwenzako ataongeza *share* zaidi ya kwako itapungua. Kwa hivyo, hili ni suala la kawaida pale tutakapokuwa na uwezo wa kuongeza *share* itakapohitajika kufanyika *investment* basi na sisi *share* yetu itaongezeka, lakini kama hatukuongeza *share* haitoongezeka. Hilo ni jibu liko *straight forward* na *share* yetu ilikuwa mwanzo asilimia 18 imeshuka mpaka kuwa asilimia 15.

Nimeshawahi kutoa majibu kwenye Baraza hili Mheshimiwa kwamba bado hatujapata mgao wa faida na hiyo inatokana na kwamba kwa muda mrefu sana Kampuni ya *ZANTEL* ilikuwa inafanya biashara bila ya kupata faida. Hivi sasa kuna matumaini makubwa kwa sababu hali imebadilika baada ya kuingia *Millicom, Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia hapo tutakapoanza kupata faida basi na mgao wa serikali nao unaweza ukapatikana.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka kuchangia hayo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma. Kwanza nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa

kutujaalia na kutuwezesha kufanya mambo yetu katika Baraza hili tukufu kama tulivyojipangia, tuzidi kumshukuru Mola kwa kutupa uwezo huo.

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati kwa namna ambayo amewasilisha ripoti yake kwa umahiri mkubwa sana, hii ni kuonesha wazi kwamba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wana uwezo mkubwa katika utendaji wa shughuli zao. Aidha, niipongeze sana Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kutayarisha ripoti hii kubwa, nzito na ya kina; lazima tukubali kwamba wamefanya kazi kubwa sana. Aidha, niwashukuru na kuwapongeza sana Wajumbe wenzangu wote ambao wametangulia kuchangia katika hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, kubwa mimi ninalotaka kusema hapa kwa upande wa wizara yetu kwa maana ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tulikuwa na hoja mbili kubwa, moja inayohusu Tume ya UKIMWI na nyengine inayohusu Mfuko wa Jimbo. Kwa ujumla niseme ushauri ambao umetolewa na kamati hii sisi tunaupokea na tutakwenda kuufanyia kazi, maana mengi yalikuwa ni maelekezo ya ushauri kwa hiyo sisi kwa heshima kubwa na unyenyekevu ushauri huo tunaupokea tutakwenda kuufanyia kazi na *In shaa Allah* ikifika mwezi wa tisa basi pale ambapo tunatakiwa kwa mujibu wa kanuni kuwasilisha majibu ya hoja hii tutafanya hivyo kama ambavyo tunatakiwa na kanuni.

Vile vile niseme kwa niaba ya serikali sisi tunaipokea hoja hii yote ambayo imewasilishwa na kamati hii ambapo imefanya kazi nzuri sana ya *PAC*. Mheshimiwa ukitazama historia kadiri ya miaka inavyokwenda ripoti hizi za *PAC* na za Mkaguzi Mkuu utaona kuna mafanikio makubwa sana, kwa hivyo tunapaswa kujipongeza Wajumbe wa Baraza hili tukufu kutokana na ushauri wao na maelekezo yao mbali mbali ambayo serikali imeyafanyia kazi na matokeo yake tumeweza kupiga hatua kubwa, ukilinganisha na ripoti za nyuma na za leo ipo tafauti kubwa sana. Kwa hivyo, tuishukuru serikali, tuipongeze, tuwapongeze watendaji woe kwa kiasi kikubwa walivyotekeleza wajibu wao vizuri na kuweza kufikia hatua kila baada ya mwaka.

Mhe. Naibu Spika, ukiziangalia ripoti nyingi katika nchi zetu za ukanda huu wa Afrika Mashariki utaoa ripoti ya Zanzibar huwezi kukuta ukaona *query* nyingi kulinganisha na nchi nyingi katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Kwa hivyo, tujipongeze sana kwa kazi kubwa lakini sana tumpongeze zaidi Mhe. Rais wetu, kwa sababu kwanza ya uadilifu wake yeye hekima zake, busara zake na uongozi wake ambao zimetoa upeo mkubwa katika kutekeleza wajibu wetu vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Rais kwa hekima zake ameanzisha taasisi mbali mbali ambazo zinasaidia sana kuleta usimamizi mzuri katika masuala mazima ya matumizi ya fedha za umma. Kwa hiyo, ukizitizama taasisi hizo zinapotekeleza wajibu wake, watendaji na Baraza hili tukufu utaona kwamba tumepata mafanikio makubwa na *In shaa Allah* kadiri ya siku zinavyokwenda mbele kwa utaratibu wa namna hii naamini kwamba tunaweza kupiga hatua kubwa zaidi. Hasa ukitizama kwamba kwa asilimia kubwa sasa ya matumizi yetu ya kila siku ya serikali yanatokana na makusanyo yetu ya ndani kwa kiasi kikubwa sana ukilinganisha na misaada ama mikopo kutoka nje. Kwa hiyo, hilo nalo tujipongeze kwa sababu inaonesha wazi namna ambavyo tumesimamia vizuri ile kila aina ya mianya iliyokuwa ikipoteza mapato. Hii ni kuonesha wazi kwamba serikali yetu ni sikivu inafuata taratibu na iko tayari kuendelea kila ambalo shauri linalotolewa na Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi napenda tena nirudie kwa kusema, ripoti hii tumeipokea tutaifanyia kazi na Mwezi wa Tisa Mwenyezi Mungu akitupa uhai na uzima tutawasilisha ripoti yetu ya serikali kutokana na taarifa ambayo tumekabidhiwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuja kufanya majumuisho ya Ripoti ya Kamati ya *PAC.*

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi kwa kuchangia ripoti yetu kwa umakini mkubwa na wamedhihirisha wazi kuwa wamekubaliana na wameungana na mapendekezo ya kamati yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imebahatika kuchangiwa na wachangiaji 42, wachangiaji 20 wamechangia moja kwa moja na wachangiaji 22 wamechangia kwa maandishi. Naomba nichukue fursa hii ya kuwatambua wachangiaji waliochangia moja kwa moja kama ifuatavyo:

1. Mhe. Nadir Abdul-lafit Yussuf
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3. Mhe. Omar Seif Abeid
4. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi
6. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
7. Mhe. Ali Salum Haji (Mnadhimu)

8. Mhe. Asha Abdalla Mussa
9. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
10. Mhe. Shehe Hamad Mattar
11. Mhe. Suleiman Sarahan Said
12. Mhe. Salma Mussa Bilal
13. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
14. Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi)
15. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
16. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum)
17. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
18. Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
19. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
20. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwatambue wachangiaji waliochangia kwa maandishi.

1. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
2. Mhe. Hidaya Ali Makame
3. Mhe. Salma Mussa Bilal pia alichangia moja kwa moja
4. Mhe. Maryam Thani Juma
5. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
6. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
7. Mhe. Hamida Abdalla Issa
8. Mhe. Suleiman Makame Ali
9. Mhe. Mussa Ali Mussa
10. Mhe. Shaibu Said Ali
11. Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei)
12. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
13. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
14. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
15. Mhe. Zaina Abdalla Salum
16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Waziri wa Afya
18. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
19. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
20. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
21. Mhe. Ali Khamis Bakar na

22. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Mawaziri kwa ufafanuzi waliotoa na niungane nao pia kuwa majibu ya ripoti yetu hii ya kamati tutayasubiri mwezi wa Septemba.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba nitoe ufafanuzi tu wa mambo mawili ambayo yaliigusa kamati yangu moja kwa moja. Moja, ripoti ya gari inayohusiana na *SUZA*. Tuliiripoti na maelezo ya ripoti yetu yote yalitokana na wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha *SUZA* maana sisi ndio tuliokwenda kuwaona. Kwa hiyo, tuliyoyaandika mule ndani ya ripoti yetu sio yetu sisi ni yao wao na sisi tumeyaripotia.

Mhe. Naibu Spika, moja tu ndio limegomba katika suala ambalo tulilifuata *SUZA* kama ifuatavyo:

Utaratibu wa sheria ya manunuzi serikalini ya mwaka 2005 Bodi ya Chuo cha *SUZA* haina mamlaka ya kuiandikia barua Wizara ya Fedha. Lakini Bodi ya Zabuni ya *SUZA* ina mamlaka ya kuiandikia barua Wizara ya Fedha kwa mujibu wa sheria ndio inayofanya *disposal* ya mali za umma. Kwa hivyo, tunachokinzana kidogo tu, Baraza la Chuo ambalo kwa sura nyengine Bodi ndio lililoandika barua ya kutaka kufanya *disposal*, lakini sisi tunasema sheria lazima ifuatwe na ichukue mkondo wake. Sheria ya Manunuzi inaruhusu Bodi ya Zabuni ya Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* ndiyo yenye mamlaka ya kufaya *disposal* ya mali za serikali. Kwa hivyo, hili nilisema nilitolee ufafanuzi.

La pili suala ambalo lilizungumzwa na Mhe. Mwakilishi mmoja la utaratibu wa kuzishirikisha Kamati. Kamati ya *PAC* sisi wajibu wetu tunapokwenda hasa katika Mifuko ya Maendeleo ya Majimbo tunakutana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo ndio inaratibu Mfuko huu. Kwa hiyo, tunapokea ripoti ya utekelezaji wa miradi ambayo inaonyesha thamani ya fedha, leo hii kuna Wajumbe wa Baraza hili tukufu wamekana yale ambayo wameyapeleka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, niombe tu na nimnukuu Mhe. Mnadhimu alisema kwamba: "Sheria ni msumeno inakwenda mbele lakini inarudi nyuma, inatugusa sote. Sote naomba kwa ujumla wetu tufuate sheria katika kutekeleza majukumu ya nchi hii".

Mwisho napenda sana kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Maofisa wote wa Serikali ambao kipindi chote cha ziara ya kamati wametupa mashirikiano makubwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, napenda pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya *PAC* kwa kunipa mashirikiano makubwa wakati wote wa ziara ya kamati na kuandaa ripoti hii. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ametoa hoja, wale wanaokubaliana na hoja hizo wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya *PAC*, lakini niwashukuru vile vile Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilish kwa utulivu wao na wale ambao wamechangia vile vile niwapongeze sana kwa kuweza kusaidia katika masuala mbali mbali. Pia niwapongeze na Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi ambao utakaoweza kutusaidia katika kuleta maendeleo.

Waheshimiwa Wajumbe muda uliobaki ni muda mkubwa kidogo kutokana na wakati wetu kulingana na ule ambao kwa kawaida huwa tunamaliza, lakini shughuli zetu tumemaliza leo. Kwanza nitamuomba Katibu kabla ya kuakhirisha aseme kwamba shughuli hizi zimemalizika ili tuweze kuakhirisha kikao hiki mpaka kesho.

Ndugu Fatma Omar Ali: (Katibu Mezani): Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa kwa mujibu wa shughuli zilizopangwa kufanyika katika *order paper* ya leo zimekamilika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru tena na sasa natangaza kwamba, naakhirisha shughuli yetu hii ya leo hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:44 Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 01/032017 Saa 3:00 asubuhi)